Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Tatu - Tarehe 14 Aprili, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 31

**Chumba cha Kuhifadhi Maiti**

**MHE. MARTHA M. WEJJA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali:-

(a) Je Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kujenga jengo kubwa la Kuhifadhia maiti hasa ikizingatiwa kuwa jengo lililopo sasa ni dogo na ni la zamani?

(b) Kama Serikali haina fedha, Je, ni kwa nini isilifanyie marekebisho jengo lililopo na kuwa la kisasa?

(c) Je, Serikali inayo dawa ya kuzuia harufu ya maiti inapokuwa imeharibika ndani ya jengo la kuhifadhia maiti?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Wejja, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hospitali ya Mkoa wa Dodoma inayo majengo mawili yenye majokofu yenye uwezo wa kuhifadhi maiti 18 kwa wakati mmoja.

Hivyo katika hali ya kawaida kuna uwezo mkubwa wa kuhifadhi maiti katika hali nzuri katika hospitali ya Mkoa wa Dodoma kuliko idadi ya maiti zinazohitaji hifadhi kwa wakati mmoja hospitalini hapo.

Kwa sababu hiyo Serikali kwa hivi sasa haioni kwamba ni lazima sana kuwepa mpango wa kujenga jengo lingine kubwa la kuhifadhia maiti katika hospitali ya Mkoa wa Dodoma kwani jengo lililopo linatosha kufanya kazi hiyo iwapo lina vifaa na wataalam wanaotosheleza mahitaji.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mara nyingi Serikali ina mambo mengi ya kufanya kuliko fedha ilizonazo. Pamoja na hayo Serikali imetoa kipaumbele kwa suala la kuhifadhi maiti katika hospitali ya Mkoa wa Dodoma kwa kukarabati jengo moja (1) la kuhifadhia maiti na kujenga uzio wa ukuta ili kutenganisha shughuli za hospitali na chumba cha maiti.

Aidha, Serikali inategemea kuboresha huduma ya hifadhi ya maiti hapo kwa kuongeza sehemu ya kuoshea maiti na kujenga sehemu ya wafiwa kukaa wakati wakisubiri maiti kabla ya kuchukuliwa na kupelekwa kwenye mazishi. Hatua zaidi zitaendelea kuchukuliwa siku zijazo kulingana na uwezo wa fedha.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zipo dawa za kuzuia kupunguza harufu ya maiti lakini kwa kiwango gani dawa hizi zinazuia harufu kwa kiasi gani. Kwa kawaida watu waliofia hospitalini na maiti zao kuhifadhiwa katika nyumba za kuhifadhi maiti, miili yao huwa haiharibiki wala kutoa harufu mbaya. Harufu mbaya hutokana zaidi na maiti toka nje ya hospitali wanaoletwa hapo wakiwa wamecheleweshwa sana na tayari wakiwa wameharibika. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama yafuatayo:-

Kama ipo kweli dawa na kweli amekubali. Lakini anasema inategemea ni wakati gani maiti inakuwa imeharibika.

(a) Je, huwa hakuna mtu/ wataalam ambao wanahusika pale na kwa nini wasiwe tayari kuangalia maiti hii iliyoharibika imeharibika kwa muda gani, na kwa kiasi gani ili waweze kuzuia harufu ya uvundo ndani ya jengo la kuhifadhia maiti. Na hii si kwa Dodoma tu, nazungumzia kwa sehemu zote ambako maiti zinahifadhiwa ikiwemo Muhimbili, Dar es Salaam utakuta maiti inanuka?

(b) Ninasikitika alivyosema kwamba jengo lililopo linafaa. Lakini wakati huo huo amesema kwamba Serikali imetenganisha. Je, wataalam walioko pale wanahusika na maiti huwa ni wataalam au ni watu tu huchukuliwa kufanya kazi hiyo? Kwa sababu jengo la maiti Dodoma ni chafu na ndio sababu hata kama maiti haikuoza lakini bado jengo lile ni chafu.

Je, waliomo humo huwa ni wataalam au wamewekwa tu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Wejja, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza, nimeeleza hapa katika maelezo ya swali hili la msingi kwamba maiti wote ambao wanaotokana na vifo ambavyo vimetokea pale hospitalini katika hali ya kawaida miili yao huwa haina sababu hata kidogo ya kuharibika kwa sababu wanahifadhiwa vizuri. Na kama ni kuwekewa madawa ya kuhifadhi mwili yanawekwa. Tatizo ni pale ambapo maiti anatoka nje ya hospitali, pengine kulikuwa na matatizo na labda matatizo ya vifo vya mashaka, maiti analetwa pale akiwa katika hali ambayo tayari imeshaharibika. Katika mazingira hayo hata kama ungefanya nini dawa ni kuzika maiti huyo mapema iwezekanavyo.

(b) Mheshimiwa Spika, swali la pili. Yako mambo mawili hapa. Jengo lile linaweza kuwa ni chafu na ni suala tu la kiutendaji. Linaweza likasimamiwa na likarekebishwa. Lakini nilichokuwa nasema ni kwamba vyumba vile viwili vya kuhifadhia maiti Serikali inatambua kwamba vinahitaji kufanyiwa matengenezo. Na ndio ikachukua hatua ya kuanzisha kulikarabati jengo moja ili kuhakikisha kwamba tunaendeleza juhudi hizo za kuweka mazingira yale yawe mazuri zaidi. Sasa hilo la uchafu nashukuru tutaliwasilisha. Lakini havihusiani moja kwa moja na juhudi za Serikali za kukarabati majengo haya.

Na. 32

**Lengo la Kuondoa Umaskini**

**MHE. HAMISI J. NGULI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina lengo la kumaliza umaskini ifikapo mwaka 2025 hii ikimaanisha kwamba wakulima na wote waishio Mijini watakuwa na kipato cha uhakika kwa maisha yao:-

(a) Je, dalili hizo za vijana kutoandaliwa taratibu nzuri Vijijini/Mijini juu ya kujitegemea kwa ni kwa namna gani tutaifikia azma hiyo?

(b) Kwa kuwa, kila kukicha vijana wanakimbilia mijini wakifikiri kuwa kuna hali nzuri ya maisha bila kufanya kazi. Je, Serikali haioni kuwa ni ndoto kuifikia azma hiyo bila kurekebisha hali hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - UMASKINI (MHE. EDGAR D. MAOKOLA MAJOGO):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inaweka mkazo mkubwa katika kujenga mazingira bora yatakayowezesha wananchi kupambana na umskini na kuboresha hali ya maisha yao. Sera mbalimbali zimeandaliwa kutoa mwongozo wa kisekta katika utekelezaji wa juhudi za Serikali ambazo zinalenga kuondoa umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. Miongoni mwa sera hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana inayosimamiwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo inayotoa mwongozo na vipaumbele kwa wadau ili kuchangia nguvu katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika sekta mbalimbali.

Sera hii ni chombo muhimu kinachowezesha sekta zinazohusika na maendeleo ya vijana kubuni mikakati na mipango ya kuendeleza vijana.

Jitihada ambazo zimekuwa zikifanywa na Serikali ni pamoja na kuadhimisha Wiki ya Vijana kila mwaka kwa lengo la kuelimishana, kuhamasishana ili kuchochea ari ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla. Ili kuhakikisha kuwa vijana wanajitegemea, Serikali pia inatilia mkazo utoaji wa elimu kwa njia ya vitendo katika taasisi mbalimbali kwa mfano, kuwepo kwa Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)* ambavyo vinatoa stadi za aina mbalimbali kwa vijana wengi ili waweze kujiajiri. Vile vile, Serikali hutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia vijana kupata mikopo ya kuendesha biashara. Kwa mfano, kwa mwaka ujao tunategemea kiasi cha shilingi 500,000,000/= kitakuwa kimeombwa kwa ajili ya kupelekwa katika Halmashauri za Wilaya ili zikopeshwe kwa vikundi vya vijana, kufanyia biashara ndogondogo za kuwaongezea vipato.

(b) Mheshimiwa Spika, Mkakati mpya wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) umezingatia mapungufu yaliyojitokeza siku za nyuma ambayo yanajumuisha kukosekana kwa taratibu nzuri za kuendeleza vijana. Wakati wa mchakato wa mapitio ya mkakati wa awali (MKU) uliopelekea kuandaliwa kwa MKUKUTA, Vijana wenyewe walichambua matatizo na kubainisha mikakati ya utekelezaji. Ilivyo MKUKUTA umeainisha maeneo ya vipaumbele kwa vijana na makundi mengine ya wanaoathirika zaidi na umaskini katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Mipango na taratibu za utekelezaji wa MKUKUTA itaandaliwa, ikijumuisha uboreshaji wa mipango ya vijana iliyopo itakayowawezesha kujitegemea na kuondokana na umaskini. Juhudi hizi zinalenga kuboresha hali ya maisha ya wananchi na hasa vijijini ili kufikia lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa mwaka 2025 la kutokomeza umaskini uliokithiri.

Juhudi nyingine za Serikali zinaendelea za kuinua hali za umaskini vijijini kama vile upatikanaji wa umeme na leo kuna Mjadala kuhusu umeme vijijini, uboreshaji wa huduma za afya, elimu, maji, barabara na kilimo ili kuvutia hasa vijana kubakia vijijini kwa shughuli za uzalishaji mali. Kwa hiyo, Serikali inaamini kwamba kutokana na mipango iliopo ya kuboresha hali ya maisha Vijijini na Mijini na ari ya vijana ya kupata maisha mazuri, malengo tuliyojiwekea ya kuondokana na umaskini uliokithiri yatafikiwa. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri,

kwa kuwa ili kuondoka na umaskini ni lazima watu wafanye kazi na waweze kuzalisha mali ya ziada. Je, pamoja na juhudi zote hizi za Serikali ambazo inazifanya, Serikali haioni upo ulazima sasa hivi wa kutunga sheria ya kumfanya kila mmoja katika nchi hii vijana au watu wa kawaida waweze kufanya kazi kwa ajili ya kuzalisha badala ya wengine kuzurura tu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - UMASKINI (MHE. EDGAR D. MAOKOLA MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Nguli, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza ninampongeza kwa kutambua kwamba sehemu ya umaskini inachangiwa kutokana na baadhi yetu kutokufanya kazi kwa bidii. Nasema ni sehemu tu ya tatizo. Lakini ningependa pia nimhakikishie kwamba tunazo Sheria mbalimbali zinazohakikisha kwamba watu wanafanye kazi.

Kwa mfano, Sheria ya Kuzuia Uzururaji *(Robby and Vagabond)* ambayo kama watu wanazurura Mijini na sehemu zingine wanaweza kuchukuliwa hatua. Lakini mimi ninafikiri Sheria siyo jawabu la matatizo haya, jawabu kubwa ni kujibadilika sisi wenyewe na kupenda kazi. Kwa sababu kama unataka kuondoa umaskini kwa kulazimishwa hufanyi kazi, umaskini hautaondoka. Kwa hiyo, tupige mbio ya kuhimiza kazi kwa bidii na kazi yenye malengo ya kuondokana na umaskini na kuuchukia pia umaskini.

Na. 33

**Hifadhi ya Ziwa Rukwa**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa hifadhi ya mazingira katika Mkoa wa Rukwa na hasa katika bonde la Ziwa Rukwa unahitaji mradi maalumu wa Kitaifa ili kulinusuru ziwa hilo lisitoweke kutokana na kujaa matope yanayoongezeka kwa sababu ya mifugo mingi iliyovamia eneo hilo.

Je, kwa nini Mpango wa Hifadhi ya Ziwa Rukwa, kupitia kwa Wahisani toka nchi za Ulaya usipewe kipaumbele ili kulinusuru ziwa hilo lenye mamba wengi kuliko ziwa lolote barani Afrika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Kimiti kwamba Bonde la Ziwa Rukwa, linakabiliwa na uharibifu mkubwa sana wa mazingira na kwamba uko umuhimu wa

kuchukua hatua. Hii ni kutokana na shughuli mbalimbali za matumizi ya ardhi na maliasili zinazofanyika katika Mikoa ya Mbeya, Rukwa na Tabora, kama vile taratibu mbaya za kilimo kwenye miinuko mikubwa na kukata miti na uvamizi wa wafugaji unaosababisha mmonyoko wa ardhi. Hali hii huchangia ongezeko la tope ambalo hutiririka kwenye ziwa na kuathiri usafi wa maji na kupunguza ujazo wake. Hivyo pana umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa shughuli hizi za maendeleo katika Bonde la Ziwa Rukwa.

Mfumo wa sasa wa Usimamizi na matumizi ya raslimali za mabonde ya maji umegawanyika katika mabonde tisa likiwemo bonde la Ziwa Rukwa. Ofisi ya Bonde la Ziwa Rukwa ni miongoni mwa Ofisi za mabonde tisa nchini iliyoanzishwa rasmi Desemba 2003.

Aidha, Bodi ya Bonde la Ziwa Rukwa iliteuliwa mwezi Mei, 2004. Pamoja na majukumu mengine, Bodi hizi zina jukumu la kupitisha mipango ya Bajeti za kuhifadhi mabonde. Maandalizi ya utekelezaji wa mipango madhubuti ya Usimamizi wa Bonde ni mojawapo ya majukumu katika kusimamia raslimali za maji. Aidha mipango ya utekelezaji itajumuisha masuala ya mazingira yakiwemo yale ya matumizi ya ardhi, maji na maliasili zilizomo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Pamoja na kuanzisha Ofisi ya Bodi ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Rukwa, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuokoa Mazingira ya Bonde la Ziwa Rukwa na kudhibiti uharibifu zaidi usitokee.

Hatua hizo zinazochukuliwa ni pamoja na:-

(a) Kupima Vijiji kwa kuainisha maeneo ya kilimo, malisho, hifadhi ya misitu, maji na kadhalika.

(b) Kuanzisha na kuimarisha Kamati za matumizi ya ardhi.

(c) Kuanzisha rejista za mifugo kwa kila kijiji.

(d) Kuanzisha barabara maalum za kupitisha mifugo.

(e) Kuwaelimisha wafugaji na wananchi kwa ujumla kuhusu taratibu na Sheria husika,

(f) Kuimarisha Usimamizi wa sheria zinazodhibiti mifugo na uharibifu wa mazingira.

(g) Kuhimiza upandaji na utunzaji wa miti.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya umuhimu wa kuhifadhi Ziwa Rukwa, Serikali kwa kushirikiana na wafadhili wakiwemo wa Ulaya, Taasisi na Halmashauri za Wilaya na Miji husika, itaendelea na jitihada zake za kuandaa kutekeleza na kusimamia mipango mbalimbali ya hifadhi za Ziwa Rukwa, ili kulinusuru ziwa hilo na raslimali zilizomo katika ziwa kwa manufaa ya wakazi na wananchi wa eneo la Bonde la Ziwa Rukwa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(1) Mheshimiwa Waziri anakubaliana na mimi ya kwamba athari ambazo zipo kwa sasa ni kubwa ambazo tungeweza kuziingiza katika mpango wa Hifadhi ya Mazingira wakati tunashughulikia pia Hifadhi ya Ziwa Tanganyika tukaenda sambamba na *Lake Rukwa* kwa wakati huo huo mmoja?

(2) Kwa kuwa eneo hili ndicho chanzo kikuu cha chakula kwa ajili ya Mji wa Sumbawanga kutokana na samaki wanaopatikana katika Ziwa Rukwa. Je, Waziri atakubaliana na mimi ya kwamba sasa kazi ifanyike pia ya kupunguza wale mamba walio wengi kwa sababu ndio wanaongeza umaskini kwa wavuvi na samaki wanazidi kupungua ambao ni chakula kikubwa katika Mji wa Sumbawanga?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la Mkataba wa Hifadhi ya Ziwa Tanganyika, tayari umeshasahiniwa na nchi zinazohusika. Na haukuhusisha Ziwa Rukwa, kwa sababu kila Ziwa kwa maana ya raslimali ya maji au Bonde husika unaandaliwa mpango wake. Na kama nilivyoeleza Ziwa Rukwa linatafutiwa utaratibu wa kuwa na mpango wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Rukwa lenyewe.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba mamba wako wengi na wanakula samaki na samaki ni chakula cha binadamu nakubaliana na hilo. Lakini nina hakika Mheshimiwa Kimiti anajua kwamba mamba ni moja kati ya viumbe pamoja na uharibifu wao wanaohesabika kwamba wanatishiwa kutoweka duniani.

Lakini mkataba wa kuhifadhi wanyama hawa ambao wako katika hali ya kutoweka, unapotekelezwa anayetaka kufanya kazi ya kuvuna au kuwawinda mamba hawa, huomba kibali na najua Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii hutoa kibali kuvuna mamba kulingana na idadi inayoruhusiwa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kutoa majibu ya nyongeza kama ifuatayo:-

Kila mwaka tunatoa vibali vya kuvuna mamba. Na kwa kuona matatizo ya mamba nchini, tumeomba vibali zaidi kutoka kwa taasisi inayohusika na tumepewa vibali zaidi katika kuvuna mamba. Kwa hiyo, hilo linafanyika na mahali ambapo kumekuwa na matatizo. Askari wa wanyama pori wamekimbilia katika maeneo haya pamoja na maeneo hayo ya Ziwa Rukwa.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kuna mabonde tisa hapa nchini na ni mabonde machache tu ambayo Mazingira yake yameboreshwa ikiwa ni pamoja na Mabonde ya Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Je, mabonde mengine hayo mipango yake itakamilika lini ikiwa ni pamoja na Bonde la Ziwa Nyasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Luoga, Mbunge wa Binga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, yako mabonde tisa ambayo yameainishwa kwamba yanahitaji kuhifadhiwa mazingira yake. Ni kweli kwamba Bonde la Ziwa Nyasa ni mmojawapo. Najua Mheshimiwa Dr. Luoga anafahamu kwamba upo mpango wa kuhifadhi Bonde la Ziwa Nyasa. Lakini kama lilivyo Bonde la Ziwa Tanganyika, bonde hili linahusisha nchi yetu ya Tanzania, Malawi na Msumbiji. Tumepata tatizo kidogo kukubaliana kwamba kama mazingira ni kipaumbele na mpaka hilo litapokuwa limetatuliwa ndipo tutapata nani wa kusaidia juhudi zetu. Kwa sababu mmojawapo ya nchi ambayo nisingependa kuitaja kwani wao wanasema mazingira si kipaumbele. Na kwa maana hiyo Wahisani wamesita kutupatia fedha kutekeleza shughuli za hifadhi ya Ziwa Nyasa.

Na. 34

**Utengenezaji wa Barabara Nchini**

**MHE. ABU T. KIWANGA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukasimu madaraka yake kwa wakala wanaojitokeza kukarabati/kutengeneza barabara zake chini ya *TANROADS* kwa vipande vipande vifupi ili kuharakisha ukamilishaji wa matengenezo ya barabara hizo kabla msimu wa mvua za masika pamoja na kuhakikisha kuwa wakala hao wanasimamiwa kikamilifu na *TANROADS* kwa utekelezaji wa kazi zao kitaalam na teknolojia kulingana na taratibu za sheria za utengenezaji barabara nchini?

(b) Je, Serikali inaonaje kama itahusisha Serikali za Mitaa moja kwa moja na taratibu za uteuzi wa wakandarasi hao bila kuhusishwa na Usimamizi wa utendaji kazi zilizopo (Wilayani) ambako pia watakuwa washika dau kimaendeleo ya sehemu zenyewe badala

tu ya kuteua mtu yeyote yule na kuwanyima kazi washika dau wa sehemu husika ambao wana uwezo na taalum mbadala na kazi husika?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Abu Towangale Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu kuna makandarasi wa aina nyingi wanaojitokeza kujenga/kutengeneza barabara zilizo chini ya Wizara na hata zilizo chini ya Halmashauri za Wilaya. Makandarasi hawa ni wale wa kigeni na wa ndani ya nchi. Serikali kama msimamizi Mkuu, ina jukumu la kuhakikisha kazi zote zinatekelezwa bila kuathiri sheria na sera zinazoongoza sekta ya ujenzi. Kwa mujibu wa sheria ya manunuzi yaani *Procurement Act 2001* na sera ya nchi kuhusiana na ujenzi, kazi zote zinazohusu kujenga/kutengeneza barabara zinapaswa kutangazwa na kushindaniwa na makandarasi wenye sifa ili kuleta ufanisi katika kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiwanga, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kwa sasa haina mpango wa kukasimu madaraka yake moja kwa moja kwa mawakala mbalimbali wanaojitokeza kujenga/kutengeneza barabara. Utaratibu uliopo ni kuwa miradi yote ya ujenzi/matengenezo ya barabara inayofadhiliwa na wafadhili pamoja na Serikali yetu huratibiwa na Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Ujenzi ndio yenye jukumu la kuitekeleza.

Wakala wa barabara *TANROADS* chini ya Wizara ya Ujenzi, huhakikisha kuwa taratibu zote za kimikataba na kitaalam kwa utekelezaji zinafuatwa. Aidha wakala huhakikisha kuwa barabara zinazojengwa katika viwango vinavyokubalika kwa kuzingatia muda uliopangwa, gharama zilizokubaliwa na taratibu zingine zote kwa mujibu wa sheria.

Anayoyazungumza Mheshimiwa Mbunge ndio hasa yanayofanyika huko kwenye maeneo ya kazi. Mkandarasi kwa mfano aliyepata kazi ya kufyeka nyasi kandokando ya barabara, kufungua mifereji ya maji, kusafisha makalvati na kadhalika. Kwa kuzingatia sera ya Taifa ya kuondoa umaskini huwa anashauriwa kuajiri wanavijiji wa maeneo husika na kuwalipa baada ya kazi kukaguliwa na *TANROADS* na kuthibitishwa kuwa imefanywa kama ilivyopaswa kitaaluma.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa inazo barabara zake na pia hutengewa fedha za Mfuko wa barabara, hivyo nayo huajiri mkandarasi wao wa kufanya kazi zao za barabara kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na sheria ya manunuzi. Makandarasi anaowasema Mheshimiwa Mbunge kuwa ni washika dau, nao wanapaswa wawe wataalam na waliosajiliwa na Bodi ya Makandarasi kwa mujibu wa Sheria Na. (17) ya

mwaka 1997. Hapo ndipo wanapoweza kuajiriwa kufanya kazi kwenye Serikali za Mitaaa. Usajili wa makandarasi ni muhimu ili waweze kuwajibika ipasavyo kufanya kazi iliyo bora, kulinda hadhi na taaluma yao.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na taratibu alizosema za kiserikali zinazofuatwa na wakandarasi walioteuliwa kufanyakazi ya barabara ya Kidatu - Ifakara na wengine kuteuliwa kutengeneza barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mlimba. Mmoja wao alifikisha tu vyombo Chita na kuacha na hajarudi tena pale. Ndio maana nikasema taratibu zingine haziweze kufanywa na Serikali haijachukua hatua yoyote. Je, anasema nini juu ya hilo?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba taarifa hizi tumezipokea na tutazifanyia kazi. Kwa mujibu wa Sheria Na. 17 ya mwaka 1997, Mkandarasi ambaye hatimizi wajibu wake anaweza hata akafungwa miaka mitano jela, akafutiwa leseni yake na pia akapigwa faini ya zaidi ya asilimia 75 ya kazi aliyopewa au vyote kwa pamoja. Kwa hiyo, kwa huyu mkandarasi ambaye katika barabara husika za Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha kwamba Bodi ya Makandarasi *(Contractors Registration Board)* inatumwa kule ili kufanya ukaguzi na kuona haki inatendeka. *(Makofi)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, barabara ya Katoma - Kanyigo tayari imekwishapewa Mkandarasi, na kwa kuwa barabara hiyo haipitiki na Mkandarasi amechelewa kuanza kazi hiyo.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuagiza wahusika kuhakikisha mkandarasi anarekebisha barabara hiyo inapitika na kuongeza kazi ya kutengeza barabara hiyo kwa haraka?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna Sheria ambazo zinawalinda na zinawajibika kwa makandarasi kila anapokiuka taratibu. Lakini pia katika mikataba yoyote ya ujenzi wa barabara huwa kuna mikataba ambayo nayo inatakiwa kuzingatiwa. Barabara anayoizungumza Mheshimiwa Dr. Diodorous Kamala ni barabara inafadhiliwa na *African Development Bank,* na katika mikataba ya kimataifa mara nyingi kandarasi huwa anapewa muda wakuanza kazi ambao unaitwa *mobilization period.*

Kwa hiyo sifahamu kwenye hiyo kandarasi anayoizungumza kama *mobilization period* ya kuanza kazi kwa huyu kandarasi ilikuwa ni miezi mitatu au miezi sita. Kwa hiyo, siwezi nikachukua hatua mpaka nitakapojua mkataba aliopewa mkandarasi wa kuanza kazi ulikuwa ni miezi mingapi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza kwa kuwa kuna wakandarasi ambao wanaotoka nje wana uwezo wa kifedha na teknolojia na kwa sababu ya uzoefu wa muda mrefu, na kwa kuwa makandarasi wa kwetu hawana uzoefu wala hawana pesa za kutosha na Mheshimiwa Waziri amekuwa akisema lazima shughuli zitatolewa kwa sababu ya uzoefu na pesa za kutosha;

Je, Wizara itaendelea na Siasa hiyo na sera hiyo au itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba wanapata pesa na uzoefu wa kutosha ili waweza na wao watanzania kushiriki.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwenye suala la ujenzi wa barabara au la ukandarasi hakuna siasa, pale ni kazi na ni biashara. Kwa sababu Mheshimiwa amezungumza Wizara itaendelea kufanya siasa, hapo hakuna siasa ni kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kueleza hapa si kweli kwamba makandarasi wengi wakizalendo hawana uwezo, makandarasi ambao wamesajiliwa na Bodi ya *Contractor, The Registration Board* kwa mujibu wa sheria Na. 17 ya mwaka 1997. Kwa sasa hivi ni zaidi ya makandarasi 3800 ambao wamesajiliwa. Lakini katika humo ni asilimia 10 tu ya makandarasi wa kigeni ambao wamesajiliwa.

Kwa mujibu wa Sheria za kimataifa na za taifa letu tunawajibika kila kandarasi unapomuweka kazi uhakikishe kazi yako ile nayo inakamilika. Hatupeleki kandarasi kufanya kazi kwa ajili ya kusema huyu ni mzalendo. Lakini hata hivyo kupitia *CRB,* pameanzishwa mfuko wa kusaidia makandarasi wadogo wadogo, na mfuko huo ulizinduliwa rasmi mwaka jana na Mheshimiwa Mkapa na kunazaidi ya bilioni 1 zimepatikana ambapo makandarasi wadogo wadogo kuanzia *group seven, group six* na *group five* wanaruhusiwa kukopa ikiwa ni pamoja na vifaa katika kujiendeleza.

Lakini pia leo kuna mkutano wa makandarasi wote chini ya kata ambao unafanyika Dar es Salaam, lengo ni katika kuwaunganisha pamoja makandarasi ili waanze sasa kuomba kazi kwa pamoja badala ya kuwa wanaomba kazi mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo hizo ni juhudi ambazo zinafanya na Serikali kwa ujumla katika kuwasaidia makandarasi wazalendo, na wala sio siasa kama alivyozungumza Mheshimiwa Mutungirehi.

Na. 35

**Barabara ya Mlowo - Msangano - Kamsamba**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza:-

Kwa kuwa jitihada zetu za kuomba matengenezo makubwa ya kiwango cha Changarawe kifanyike kwenye barabara za Mlowo - Msangano na Mlowo - Kamsamba zinaonakana kushindwa licha ya ahadi kadhaa za Serikali kuhusu tatizo hilo sugu kutotekelezwa.

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani sasa?

(b) Je, wananchi wa maeneo hayo wategemee kutengenezwa kwa barabara hiyo aul la na kama zitatengenezwa ni lini kazi hiyo itafanyika?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Eliachimu Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2001/2002 barabara ya Mlowo - Kamsamba yenye jumla ya km 130 ilifanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwenye kipande chenye jumla ya kilometa 4 kwa gharama ya shilingi milioni 66.582/= katika vijiji vya Itaka na Mwanjelwa.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003 barabara hii ilifanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwenye vipande vyenye jumla ya kilometa 12 kwa gharama ya shilingi milioni 81.286/= kati ya Vijiji vya Halugu, Itaka na Nambinzo Ipapa.

Katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, matengenezo ya muda maalum kwenye vipande vyenye jumla ya kilometa 8.3 yanaendelea kufanyika katika Vijiji vya Zelezeta na Itepula kwa gharama ya shilingi 60.707/=. Pia matengenezo ya sehemu ya kilometa 5 katika maeneo ya Vijiji vya Igamba na njia panda ya *NAFCO* kwa gharama ya shilingi milioni 37.200,074/=

Aidha, ukarabati unaendelea kufanyika kati ya Vijiji vya Mbao na Itumbula kwenye kipande chenye jumla ya kilometa 13.6 ambapo kati ya hizo kipande cha kilometa 6 kitamwagwa changarawe. Kazi hii itagharimu shilingi milioni 75.0/=. Hivyo, hadi sasa jumla ya kilometa 35.3 zimefanyiwa matengenezo makubwa ya kiwango cha changarawe kwa shilingi ya milioni 314.500,043/= katika barabara hii.

Kwa upande wa barabara ya Igamba, Msangano hadi Utambalila, juumla ya kilometa 7 kati ya kijiji cha Malolo na Wasa zinaendelea kufanyiwa matengenezo katika mwaka huu fedha kwa gharama ya shilingi milioni 45.677/=. Aidha barabara hii imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kawaida ambapo jumla ya shilingi milioni 86 zimetumika kuanzia mwaka 2001/2002 hadi 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo kadri Bajeti itakavyoruhusu.

(b) ananchi wa maeneo hayo wategemee kutengenezwa kwa barabara hizo. Aidha, katika Bajeti ya mwaka huu unaokuja fedha za kutosha tutahakikisha tunazitatenga kumalizia sehemu iliyobaki ya kuanzia Kamsamba hadi Ivuma au Itumbura.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa shughuli mbalimbali anazofanya katika Wizara yake.

La pili nataka nimshukuru sana kwa kazi inayofanyika katka kipande alichokitaja. Pamoja na hayo nina maswali mawili madogo.

(1) Pamoja na kwamba barabara zote zimekuwa nyingi za upande wa mwenzangu, lakini jitihada ambayo inafanyika ni nzuri kwangu kidogo. Sasa kuna fedha ambazo nilipewa shilingi milioni 100 katika eneo aliyoitaja, hela ambazo zilitolewa sasa hivi ni 70. Je, zile 30 sasa zilizobaki ili kukamilisha hiyo kazi anaweza kutuahidi kwamba atazitoa katika kipindi hiki ili ikamilishe kazi iliyobakia upande ule?

(2) Kwa kuwa eneo lile la Kamsamba lenye halijapata kuona barabara ambayo imelimwa ingawa inaitwa barabara ya Kamsamba. Je, atatafuta hela za kutosha atusaidie ili safari hii kulima kuanzia Kamsamba kuelekea mpaka Ivuna ili barabara iweze kukamilika na wananchi wangu waweze kuondokana na umasikini? Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Simpasa kwa kazi nzuri anazozifanya katika jimbo lake hasa katika masuala ya kufuatilia masuala ya barabara. Kuhusu maswali yake mawili ya (a) na (b), napenda kumuhakikishia kwamba hizi milioni 30 zilizobaki kwa vile zilikuwa zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu tutahakikisha tunazitoa katika kipindi cha mwaka huu ili ziendelee kutengeneza maeneo yaliyokuwa yamepangwa.

Halafu kuhusu matengenezo ya kutoka Kamsamba kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, nimeeleza katika bajeti ya mwaka huu tutahakikisha tunatenga fedha za kutosha na nataka kumthibitishia Mheshimiwa Simpasa kwamba ujenzi sasa utaanzia Kamsamba kuelekea Ivuna ili sehemu hiyo iliyobaki iweze kukamilika kama ambavyo imepangwa.

Na. 36

**Uuzaji wa Viumbe/Wanyama Hai Nje ya Nchi**

**MHE. DK. THADEUS LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wapo watalii wengine kutoka nje wanakuja nchini kwa lengo la kuona viumbe ambao huko kwao hawaonekani kama vile Wanyama, Mijusi, Nyoka, Vinyonga, Vyura, Ndege wa aina mbalimbali, Wadudu n.k:-

(a) Je, biashara ya kuuza viumbe hai haiwezi kuchangia katika kupunguza idadi ya watalii, hasa wale wenye nia ya kuja kuona hao viumbe hapa Afrika ikiwa wanaweza kutimiza nia yao huko kwao;

(b) Ikiwa biashara ya kuuza viumbe hai nje inapunguza watalii; je isingekuwa vema sasa biashara hiyo ikasitishwa mara moja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Biashara ya kuuza viumbe hai nje ya nchi inafanyika kwa makini na ni kwa baadhi ya wanyama tu. Aina ya wanyama hai wanaofanyiwa biashara ni wale ambalo uchambuzi wa kitaalam umethibitisha kuwa idadi yao haiwezi kuathiriwa na biashara hiyo.

Mbali na hayo, ikumbukwe kuwa watalii wengi kutoka nje wanapenda kuja kuwaona wanyama kwenye mazingira yao ya asili. Licha ya kivutio cha wanyama, watalii hao pia wanavutiwa na vivutio vingine kama mandhari ya nchi, kumbukumbu za kihistoria, pamoja na mila/desturi za makabila mbalimbali hapa nchini na kadhalika.

Aidha, wanyamapori hai wanaosafirishwa kwenda nje ya nchi wanachangia kuitangaza nchi yetu na kuwafanya watalii wengi kupata hamasa ya kuja Tanzania kuwaona wanyama hao katika mazingira yao ya asili.

Kwa misingi hii, hakuna sababu ya kuhofu kuwa biashara ya wanyamapori hai inaweza kuathiri utalii kwa kupunguza idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu. Aidha, ni dhahiri kuwa biashara hii ina faida zaidi kwa wananchi na taifa letu hivyo inapaswa kuendelezwa.

**MHE. PROF. JUMA MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Hapo nyuma kulikuwa na utaratibu wa kuuza ndege, watu walikuwa wanauza mitaani tu ndege wa aina mbalimbali sasa ikaonekana kwa wakati fulani isimame biashara hiyo. sijui mpaka sasa hivi biashara hiyo inazidi kuendelea kwa sababu katika maeneo mengine wanaonekana ndege hao wanateswa sana, na kwamba katika hali hii ya yaonyesha kama sisi tunasaidia ukatili wa ndege hao.

Je, Wizara ina mpango wowote wa kuangalia na kuchunguza suala hilo la ndege wanaoteswa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba huko nyuma kulikuwa na matatizo kama hayo na sio ndege tu lakini pamoja na wanyama wengine kama kima na kadhalika, na Serikali ililiangalia suala hili na hata kuwafungia leseni wale ambao wanashughulika na suala hili.

Lakini nipende kusema kwamba biashara ya ndege huwa pia nayo inauzwa nje ya Tanzania, na imeamuliwa kwamba biashara aina hii hifanywe na watanzania peke yao.

Na. 37

**Mapato Yatokanayo na Utalii**

**MHE. ANATORY K. CHOYA (K.n.y. MHE. OMARI KWAANGW')** aliuliza:-

Kwa kuwa, mapato ya maliasili na Utalii ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu; na kwa kuwa, ni muhimu kuwashirikisha wananchi katika maamuzi ya kutunza mali hiyo na wao kufaidika na mapato yanayotokana na maliasili hiyo:-

(a) Je, uwindaji wa Kitalii umeliingiza Taifa fedha kiasi gani kuanzia mwaka 2000 hadi 2004?

(b) Je, ni kampuni ngapi za Uwindaji wa Kitalii zinamilikiwa na Watanzania wageni, na yale yaliyoingia ubia kati ya Watanzania na wageni?

(c) Je, vijiji vyenye vitalu vya uwindaji wa Kitalii vinahusishwa vipi katika kugawa maeneo hayo na katika maamuzi ya kuteua kampuni au wawindaji wa kitalii katika maeneo yao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Kwaangw Mbunge wa Babati Mashariki lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ugawaji wa maeneo ya uwindaji wa kitalii hufanywa kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Ushauri kwa kugawa vitalu iliyoundwa na Bunge mwaka 1996.

Muundo wa Kamati hiyo unazingatia uwakilishi wa wataalam wa wanyamapori, wanasheria na wananchi kwa maana ya Waheshimiwa Wabunge. Mapendekezo na ushauri wa Kamati hiyo hutumika katika kugawa vitalu kwa kampuni zenye sifa stahili. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi 2004 uwindaji wa kitalii umeliingizia Taifa jumla ya Dola za Kimarekani 46,422 343.00.

(b) Jumla ya kampuni 46 zimeruhusiwa kuendesha shughuli za uwindaji wa kitalii katika maeneo mbalimbali ya uwindaji hapa nchini. Kati ya hizo, kampuni 24 zinamilikiwa na watanzania, 14 zinamilikiwa na wageni na 8 ni za Ubia, kati ya Watanzania na wageni.

(c) Kutokana na maelezo haya, ugawaji wa maeneo ya uwindaji wa kitalii hufanywa kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ya Ushauri wa kugawa vitalu.

Mheshimiwa Spika, kwa vijiji vitakuwa na maeneo ya uwindaji wa kitalii yenye hadhi ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Jamii yaani *Wildlife Management Area (WMA),* ugawaji wa maeneo hayo yaani vitalu utazingatia Kanuni za Uendeshaji *WMAs,* ambapo Umoja wa Jumuiya ya Jamii zilizoidhinishwa yaani *Consortium of Associations* utapanga utaratibu wa kuchagua wawakilishi wawili ambao watajumuishwa kwenye Kamati ya Ushauri wa Kugawa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii mimi na swali dogo la nyongeza. Kwanza nishukuru uwindaji wa utalii unaleta pesa nyingi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Lakini nilikuwa naomba Waziri anipe maelezo hapa; kwamba je, kutakuwa na uwezakano kwa vile vijiji ambavyo vinatunza vitalu vya utalii kuweza kupata kiasi fulani cha pesa kwa ajili ya maendeleo ya vijiji vyao kwa vile na wao wanaangalia shughuli hizo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ndio utaratibu huo unatumika na asilimia 25 ya mapato yote ambayo yanatokana na utalii yanakwenda kwenye Halmashauri ili kuendeleza Halmashauri hizo kwa vijiji vile ambavyo vinapakana na vitalu vya uwindaji wa kitalii.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Je, Serikali inatambua kwamba baadhi ya watalii, wawindaji wa kitalii, huwa wanaua wanyama kwamba maana yake ni mahali pengi wanafanya hivyo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, pale ambapo wawindaji wa utalii wanakwenda kuwinda basi wanapewa *quarter* ya wanyama wa aina gani ambao wana winda. Kwa mfano labda simba wanaweza *pay quarter* labda simba watano au sita na kadhalika, na hii pamoja na tembo.

Hii inaandikwa kwenye karatasi maalum, na hii karatasi ndio ambayo kwa kweli huyu mwindaji ndio anakwenda nayo, lakini pamoja na hayo kuna utaratibu wa maafisa maliasili kwa maana afisa wa wanyamapori katika maeneo hayo kuhakikisha kwamba wale wanaowinda wanawinda wanyama hao tu. Kwa hivyo hilo linafanyika na tumekuwa tunafuatilia kwa karibu sana. Mahali ambapo kunatokea na matatizo yoyote tumekuwa

tunafuatilia, na nisema kwamba kwa sababu ya ushikirishwaji wa wananchi jambo hili limesaidia sana katika kudhibiti uwindaji holela katika maeneo yetu.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kunipatia nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba kuna Kamati ya ugawaji wa vitalu ambao ndani yake kuna wawakilishi wa maeneo ambayo vitalu hivyo viko;

Je, kuna utaratibu wowote wa hawa wawakilishi kuwa na *rotation,* kwa sababu hivi vitalu vipo katika sehemu nyingi tu Tanzania, na sisi Manyoni nafikiri tunavyo vinne.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Kamati hii ambayo niliyozungumzia ni Kamati ya kitaifa, na kama vile Bodi, kwa mfano Bodi za kitaifa kwa mfano unachakua labda *TANAPA* na kadhalika.

Kwa hiyo, hii ni Kamati ya kitaifa na pale ambapo inakwisha muda na kuweza kuteuliwa Kamati nyingine basi uwezakano unakuwepo wa kuweka wajumbe wengine.

Lakini katika suala la *rotation* hili ambalo unazungumza la vijiji, nimeeleza hapo mwanzo kwamba mahali ambapo tutakuwa na *DWMS* basi wananchi wenyewe katika maeneo yao watachagua viongozi wawili ambao watakaa kwenye Kamati hii ya kitaifa ya ugawaji.

Na. 38

**Mahakama ya Kimataifa ya Kesi za Jinai**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa yapo mawazo ya kuanzisha Mahakama ya kimataifa ya kushughulikia kesi za jinai na kwamba makao yake yawe *The Hague International Criminal Court , (At The Hagu):-*

(a) Je, kuna tofauti gani kati ya Mahakama itakayoanzishwa na ile iliyopo hivi sasa huko, *The Hague;*

(b) Inasemekana kuwa nchi ya Marekani *(USA)* inafanya kampeni ili Mahakama hiyo itakapoanza kufanya kazi, askari wake watakaokuwa wamefanya makosa ya kivita wasishitakiwe katika Mahakama hiyo. Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo? Kama ina ukweli ndani yake kwa nini wametofautisha na askari wengine wanaofanya makosa ya aina hiyo?

(c) Kwa kuwa, inasemekana kuwa nchi 69 wameshakubali kuweka saini makubaliano kati yao na Marekani ili kuweka kinga ya kutoshitakiwa, na miongoni mwa nchi hizo,

nchi 26 ni za Kiafrika. Je, Tanzania ni miongoni mwa nchi 26 za Kiafrika? Kama ni hivyo, Je, ni lini Bunge letu liliridhia Mkataba wa Makubaliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye vipengele (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:

Itakumbukwa kwamba Jumuiya ya Kimataifa, kwa muda mrefu, imekuwa ikitafuta njia bora ya kuwa na mahakama ya kudumu ambayo itashughulikia makosa makuu ya jinai kama vile mauaji ya halaiki *Genocide,* makosa dhidi ya binadamu *Crimes Against Humanity,* makosa ya kivita *War Crimes* na makosa ya uchokozi wa kutumia nguvu *Aggression.* Hoja imetokana na ukweli kwamba matukio ya makosa hayo yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku duniani. Kwa ajili hiyo Umoja wa Mataifa uliitisha mkutano maalum wa kuzungumzia kuanzishwa kwa Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya jinai. Mkutano huu ulifanyika mjini Roma Italia, tangu tarehe 1 Juni hadi 17 Julai, 1998, na kupitisha Mkataba wa Roma wa kuanzishwa Mahakam hiyo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilishiriki kwa ukamilifu katika Mkutano wa Roma na tulitia saini Mkataba huo tarehe 31 Desemba, 2001 kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa mjini New York.

Bunge lako Tukufu liliridhia Mkataba wa Roma tarehe 1 Agosti, 2002 na hati za kuridhia kwetu Mkataba huu ziliwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa tarehe 20 Agosti, 2002. Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi wanachama wa mwanzo kuridhia Mkataba wa Roma wakati ulipoanza kutumika tarehe 1 Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Msindai Mbunge wa Iramba Mashariki lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Tofauti ya Mahakama hii ya Jinai na Mahakam Kuu ya Kimataifa ipo katika masuala inayoshughulikia. Mahakama hii ya Jinai, inashughulikia makosa makuu ya jinai kama nilivyoyaorodhesha katika utangulizi.

Wakati mahakama ya kimataifa iliyoko *The Hague* inashughulikia kusuluhisha migogoro ndani ya mataifa kwa masuala mbali mbali na migogoro baina ya Mataifa kama vile migogoro ya mpaka. Kwa ujumla mataifa ya wanachama wote wa Umoja wa Mataifa ni wanachama wa Mahakama Kuu ya Kimataifa.

Lakini sio hivyo kwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai, ni mataifa 98 tu miongoni mwa taifa 191 ya Umoja wa Mataifa hadi sasa ndio wanachama wa mahakama hiyo.

(b) Ni kweli kwamba Marekani imekuwa inazishawishi nchi kahaa, wanachama na zisizo wanachama wa Mkataba wa Roma, zikubali kwamba askari wa Kimarekani wanapofanya makosa yaliyo kwenye mamlaka ya Mahakama ya Jinai ya Kimataifa wasishitakiwe katika Mahakama hiyo.Hii inatoka na ukweli kwamba kwa mujibu wa Sheria za Marekani ni mwiko kwa askari wa Marekani kushitakiwa na mamlaka yoyote isiyokuwa ya kimarekani.

(c) Ni kweli kwamba zipo baadhi ya nchi zimekubaliana na kutia saini na Marekani kwa utekelezajwi wa mpango wa mikutano hayo. Lakini Tanzania siyo miongoni mwa nchi hizo na wala haitakuwemo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Je, na sisi Tanzania hatuwezi kuanzisha Sheria ambao askari wetu hawatashitakiwa nje ya Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, sisi Mahakama ya Kimataifa ya Arusha ya jinai imeanzishwa kwa sababu tu pale ambapo nchi husika inaposhindwa kwa makusudi au kwa sababu tofauti ile kuwachukulia hatua wale ambao wamefanya makosa haya ndani ya nchi zao.

Lakini kama nchi yenyewe inautaratibu wa kuchukua hatua hizo Mahakama ya Kimataifa watu wale hawawezi kufikishwa huko. Tanzania sisi hatukubali kufishwa hapo kwamba mpaka mtu wetu akifanya kosa hilo akafikishwa Mahakama ya Kimataifa, tutawahukumu hapa hapa ndani. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, pia nampongeza Waziri kwa majibu ya kina kuhusu suala hili. Sasa swali lingine la nyongeza, kwa vile baada ya kuundwa kwa Mahakama ya Kimataifa ya makosa ya jinai.

Sasa haya mabaraza ya muda ya umoja wa mataifa ya makosa ya jinai kama yale ya Ruanda yalikuwa Arusha na yale Australia yaliyoko *The Hague* sasa yatakwisha na mashauri yatashughuliwa na mahakama haya ya kudumua.

Je, Serikali ya Tanzania inafanya jitihada gani za kidiplomasia ili Arusha ambapo Umoja wa Mataifa umewekeza sana katika baraza hili la Ruanda pia iwe sehemu ya mahakama ya umoja wa mataifa ya makosa ya jinai?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mahakama mbali mbali zilianzishwa moja wapo ikiwa ya Arusha kuhusu makosa ya jinai kwa Ruanda na mahakama nyingine iliyoanzishwa ya makosa ya jinai kule Sierra Leon na kadhalika.

Lakini tuelewe kwamba mahakama hizi zilianzishwa wakati ambapo mahakama ya kimataifa ya jinai ilikuwa bado haikuanzishwa, ndio zikaanzishwa hizi. Sasa mahakama hizi zimepewa muda wake maalum kwamba ikifika muda ule mahakama ile inasimamishwa.

Lakini mara nyingi inakuwa mpaka imalize zile kesi zilizopo, kwa hiyo hatutazamii kwa mfano mahakama ya kimataifa iliyokuwepo Arusha kusita kufanya kazi zake kwa sababu kesi nyingi zitakuwa bado zipo, hatutazamii hivyo.

Lakini kwa vile sasa kumeshaanzishwa mahakama ya kimataifa kwa makosa ya jinai, kimsingi makosa kama hayo yakitokea yanawekwa chini ya mahakama ile.

Lakini haina maana kwamba kila kosa au kesi zake lazima zikasikilizwe *The Hague,* ndani ya mkataba huu wa Roma, inaeleza wazi wazi kwamba makao hii ya makao makuu tu ya mahakama hii ndio watakuwa *The Hague,* lakini usikilizaji wa kesi mbalimbali ni mahakama inaweza ikaamua ikafungue wapi mahakama ya kusikiliza kesi hizo.

Sasa inawezekana sana kwa vile mahakama ya jinai iliyokuwepo Arusha inasimamia mambo ya Ruanda, inawezekana sana kwamba katika kurahisisha usikilizaji wa kesi hapo baadaye itakapofika kwamba kesi za Ruanda kwa mfano zikaisha na ikawa kuna kesi zingine za nchi jirani katika maeneo yetu haya iwe ndani ya Afrika nzima inawezekana sana kwa umoja wa mataifa kupitia mahakama yake ya jinai ikaamua kwamba kwa sababu kuna miundo mbinu hapa Arusha ikaendelezwa upo uwezekano.

Mheshimiwa Spika, sisi kama nchi na kama Serikali tupo tayari siku zote wakiamua. Hivyo kurahisisha zaidi kwamba mahakama ile iendelee kuweza kukidhi haja kama hizo siku za usoni. *(Makofi)*

Na. 39

**Mikataba Mbalimbali Inayoletwa Bungeni**

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa ni kawaida ya Serikali kuleta Bungeni Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa huku tayari ikiwa imeweka saini:-

(a) Je, ni Mikataba mingapi iliyofikishwa Bungeni kwa utaratibu huo tangu mwaka 2000?

(b) Je, Bunge limewahi kukataa kuridhia Itifaki au Mkataba wowote ambao Serikali ilikwishaweka saini tangu utaratibu huo wa kuridhia na Bunge ulipoanzishwa?

(c) Je, ni nini kitatokea ikiwa Itifaki au Mkataba uliosainiwa na Serikali utakataliwa kuridhiwa na Bunge?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Msekela Mbunge wa Tabora Kaskazini, naomba kutoa maelezo ya jumla yafuatayo:-

Nchi yoyote, kama sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa, inao uwezo wa kuingia mikataba na nchi nyingine au Jumuiya za Kimataifa na ni jukumu la nchi hiyo kuyatekeleza majukumu yake chini ya mikataba hiyo. Mikataba ya kimataifa inazo hatua mbili zinazohitajika kuzingatiwa kabla mikataba hiyo haijaanza kutekelezwa. Hatua ya kwanza ni mikataba hiyo kusainiwa ili kuthibitisha kwamba yaliyomo katika mkataba ndiyo yaliyokubalika na pande husika na hatua ya pili ni mikataba hiyo kuridhiwa.

Kila nchi inao utaratibu wa namna ya kuridhia mikataba mbalimbali. Zipo nchi ambazo uridhiaji wa mikataba hufanywa na mamlaka ya utendaji executive na zipo nchi nyingine, kama ilivyo Tanzania, ambazo kikatiba uridhiaji hufanywa na mamlaka ya kutunga sheria legislature. Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba inaelekeza kwamba mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa basi itaridhiwa na Bunge.

Kwa kuzingatia mgawanyo wa madaraka tuliona nchini, jukumu la kuingia katika mikataba mbalimbali, ikiwemo ile ya kimataifa, ni jukumu la mamlaka ya utendaji. Kwa hiyo, ni wazi kwamba mara zote hatua ya kwanza kama nilivyoieleza, itafanywa na mamalak ya utendaji na hivyo hata utiaji sahihi wa mikataba hiyo utafanywa na mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Tangu mwaka 2000 mikataba 98 iliwasilishwa Bungeni na Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba kwa kuridhiwa. Kwa kuzingatia taratibu kama nilivyozieleza, ni wazi kwamba mikataba yote iliyofikishwa Bungeni kwa kuridhiwa ilikuwa tayari imewekwa sahihi na Serikali.

(b) Bunge halijawahi kukataa kuridhia Itifaki au Mkataba wowote wa Kimataifa ambao Serikali ilikwishaweka saini. Hii inathibitisha kwamba mikataba yote hiyo huwa imezingatia ipasavyo maslahi ya Taifa.

(c) Mkataba au Itifaki iliyosainiwa na Serikali ikikataliwa kuridhiwa na Bunge maana yake ni kwamba hautakuwa na nguvu yoyote ya kisheria na nchi haitabanwa na masharti ya mkataba huo.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kwa maelezo ya Mheshimiwa *Attorney General* inaonekana kwamba mipaka ya kuweka au nguvu ya kuweka sahihi Mkataba na Serikali, na nguvu ya kuridhia Mkataba na Bunge haijaonekana mipaka yake iko wapi na kwa sababu baada ya kuweka sahihi Mikataba hii hupelekwa huko kunakohusika.

Je, Serikali haioni kwamba ingekuwa vema basi Mikataba hii ikawekwa sahihi na Serikali baada ya Bunge kujadili na kuridhia, kwa sababu huwa kuna muda wa majadiliano ndani ya Serikali kabla ya sahihi. Basi muda ule vile vile ungetumika kwa kuuleta Bungeni Mikataba hiyo ili iweze kuridhiwa na Bunge kabla ya kuwekewa sahihi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA):** Mheshimiwa Spika, neno kuridhia nikisema kwa kiingereza to ratify, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi ni kwamba unathibitisha kile ambacho kimewekewa saini. Ndio maana Serikali inapokuja Bungeni haiwezi ikaleta kitu ambacho inaomba kuridhia ambacho hakijawekewa saini na Serikali. Huo ndio utaratibu wa Nchi zote kwa masuala haya ya Mikataba. Kwamba hatua ya kwanza Serikali itafanya shughuli hiyo ya kuridhia kwa sababu ndio jukumu la haki ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, na Bunge hili kwa sababu ndio linasimamiwa utekelezaji wa shughuli za umma, sasa ndio linafanya hiyo kazi ya kuridhia. Linaweza likaridhia au likakataa kuridhia na kama nilivyoelezea ikitokea hivyo maana yake ndio nini. Kwa hiyo, Bunge bado lina nafasi kubwa sana ya kusema kwa haya mliyoyafanya sisi hatukubali tunawanyima idhini ya kuridhia Mkataba huo.

Na. 40

**Ruzuku kwa Kilimo cha Tumbaku - Mpanda**

**MHE. LEPHY B. GEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa zao la Tumbaku limekuwa likilimwa Wilayani Mpanda kwa miaka mingi tangu mwaka 1970 hadi sasa kama zao kuu la biashara na kwa kuwa kutokana na ukweli huo. Ni dhahiri kwamba wakulima wa zao hilo watakuwa wamechangia kwa kiwango kikubwa kukuza uchumi wa nchi hii.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kutoa ruzuku kwa wakulima wa zao hilo ili waweze kuboresha kilimo na hatimaye kuinua kipato cha pato la Taifa kwa ujumal.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lephy Benjamini Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Mpanda inalima tumbaku kwa wingi. Kwa msimu wa 2003/2004 wilaya ya Mpanda ilizalisha kilo 4,234,785 za tumbaku ya mvuke na kuifanya wilaya hiyo kuwa ya nne katika uzalishaji wa tumbaku nchini. Serikali inatambua mchango wa wakulima wa tumbaku wa Mpanda katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa Taifa na inawapongeza kwa mafanikio waliyoyapata.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kutoa ruzuku ya kufidia sehemu ya gharama za kusafirisha mbolea ulianza mwaka wa 2003/2004 kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana, Serikali iliamua kuongeza kiwango cha fedha kilichotengwa kwenye bajeti kutoka shilingi bilioni 2.0 za mwaka wa 2003/2004 hadi shilingi bilioni 7.244 kwa mwaka wa 2004/2005 na kupanua mpango huo kujumisha nchi nzima, ikiwa ni pamoja na wilaya ya Mpanda. Kilimo cha tumbaku hutumia mbolea aina ya *NPK 10:18:24.* Serikali inafidia asilimia 75 ya gharama za kusafirisha mbolea hiyo hadi vituo vikuu vya kupokelea mbolea, ambavyo kwa Mpanda ni Tabora na Sumbawanga. Katika mwaka wa 2004/2005 wilaya ya Mpanda imetengewa tani 3,320.5 za mbolea za tumbaku na hadi tarehe 9 Aprili, 2005, tani 3,265.5 za *NPK 10:18:24* na kupanua mpango huo kujumuisha nchi nzima, ikiwa ni pamoja na wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuendelea kutoa ruzuku kwenye mbolea katika mwaka wa 2005/2006 ili kumwezesha mkulima kupata mbolea kwa bei nafuu na kumwezesha aongeze matumizi ya mbolea. Wakulima wa tumbaku wa Mpanda watafaidika na mpango huu.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu, kwa kuwa makampuni binafsi ambayo yananunua tumbaku wameamua kuunda chombo kinachoitwa *ATTT,* na hicho chombo kuonekana kinapanga bei kinavyotaka na Serikali kutokuweza kuingilia kati suala hilo. Kwa sababu *TTB* wapo kwa ajili ya ku-oversee kama chombo kinachowatetea wakulima, lakini *TTB* inaonekana kumezwa na *ATTT.*

Je, Serikali inasemaje kuhusu udhaifu huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kisheria *TTT* haitakiwi iweze kuwa na mamlaka ya kufanya shughuli za aina hii. Masuala yote yanapangwa na wale wanaohusika na zao hili na kusimamiwa na *TTB*. Sasa nimepata taarifa tutafuatilia, lakini ni marufuku kwa *TTB* kufanya shughuli hizi. Hapo Hapo lakini napenda kusisitiza, mkulima ana uhuru wa kuchagua wapi kununua mbolea na ninapenda kupendekeza wafuate mbolea zile zenye ruzuku ambazo Serikali inatoa bei ya nafuu au *serving charge* kwa asilimia 75.

Na. 41

**Baa la Panya Mikoa ya Lindi na Mtwara**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mikoa ya Lindi na Mtwara ilikumbwa na panya katika msimu wa 2004/2005; na kwa kuwa, panya hao walifanya uharibifu mkubwa kuanzia mbegu, mimea hadi mazao yaliyokuwa mashambani:-

(a) Je, Serikali imefanya tathmini ya uharibifu huo na kwa kiasi gani katika baadhi ya sehemu za Mikoa hiyo zimeathirika?

(b) Kwa kuwa baa hilo linaweza kusababisha maeneo husika kukumbwa na njaa; je Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na hali hiyo?

(c) Kwa kuwa baa hilo limekuwa likitokea mara kwa mara bila udhibiti unaofaa kwa wakati. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzuia janga hilo kuliko kutibu ili kupunguza athari zake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula ilipokea taarifa juu ya kuwapo kwa milipuko ya panya katika Mikoa ya Lindi na Mtwara katika mwezi wa Novemba 2004. Tathmini iliyofanywa na Wizara ilionyesha kwamba wilaya zote za mkoa wa Lindi na Wilaya ya Masasi, katika Mkoa wa Mtwara, zilikuwa zimepatwa na baa hilo. Jumla ya vijiji 155: vijiji 133 katika Mkoa wa Lindi na vijiji 22 katika Wilaya ya Masasi vilikuwa vimeathirika.

Katika Mkoa wa Lindi, inakisiwa kwamba hekta 61,620 zilikuwa zimepandwa mahindi na hekta 510, sawa na asilimia 0.83 zilikuwa zimeathiriwa na panya. Katika Mkoa wa Mtwara hekta 105 sawa na asilimia 0.3 ya hekta 82,000 zilizolimwa mahindi na mtama ziliathiriwa na panya.

(b) Mheshimiwa Spika, kiasi cha athari kinachotokana na milipuko ya panya katika Mikoa ya Lindi na Mtwara katika msimu wa 2004/2005 ni kidogo na hakiwezi kuwa sababu ya Mikoa hiyo kukumbwa na njaa. Hata hivyo, Serikali imechukua tahadhari ya kujikinga na njaa. Hadi mwezi wa Januari, 2005 Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilikuwa na tani 125,464 za mahindi. Hiki ndicho kiasi kikubwa cha chakula kilichowahi kuhifadhiwa tangu Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilipoanzishwa mwaka wa 1991.

Aidha, Wizara ina utaratibu wa kudumu wa kufuatilia kwa karibu mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao mengine. Katika maeneo yaliyoathiriwa na mashambulizi ya panya wakulima walihimizwa kupanda mazao ya chakula upya,

walisaidiwa tani mbili za mbegu za mahindi, mtama na ufuta na tathmini iliyofanywa mwezi wa Machi, 2005 ilionyesha kwamba asilimia 80 ya mazao yaliyopandwa upya yalikuwa yamebeba mbegu na asilimia 20 yalikuwa katika hatua mbali mbali za kukua.

(c) Mheshimiwa Spika, tatizo la milipuko ya panya katika Mikoa mingi ya Tanzania Bara linatokana na mifumo ya kilimo ambayo inawawezesha panya hao kuongezeka kwa kasi kubwa. Panya huzaliana kwa kasi kwenye maeneo yenye chakula chao, ambacho ni mbegu za manyasi na maficho ya kuwahifadhi dhidi ya maadui wao, kama bundi na nyoka. Katika Mikao inayoathiriwa sana na panya , kilimo ni cha kuhamahama na cha vishamba vidogo vilivyozungukwa na vichaa ambavyo vinawapatia panya chakula na hifadhi.

Aidha, wakulima wengi, hawachukui na kutumia dawa ya kuulia panya. Ili kuthibiti milipuko ya panya, inabidi uwekwe utaratibu wa wakulima kulima mashamba makubwa na kuhakikisha kwamba eneo lisilopungua upana wa meta 10 kuzunguka mashamba limesafishwa.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa panya hao bado wapo na wanaendelea na uharibifu wa mazao mashambani na majumbani.

1. Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka katika kuwaangamiza panya hao ili kunusuru mazao yaliyobakia?

2. Kwa kuwa sehemu kubwa ya mazao imeathirika kutokana na janga la panya na wanyama waharibifu hasa katika Jimbo langu la Nanyumbu. Je, Serikali ipo tayari kushirikiana na Serikali za Vijiji kufanya tathmini ya kina ili kubaini uharibifu uliotokea na kutoa msaada ambao unahitajika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya mawili ya Mheshimiwa Aridi Uledi, kama ifuatavyo:-

Tunatambua tatizo hili, ni kweli ikitokea linakuwa adha kubwa sana. Nakumbuka wakati fulani nilifika Wilaya fulani katika maeneo hayo hayo panya walikuwa na ujasiri wa pekee. Wakati unamega ugali kabla haujaingia anakuja kuchukua tulishangazwa sana. Sasa tunachoomba ufanywe utaratibu kuhusu utaratibu kushirikiana tu, sisi na vijiji, Wilaya na Mkoa. Tupewe hasa ukubwa wa tatizo hili tupo tayari, hivi tumejiandaa kungojea kuna kitengo maalum kushughulikia shughuli hii.

Kwa hiyo, tushirikiane tukiwa hapa Bungeni tuweze kulikabili tatizo hili la mapanya wanaochupa na kuharibu hata matonge ya ugali kabla hayajaingia mdomoni. *(Makofi)*

Na. 42

### Mpango wa Uboreshaji Huduma ya Maji

**MHE. DR. HASSY H. B. KITINE** aliuliza:-

Je, ni vijiji vingapi kwa majina vimo katika mpango wa Uboreshaji na uenezaji wa huduma ya maji katika awamu zote mbili katika Wilaya ya Makete?

**NAIBU WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Hassy H.B. Kitine, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Wizara yangu inasimamia utekelezaji wa Mradi wa Maji Vijijini unaofadhiliwa kwa mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Utekelezaji wa Mradi huu ulianza katika Wilaya tatu za Kilosa, Mpwapwa na Rufiji mwaka 1999 na kwa sasa unatekelezwa katika jumla ya Wilaya 12 hapa nchini. Wilaya hizo ni Rufiji, Kilosa, Mpwapwa, Morogoro, Kongwa, Kiteto, Kondoa, Manyoni, Singida, Iramba na Igunga.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwezi wa Aprili na Mei 2004 Wilaya zote nchini ikiwemo Wilaya ya Makete zilishiriki katika warsha ya uandaaji wa mipango ya awali ya utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Sambamba na hatua hii, mwezi Novemba na Desemba 2004, Wizara ilituma wataalam katika Wilaya zote nchini isipokuwa zile 12 za mradi, kupata orodha ya miradi midogo ya maji ambayo haihitaji usanifu na ambayo inaweza kutekelezwa kwa haraka kwa lengo la kupunguza kero ya maji kwa wananchi. Orodha na maelezo ya miradi husika imepatikana na katika Wilaya ya Makete vijiji vinne vilivyoainishwa katika mpango huu wa Uboreshaji na uenezaji wa huduma ya maji ni Isapulano, Ilevelo, Ipelele na Luvulunge.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji uliopendekezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Makete katika kijiji cha Isapulano chenye wakazi wapatao 1,781 umekadiriwa kugharimu shilingi milioni 40.6 kwa kutumia chanzo cha maji cha Mto Lwamalo. Mradi wa maji uliopendekezwa katika Kijiji cha Ilevelo chenye wakazi wapatao 586 umekadiriwa kugharimu shilingi milioni 42.8 kwa kutumia chanzo cha maji cha mto Ilevelo.

Mradi wa maji uliopendekezwa kufanyiwa ukarabati katika Kijiji cha Mlo Ilevelo. Mradi wa maji uliopendekezwa kueanyiwa ukarabati katika cha Ipelele chenye wakazi wapatao 3,123 umekadiriwa kugharimu shilingi milioni 9.6 kwa kutumia chanzo cha maji cha mto Kitulo; na mradi wa maji uliopendekezwa kukamilishwa katika kijiji cha Luvunge chenye wakazi wapatao 598 umekadiriwa kugharimu shilingi milioni 8.9 kwa kutumia chanzo cha Mto Mwapima.

Hivi sasa Wizara inawasiliana na Benki ya Dunia kuhusu utekelezaji wa programu hii ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Maandalizi ya programu hii yanaendelea vizuri na utekelezaji wake utaanza katika mwaka wa fedha 2005/2006 baada ya kukamilisha na kutiwa saini mkataba wa mkopo laini wa Benki ya Dunia.

**MHE. DR. HASSY H. B. KITINE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Sasa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza katika vijiji vya Wilaya kuna Vijiji 98 na katika mpango huo Vijiji vinne ndio vimetamkwa kama vimo katika mpango ambao ni mpango unaoendelea sasa hivi. Nitashukuru kama nitapata majina ya Vijiji vingine ambavyo mpango huo unavyoendelea, yaani Vijiji vingine zaidi ya hivyo vinne.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mahakama Kuu ya Wilaya pana huduma ya maji, lakini huduma hiyo kwanza maji yanakatika mara nyingi, pili yanaenda kwa mgao, sasa sijui Serikali ina sema nini juu ya tatizo hilo?

**NAIBU WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Dr. Hassy H.B. Kitine, kama ifuatavyo:-

Mpango huu wa huduma ya maji na Uboreshaji wa mazingira Vijijini unaendeshwa kwa utaratibu wa ushirikishi, ambako Wilaya zilishirikiana na Vijiji ndio zinapanga ni miradi inakwenda kijiji kipi na ni miradi ipi iende kwenye vijiji vipi katika Wilaya. Kwa hiyo, tulichofanya ni kwamba tuliomba Vijiji au tuliomba miradi ambayo inahitaji kufanyiwa kazi kidogo tu na Wananchi wanaanza kupata huduma hizo za maji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika Wilaya ya Makete wakachagua Vijiji hivyo vinne vya kuanzia. Nina hakika kwamba tutakapoendelea na program hii kwanza watakuwa wamepata uzoefu wa kuendesha hii miradi au ujenzi wa miradi hii na pili watakuwa wameoanisha maeneo mengi kati ya hivi Vijiji 98 alivyosema.

Kwa hiyo, ni jukumu la Wilaya ya Makete kuleta miradi hiyo na kuchagua ni Vijiji vipi pale ambapo tutakuwa tumekamilisha hivi Vijiji vitakavyoanza na mradi huu. Ili kujenga uzoefu na kupima uwezekano mwingine ni maeneo yapi ambayo tunaweza kufanya marekebisho ili huduma ya maji Vijijini iweze kuendelezwa na kupatikana kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Na 43.

**Upatikanaji wa Nishati Mbadala.**

**MHE. LEKULE M. LAIZER (K.n.y. MATHEW T. OLE-TIMAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa, asilimia kubwa sana ya Watanzania mijini na vijijini hutumia kuni au mkaa kupata nishati jambo ambalo linahatarisha mazingira ya nchi kwa ujumla.

Je, ni lini Serikali itatafuta na kuanzisha utaratibu wa upatikanaji wa nishati mbadala ili kuyanusuru mazingira yetu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Ole Timan Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro kwamba matumizi ya kuni na mkaa nchini bado ni makubwa sana na yanaathiri mazingira yetu na afya za watumiaji. Karibu asilimia 90 ya nishati yote itumikayo hutokana na misitu ambayo inakatwa kwa kasi inayokadiriwa kuwa hekta zaidi 90,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ili kuyanusuru mazingira (hasa misitu), Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikibuni na kutekeleza miradi ifuatayo:-

(a) Utumiaji majiko Sanifu ya mkaa na kuni, mradi huu unaosimamiwa na shirika la *TATEDO* pamoja na *NGO* zingine.

(b) Utumiaji matanuru fanisi ya kuzalisha mkaa. Mradi huu umefadhiliwa na Serikali ya Uholanzi kwa nchi za *SADC.*

(c) Utumiaji tungamotaka zingine *(biowaste)* badala ya kuni au mkaa, kwa mfano: Uzalishaji wa vitofali vitokanavyo na pumba za mbao *(saw dust briquettes)* unafanywa na *Kilimanjaro* I*ndustrial Development Trust (KIDT)* huko Moshi.

(d) Utafiti wa teknolojia muafaka ya makaa wa mawe kwa ajili ya kupikia na viwanda vilivyoko vijijini.

(e) Utumiaji wa umeme nuru chini ya mradi unaofadhiriwa na *UNDP/GEF/SIDA* kule Mwanza na sehemu zingeni nchini.

(f) Serikali ya Denmark *(SIDA)* inaisaidia Serikali yetu kuendeleza mradi wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu za upepo.

(g) Utumiaji wa vyanzo vingine vya nishati kama vile bayogesi, maporomoko madogo ya maji, na kadhalika ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya nishati itokanayona mazao ya misitu.

(h) Mswada wa kuanzisha wakala na mfuko wa nishati vijijini utajadiliwa leo hapa Bungeni. Mswada huu ukiwa sheria utaiwezesha Serikali na sekta binafsi kusambaza umeme vijijini kwa kasi kubwa na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa nchini.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Ngorongoro ni Wilaya mojawapo kati ya Wilaya ambazo hazijawahi kupata umeme na hasa Makao Mkuu ya Wilaya pamoja na maeneo mengi katika Wilaya hiyo. Kwa kuwa Serikali iliwahi kutoa ahadi ya Vijiji vingi kupatiwa umeme kama Namanga, Longido inayopakana na Wilaya hiyo.

**SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Je, Serikali itafikisha lini umeme katika maeneo hayo ya Ngorongoro?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lekule Laizer, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya kufikisha umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro na Wilaya nyingine ambazo hazijapata umeme, bado iko pale pale na tutafikisha umeme huo mara tutakapopata fedha za kutosha kufanya kazi hiyo. Lakini vijiji mbalimbali kama ninavyosema Muswada ambao tutaujadili asubuhi hii, kwa kweli nadhani ndio mkombozi mkuu wa kusambaza umeme vijijini kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge muupitishe haraka haraka ili tuweze kuanza kazi hiyo mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Na. 44

**Umeme Usio na Uhakika Tandahimba**

**MHE. ABDULA S. LUTAVI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa sehemu kubwa ya Mkoa wa Mtwara hasa Wilaya ya Tandahimba imeendelea kutegemea umeme usio hakika kutoka kwenye mitambo iliyopo Masasi na kwa kuwa tumekuwa tukipewa matumaini ya kurekebishwa kwa hali hiyo kufuatia kugundulika kwa gesi ya *Mnazi Bay.*

Je, ni hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa mradi huo na ni nini mategemeo ya Wilaya ya Tandahimba kunufaika na mradi huo wa *Mnazi Bay?*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mikoa ya Kusini hasa Mtwara na Lindi kwa muda mrefu imekuwa ikitegemea umeme wa mitambo inayoendeshwa na dizeli. Kutokana na kukua kwa matumizi na kuchakaa kwa mitambo, mara nyingi umeme umekuwa hautoshi. Ili kukabiliana na tatizo hilo, *TANESCO* ilifunga jenereta mpya yenye uwezo wa megawati mbili mjini Mtwara kama hatua za muda mfupi.

Hatua za muda mrefu ni kutumia gesi ya *Mnazi Bay* kuzalisha umeme kwa ajili ya Mikoa ya Mtwara na Lindi. Tayari kampuni ya *Artumas Group* ya Canada sasa hivi inafanya kazi kule *Mnazi Bay.* Katika awamu ya pili ambayo itaanza baada ya kupata uhakika wa gesi, itahusu uzalishaji wa umeme.

Ili kukamilisha shughuli hizo, Serikali imeunda timu ya wataalamu wanaofuatilia kwa karibu utendaji na mwekezaji. Kama shughuli zote zitaenda kama ilivyotarajiwa basi umeme wa uhakika utapatikana Mikoa ya Kusini ikiwa ni pamoja na Tandahimba ifikapo mwaka 2006. *(Makofi)*

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri lakini nilikuwa nataka niwekwe sawa tu na Serikali kwenye jambo hilo.

Nilipata kusoma kwenye vyombo vya habari kwamba hiyo kampuni inayotajwa kwamba inashughulika na mradi wa *Mnazi Bay* umefanya tathmini yake na kwa kuanzia inalenga kufanya shughuli hii kwenye maeneo ya Mtwara kupitia Mnazi Mmoja, kupitia Masasi na maeneo mengine na sababu waliyoitoa kwenye maelezo haya ni Ubora wa Miundombinu.

Sasa nilitaka niiulize Serikali kwamba siku moja niliwahi kuuliza swali kuhusiana na ujenzi wa barabara ya Mtwara Kolivu kama inapita Masasi, Newala na Tandahimba nikaambiwa inapita kwenye barabara ya lami sasa kwenye hali hii kama inavyojionyesha mradi Serikali haioni kwamba kukosekana kwa miundombinu kwenye eneo lile tunalolizungumzia ni kichocheo cha eneo lile kuendelea kudorora kiuchumi kama inavyojionyesha sasa hivi? Tuna viwanda vya korosho katika eneo la Newala, viwanda vile vinategemea umeme na umeme kama ninavyoujua kwa kweli ni wa kukatika kila baada ya nusu saa. Sasa kama mtazamo wa hao wawekezaji tunaowazungumza ni huu wa kwamba waanzie huku kwanza na viwanda vile wameshapewa watu ili waanze kuvifanyia kazi, viwanda hivi vitafanyaje kazi kama umeme haupo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lutavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* na wawekezaji wote wanaozalisha umeme wanazalisha umeme kwa biashara, yaani ni huduma au ni bidhaa au ni *commodity* ambayo inatakiwa iuzwe wapate fedha na kuendelea na shughuli hiyo katika sehemu nyingine, wapate faida. Wale wawekezaji kwa hiyo lengo lao mara kwa mara ni kupeleka umeme kule ambako kuna *demand* yaani kuna mahitaji ya nishati hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi kwamba kwa sababu utapitia sehemu fulani utakwepa maeneo ambayo kwa kweli ndiko unakohitajika kwa sababu nia yao nikuwafikia wateja, wauze umeme huo wapate fedha na kama ni *TANESCO* waendeleze shughuli hiyo sehemu nyingine na kama ni mwekezaji apate faida ya kulipa madeni yake.

Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kampuni hii itafikisha umeme kila mahali ambapo kuna *demand* au mahitaji ya nishati hiyo na tutaanzia na kuhakikisha kwamba viwanda vinapata nishati hiyo ili ili viweze kufanya kazi na kusaidia Taifa hili katika kujenga uchumi wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha kwa hiyo swali la Mheshimiwa Iwvatta litapangiwa nafasi nyingine. Baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo la Kikao cha Kamati mojawapo ni Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Mwenyekiti wake, Professor Mgombelo, anawajulisha Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa leo tarehe 14 Aprili, 2005 saa 7.00 mchana watakuwa na Kikao katika Ukumbi Namba 231 ghorofa ya pili, jengo la utawala. Wajumbe wanaombwa kuhudhuria. Kamati ya Miundombinu.

Baada ya hapo nitoe maelezo yafuatayo kwamba kulingana na kasi yetu ya kupitisha Miswada inavyokwenda ni kasi nzuri kwa hiyo sasa ukiondoa Muswada uliopo kwenye *Order Paper* ya leo tutakuwa tumebaki na Miswada miwili tu ya *Warehouse Receipts* na ile ya *Cooperative Audit.* Tumeshauriana na Serikali kwamba huu Muswada wa *Warehouse* na kwa kweli lilikuwa ombi la Kamati iliyouchambua Muswada huu kwamba utatendewa haki vizuri zaidi Bungeni endapo utatanguliwa na semina ili Waheshimiwa Wabunge wapate uelewa mzuri zaidi juu ya mambo haya ya *Warehouse Receipts.*

Kwa hiyo, nimepanga kwamba kwa kuwa kasi yetu ni nzuri semina hiyo inayotakiwa ili kusudi Muswada huu uweze kuingia kwenye *Order Paper* za wiki ijayo na kwa kuwa Jumamosi inayokuja ilikwisha kupangiwa semina nyingine, kwa hiyo nimepanga kwamba semina hiyo inayohusu Muswada huu ifanyike kesho Ijumaa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutakuwa na semina mbili, kesho Ijumaa na Jumamosi. Kwa ajili hiyo, Muswada huu uliopo kwenye *Order Paper* umepata wachangiaji wengi wa kutosha, waachangiaji 25 mpaka sasa. Kwa hiyo, utajadiliwa kwa siku mbili yaani leo na siku ya Jumatatu ijayo, ili kusudi mwisho wa mjadala wa leo Bunge litaahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 12 Aprili, 2005 ili kusudi kesho tuingie kwenye Semina.

Baada ya maelezo hayo sasa tunaendelea na *Order Paper.* Katibu endelea.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI.

### Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini wa Mwaka 2005 *(The Rural Energy Bill, 2005)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtoa Hoja ungesubiri kwanza Waheshimiwa wanaokwenda kunywa chao waondoke ndipo nitakuita.

Sasa timaweza kuanza, namuita Mheshimiwa Mtoa Hoja Waziri wa Nishati na Madini.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Muongozo wa Spika.

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nahitaji mwongozo kidogo katika *Order Paper* Muswada ulioandikwa umeandikwa Muswada wa Sheria ya kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini. Samahani maana yake hasa ni Muswada wa Sheria ya Nishati Vijijini *Rural Energy Bill* na ndiyo inayounda Wakala wa Mfuko na *Board.* Nataka tu ufafanuzi kama nilivyoelewa ni hivyo.

**SPIKA:** Tufuate maneno ya Kiingereza ya Muswada wenyewe kwa sababu umeandikwa kwa Kiingereza. Hii ni tafsiri, nadhani ya Katibu. Kwa hiyo isitusumbue sana, sisi tushughulikie Muswada kama ulivyoandikwa kwa Kiingereza. Mheshimiwa Mtoa Hoja endelea.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha Muswada wa Nishati Vijijini hapa Bungeni asubuhi hii ninaomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Rahaleo, kwa kufiwa na Mbunge wao, Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, mwezi uliopita.

Aidha naipa pole familia ya Mzee Paul Bomani, aliyefariki mwanzoni mwa mwezi huu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi.

Baada ya hayo ningependa kuishukuru Kamati ya uwekezaji na biashara chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo, pamoja na Wadau wote ambao wamejadili Muswada huu wa kuanzishwa kwa Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini. Ushauri wao tumeuzingatia na umesaidia kuboresha Muswada uliopo mbele yetu. Ningependa pia kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuandaa Muswada huu, kwa ajili ya kuwasilishwa hapa Bungeni leo.

Maudhui ya Muswada huu ni sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003, sera hii inasisitiza kuongeza juhudi ya kuendeleza upatikanaji wa nishati vijijini ili kuboresha uzalishaji mali na kupunguza umaskini. Sera hii inaainisha kuwa ili kuharakisha upatikanaji wa huduma ya nishati ya kisasa vijijini ipo haja ya mfumo wa kitaasisi wa kuhamasisha, kuratibu na kuharakisha jitihada za Sekta binafsi na za umma za kuwekeza katika kuzalisha na kusambaza nishati bora vijijini. Kwa hiyo basi, madhumuni ya Muswada huu ni kuanzishwa kwa wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini, ili kutimiza azma hiyo katika maeneo ya vijijini Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Muswada una sehemu sita zenye jumla ya vipengele 28 vilivyopangwa kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ya Muswada inatoa utangulizi, ufafanuzi wa vipengele, vifupisho na matumizi ya sheria, tafsiri ya maneno pamoja na dhana ya sheria hiyo.

Sehemu ya II ya Muswada inaweka misingi ya maendeleo ya Nishati Vijijini. Misingi hiyo inatajwa katika kipengele cha nne kuwa ni pamoja na kutoa fursa ya uwezeshaji katika usambazaji wa nishati ya kisasa katika maeneo ya vijijini ili kuhamasisha ukaji wa uchumi, uzalishaji mali na uboreshaji wa huduma za jamii.

Kipengele kinaendelea kueleza kwamba maendeleo endelevu yatafikiwa ikiwa huduma za nishati ya kisasa zitahamasishwa kwa kuhusisha juhudi za Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. Wajibu wa Serikali katika upatikanaji wa huduma za nishati vijijini ni kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha Sekta Binafsi na Vikundi vya Kijamii kuweza kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha tano katika sehemu hii pia kinaainisha majukumu ya Waziri anayeshughulikia masuala ya Nishati kuwa ni kuangalia na kusimamia utekelezaji wa sera ya Nishati. Vilevile kwa kushauriana na Waziri wa Fedha kuweka mipango ya kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya nishati nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya III ya Muswada inaelezea kuundwa kwa Board ya Wakala, kipengele cha sita kianelezea kuwa Board itakuwa na majukumu ya kuidhinisha miradi na kuifadhili ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za nishati za kisasa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kiuchumi, afya na elimu, upatikanaji majisafi na shughuli za usalama.

Aidha, *Board* itatoa msaada wa kiufindi kwa wawekezaji wenye sifa watakaochangia upatikana wa huduma za nishati za kisasa vijijini na kutoa ruzuku katika hali ya uwazi na ushindani.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha saba kinatoa mfumo wa muundo wa *Board* ya Nishati Vijijini, Wajumbe wa *Board* watatokana na wadau wakuu ikiwa ni pamoja na Wizara zinazohusiika na Nishati, Fedha na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sekta Binafsi itawakilishwa kwenye *Board* na vile vile Jumuiya ya Wafadhili itawakilishwa na Mjumbe ambaye hatapiga kura kweny Kikao cha *Board.*

Masuala mengine katika sehemu hii yanahusiana na uundaji wa *Board,* vipengele vya nane hadi kumi na tatu vinaelezea Sifa na Taratibu za Kuwateua Wajumbe wa *Board,* Kipindi cha Kutumikia *Board,* Mikutano na Taratibu za Board, Mamlaka na Kazi za *Board,* Uwezo na Uwajibikaji wa *Board.*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya IV ya Muswada inaelezea Muundo wa Wakala wa Nishati Vijijini ambao madhumuni yake itakuwa ni kutekeleza Mipango na Maamuzi ya *Board* pamoja na kuwezesha utoaji wa Misaada ya Kiufundi, Mafunzo na aina nyingine za kujenga uwezo kwa Wawekezaji wenye sifa watakaofikia vigezo vitakavyowekwa na *Board* katika maeneo ya Mipango na Maandalizi ya miradi ya maombi ya wafadhili. Kazi za Wakala zimeainishwa kwenye kipengele cha 16.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya V ya Muswada inaelezea kuanzishwa kwa Mfuko wa Nishati Vijijini, Mfuko utatumika kama chombo cha kugharimia miradi ambacho Boardi itakitumia kutimiza wajibu wake wa kutoa misaada na ruzuku ili kupunguza miradi inayoendelezwa na makampuni Binafsi na yale ya Umma, Vyama vya Ushirikia na Vikundi vya Kijamii. Vyanzo vya fedha vitatokana na mchango wa Serikali kutokana na mgawo katika *budget* ya Serikali, michango kutoka kwenye mashirika ya fedha ya kimataifa yaani *Multilateral and Bilateral Agencies* na wafadhili wengine, kodi au tuzo hadi kiasi cha asilimia tano kwenye uzalishaji na usambazaji wa umeme kwenye *grid* ya

Taifa na ada inayohusiana na *program,* majarida, semina, huduma na ushauri wa kitaalam na huduma nyingine zitakazotolewa na Wakala.

Mheshimiwa Spika, mwisho sehemu ya VI ya kipengele cha 25 kinatoa muongozo juu ya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, Maafisa wengine na wafanyakazi, aidha kipengele hicho kinasisitiza kuwa uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu utakuwa wa ushindani na kwamba kufuatana na mwongozo wa *Board* atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala pamoja na Mfuko wake. Kipengele cha 26 kinaeleza kazi za Mkurugenzi Mkuu na kinatoa kinga ya wafanyakazi wa Wakala wakati wakifanya kazi kwa niaba ya Wakala au *Board.*

Muswada pia una viambatanisho yaani *schedules* viwili vinavyotoa mwongozo wa *management* ya mfuko na maelekezo ya vikao na mikutano ya *Board.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALI ASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI (K.n.y. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, maoni ya mapendekezo ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Muswada wa Sheria ya Nishati Vijijini wa mwaka 2005 yaani *The Rural Energy Act 2005.*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya Bunge namba 70(2) toleo la mwaka 2004 naomba kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Muswada wa Sheria ya Nishati Vijijini ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Wabunge wenzangu kwa kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kutoa salaam za rambirambi kwa familia na jamaa ya Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyefariki mwezi Machi mwaka huu. Marehemu tumeshirikiana naye kwa nyanja mbalimbali akiwa Mbunge mwenzetu, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Muswada. Kabla ya kuanza kuchambua na kujadili Muswada huu Kamati iliwaalika Wadau mbalimbali ili nao watoe maoni yao. Michango ya wadau hawa imesaidia sana katika kuboresha Muswada huu. Nachukua nafasi hii kuwatambua Wadau hao:-

*COSTHEC, TIRDO, DAR ES SALAAM INSTITUTE OF TECHNOLOGY, TANZANIA GEN AND NETWORKING PROGRAM, TAX INVESTMENT* na *GESCO LIMITED.*

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Muswada huu, Kamati ilizingaitia yafuatayo:-

Kwanza, ili sheria hii ieleweke na wananchi wa vijijini ni vema kutumia umeme badala ya neno lingine lolote vinginevyo wananchi hawataelewa.

Pili, Muundo wa *Board,* Kamati pamoja na Wadau waliona ni muhimu kwa *Board* ya Nishati Vijijini kuwa na Wajumbe wenye taaluma au wanaotokana na Taasisi zenye taaluma inayohusika.

Tatu, suala la jinsia wakati wa kuteua *Board* lisisitizwe na lizingatiwe. *(Makofi)*

Nne, gharama za umeme ziangaliwe ili wananchi wetu waweze kuzimudu.

Tano, kodi kwa vifaa vya umeme iangaliwe.

Sita, nimeangalia juu ya uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa *Board.*

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati. Muswada huu umekuja wakati muafaka hasa ukizingatia hoja ya Wabunge wengi humu Bungeni juu ya mahitaji ya umeme sehemu wanakotoka hususani Vijijini.

Katika kuchambua Muswada Kamati imezingatia kuwa umeme ni kichocheo kikubwa katika kuleta mapinduzi ya maendeleo vijijini kama vile kusukuma maji, kusaga nafaka, viwanda vidogovidogo na kadhalika. Hivyo kuongeza kipato kwa wananchi wengi. Pamoja na Serikali kujua umuhimu huo wa umeme imeshindwa kusambaza kwa kasi kama ilivyotarajiwa kutokana na gharama kubwa ya vifaa vya kusambazia umeme huo kama mitambo, nguzo, nyaya na kadhalika.

Kuanzishwa kwa Wakala huu na Mfuko wa Nishati Vijijini ni njia sahihi na endelevu ya kumaliza ama kupunguza matatizo ya umeme vijijini. Muswada vile vile unatoa nafasi kwa wazalishaji umeme wadogowadogo kuweza kufanya biashara hiyo kwa jamii iliyowazunguka kwa gharama nafuu. Kamati inaamini kuwa kushirikishwa kwa sekta binafsi kwenye Muswada huu kutawezesha usambazaji wa umeme kwa haraka zaidi kwa ngazi za vijiji wakati serikali itaendelea na jukumu la kuweka miundombinu ya kuzalisha umeme kwa ngazi ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili Muswada huu Kamati inayo mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 4 na ufafanuzi kutolewa kwenye nyongeza ya kwanza, maliasili ya mafuta, gesi asilia, petroli na kadhalika, ambavyo ni malighafi katika kuzalisha umeme ni masuala ya Muungano kwa maana hii kuna umuhimu wa kuhusisha Tanzania - Zanzibar pia.

Kamati imeelezwa kua wawekezaji chini ya sheria hii watapewa ruzuku kwa lengo la kuwezesha kupanga bei nafuu kwa umeme watakao uzalisha. Kwa hiyo, Kamati inapendekeza kuwa Serikali pia iangalie bei za vifaa vya uzalishaji umeme ili viwe nafuu kuvinunua. Ili kutimiza azma hii Kamati inapendekeza kodi za vifaa vya kuzalisha umeme ulioelekeza vijijini ziangaliwe upya kwa lengo la kuzipunguza.

Pendekezo la tatu, kifungu cha 7(1) kuhusu Wajumbe wa *Board* ya Wakala wa Nishati Vijijini pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Kamati inapendekeza kuwa uteuzi kwenye *Board* hiyo uzingatie zaidi taalum, uzoefu na jinsia badala ya Taasisi mbalimbali ambazo hazina mtandao hata vijijini. Aidha, inapendekezwa kuwa uwakilishi wa wananchi vijijini wawe miongoni mwa Wajumbe wa *Board* hiyo. Umakini wa kuwateua Wajumbe hao uzingatie uzoefu uliopatikana katika uteuzi wa *Board* za wakala wa Barabara *TANROADS* ambayo inafanya kazi yake kwa ufanisi mkubwa. Kuhusu uteuzi wa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kwamba Mwenyekiti wa Board ateuliwe na Waziri badala ya Wajumbe wa *Board* kumchagua.

Tano, kwenye kifungu cha 25(2) kinachohusu namna ya kumpata Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini, Kamati inapendekeza kuwa apatikane kwa njia ya ushindani ili kutoa nafasi kwa Watanzania wanye sifa waweze kuomba nafasi hii hivyo neno *internationally* liondolewe.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati, namshukuru Mheshimiwa Daniel Yona - Mbunge, Waziri wa Nishati na Madini, Wakuu wa Idara, pamoja na Watendaji Wakuu wa Mashirika mbalimbali chini ya Wizara hiyo, kwa ushirikiano wao.

Shukrani nyingi ziende kwa Wadau wote waliosaidia kuboresha Muswada huu kama nilivyowataja hapo nyuma. Hawa wote walitoa michango yao ambayo iliipa Kamati msingi wa kufikia maoni niliyowasilisha hapa.

Namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi zake vizuri na Ndugu Aggrey Nzowa Katibu Kamati, kwa kuihudumia Kamati kuanzia mwanzo hadi mwisho wa vikao vya Kamati.

Mwisho napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yangu kwa michango yao iliyokuwa makini na kutuwezesha kutoa taarifa hii leo. Wajumbe hao kwa mujibu wa kanuni ya 95(1) toleo la mwaka 2004 ni wafuatao:-

Mheshimiwa William H. Shellukindo - Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Salome J. Mbatia - Mbunge na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe

wengine ni kama wafuatao: Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchuno, Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mheshimiwa Dr. Aaron D Chiduo, Mheshimiwa Omar S. Chubi, Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta, na Mheshimiwa Stephen M. Kazi.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Aisha P. Magina, Mheshimiwa Khasim Hamis Aboud, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Ali S. Musa, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulazizi, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Christopher S. Wegga, Mheshimiwa Sumri A. S Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga na mwisho ni mimi mwenyewe, Mheshimiwa Nazir Karamagi, .

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Sekta hii Mheshimiwa Isaac M. Cheyo, ili atoe maoni ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. ISAAC M. CHEYO - NAIBU KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe shukrani kwa kunipatia fursa hii ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kutoa pole kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bariadi Magharibi kwa familia za Marehemu Balozi Paul Bomani na Marehemu Balozi Hassan Diria, kwa kuondokewa na wakuu wa familia hizo. Naomba Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, mbele yetu kuna Muswada unaoitwa *The Rural Energy Bill, 2005,* madhumuni na malengo yake yameainishwa. Mimi sina haja ya kuyabadilisha isipokuwa tu kutoa taarifa kuwa huko nyuma Serikali ilitoa sera ya kueneza nishati umeme katika maeneo ya uzalishaji na usindikaji wa mazao kama vile *Gineries* na viwanda vya kusindika chai, matunda na kadhalika, ambavyo vilikuwa vyote viko vijijini. *(Makofi)*

Lengo la sera hiyo ilikuwa ni kuwezesha viwanda hivyo kuja na wanavijiji kupata nguvu umeme kwa uzalishaji na wanavijiji kupata nishati hiyo kwa urahisi japo sio kwa bei ndogo. Viwanda vingi na Vijiji vilivyokuwa karibu na viwanda hivyo vilipata nishati umeme na hivyo kuharakisha nishati viwandani na Vijiji kuibua shughuli zingine za kiuchumi kwa lengo la kupunguza umaskini. Sina uhakika sera hiyo ilifanikiwa kwa kiasi gani kuwafikia wananchi na viwanda vyote vilivyoko Vijijini.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kuweka utaratibu wa kisheria wa kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini ili kuratibu juhudi za kuweka nishati endelevu na za kisasa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina sura ya Muungano suala la nishati iwe ya nyuklia, mafuta, maji, makaa ya mawe au gesi, Tanzania Visiwani nao wana sehemu yao ya kufikiriwa au kuhusika moja kwa moja na suala la uendelezaji wa nishati hii.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba mwaka jana wakati wa Bunge, Waziri wa Nishati na Madini alipokuwa anazungumzia utafiti na uchimbaji nishati mafuta kwenye maeneo ya Zanzibar, Serikali ilisema suala la uchimbaji na utafiti wa nishati mafuta ni suala la Muungano kama ambavyo imeainishwa katika *schedule* ya kwanza ya *Union matters item number fifteen.* Leo Kambi ya Upinzani inashangaa na Kamati pia nashukuru kwamba na wenyewe wameliona hilo, inashangaa kuona tunaunda Mfuko wa kuendeleza nishati kwa Tanzania Bara tu. Hii tunaona ni kutowatendea haki wenzetu wa Visiwani. Ikumbukwe kwamba kule Pemba hawana umeme wa *grid* na kwenyewe kuna Vijiji na wao pia wanastahili kupata huduma kama hii ambayo inataka kuwepo Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungependekeza Mfuko huu uwe kwa kuendeleza nishati Vijijini, Tanzania Bara na Visiwani yaani uwe ni Mfuko kwa kutoa huduma kwa Tanzania nzima bila kutenga Tanzania Bara na Visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada huu inaelezea misingi ya uendelezaji wa nishati umeme Vijijini, ibara ya nne inasema kama ifuatavyo: "Kuwe na mpango endelevu wa kuwezesha kuharakisha upatikanaji wa nishati ya kisasa Vijijini ili kujenga uchumi na kuleta ustawi wa jamii". Pia katika ibara hii kuna msisitizo kuwa mpango huu endelevu usaidie kuibuliwa kwa upatikanaji wa huduma ya kisasa kabisa ya nishati Vijijini kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi, sekta ya umma, kubuni na kuendeleza nishati ya aina yoyote huko Vijijini kwa lengo la kuwafanya wananchi waishio Vijijini wapate nishati kwa urahisi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, sisi hatuna pingamizi na hilo kwani malengo hayo yanaondoa ukiritimba wa shirika moja la umma kuhodhi na kuendesha shughuli zote za kuendeleza nishati umeme Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba unaporuhusu watu wengi kuingia katika soko kama hili wengi watashindana kujenga miundombinu ya nishati kwa lengo la kuwafikia wateja wao ambao ni wananchi waishio Vijijini ambao wapo takriban asilimia themanini ya Watanzania wote. Ushindani wa namna hiyo utaleta ufanisi na hatimaye kutoa huduma iliyo bora na rahisi kwa walaji (*consumers)* na hivyo watumiaji wa nishati umeme huko Vijijini nao wataibua miradi ya kiuchumi na hivyo kupunguza janga la umaskini.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa kwa kupitia Muswada huu mtu yeyote atakayetaka kuendeleza mradi wa nishati Vijijini hatahitajika kuomba kibali cha *TANESCO,* shirika ambalo kwa kweli limeingiliwa na mtu mmoja anayeitwa *Net Group Solution* na kuwa *confusion.* Sasa shirika hili limekuwa na matatizo mengi kuliko hata lilipokuwa chini ya Wamatumbi wenzetu. Kwa kuwa na *Net Group Solution* umeme bado unakatika, kukatika katika kwa mara kwa mara bado kupo pale pale na hata bei ya

umeme bado ipo juu na hata ujenzi wa miundombinu kufikia kwenye Vijiji na Makao Makuu ya Wilaya nyingi bado haujaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, tumeeleza hapo mwanzo kuwa sekta binafsi ikipewa nafasi bila ya kuingiliwa au kuminywa na sekta ya umma inaweza kufanya maajabu katika kuendeleza nishati Vijijini. Sekta binafsi ikiruhusiwa kupata ruzuku au kutafuta wabia tunaamini maendeleo endelevu ya nishati Vijijini yatapatikana.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano ya Muswada huu inatutia wasiwasi pamoja na kuamini kwamba zimeruhusiwa sekta binafsi kushirikiana. Inatutia wasiwasi kwamba sekta binafsi haitafanya shughuli bila kuingia ubia na sekta ya umma kwan *funding mechanism* iliyotajwa katika sehemu ya tano ya Muswada huu inasema: "Mfuko umeanzishwa ili kufanya maamuzi ya namna Bodi ya Wakala kupitia Mfuko huu utakaoshughulikia utoaji wa ruzuku na punguzo la gharama za kuwekeza katika miradi ya nishati endelevu ambayo imetayarishwa na sekta binafsi na sekta ya umma, vyama vya Ushirika na jamii".

Mheshimiwa Spika, suala hili linalazimisha sekta binafsi ishirikiane na sekta ya umma kama *TANESCO* ama shirika lingine kuibua miradi endelevu ya nishati Vijijini kwa kupita funding mechanism. Kama sekta binafsi haitashirikiana na sekta ya umma basi haiwezi kupata ruzuku. Nayasema haya kwa sababu ya neno moja tu la Kiingereza ambalo lipo katika wording, linasema: *"The fund represents the funding mechanism by which the Board shall fulfill its mandate to provide grant to subsidize capital costs of the project that are developed by private and public entities".* Sisi tulikuwa tunafikiri kwamba hapa neno *and is compel,* linawalazimisha kwamba hamwezi kuingia ubia wa aina yoyote ile lazima ushirikiane na sekta ya umma. Tulikuwa tunafikiria kwamba ingekuwa imerahisisha na kutoa nafasi kwa mtu yeyote yule ambaye ana uwezo wa kuwa na pesa ama akapewa ruzuku akatengeneza miundombinu ya nishati Vijijini kwa kulitoa lile neno na kusomeka kwamba: *"Are developed by private or public sector".* Neno *'or'* lingetoa ule ulazima wa *private sector* kulazimika kushirikiana na *public sector* ili ipate ruzuku.

Mheshimiwa Spika, hapa tunaingia kwenye mkenge ule ule wa *IPTL* na *TANESCO* ambapo Taifa hadi sasa linaumia kwa kulipa zaidi ya 3.5bn kila mwezi bila sababu yoyote ile. Kama Serikali inahofu kwamba sekta binafsi itaimeza sekta ya umma, basi Serikali ikubali sekta binafsi iendeleze miundombinu ya nishati na hatimaye kuiuza kwa sekta ya umma badala ya kulazimisha kupitia Mfuko huu kuwa sekta binafsi lazima ishirikiane na sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema pale mwanzo sina sababu yoyote ya kupinga Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa siku ya leo ili nami niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu wa kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Umeme Vijijini. Kabla sijafanya hivyo naomba kutoa rambirambi zangu kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Balozi Diria. Mwenyezi Mungu aiweke

roho yake mahali pema. Nilifika wakati mliponipa nafasi kwenda Nairobi, kwenda kumwona pale hospitali ya Aghakhan na familia yake tuliiona, tuliwawakilisha Wabunge wenzetu na tukamwona. Kwa kweli walimsaidia sana kule, lakini Mungu amemchukua Marehemu kwa wakati ambao ameupanga.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nichangie Muswada huu. Muswada uliopo mbele yetu unasema Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini. Neno nishati tumeona tumezamia chini sana ya neno umeme. Nishati katika nchi hizi zipo nyingi hasa baada ya kuangalia vipengele vinavyotoa *definition* ya nishati *is so wide.*

Lakini kabla sijafanya hivyo, wakati ule nilimwuliza Waziri na alijibu vizuri sana kwamba Muswada huu unatekeleza ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2000, Ibara ya 50(i)-(iii) ambapo tumetoa maamuzi ya makusudi pale kwamba uanzishwaji wa suala hili utafanyika na baadaye tukafanya maelekezo kwa wananchi na hasa kutokana na juhudi zilizofanywa na Serikali mpaka kufikia tuna Tanzania *production* ya umeme. Sasa hivi tuna *megawatt* karibu 770 na tathmini niliyofanya ni kwamba usambazaji ile *transmission* imefikia karibu kilomita 4534 za kugawa kwa wateja peke yake, kupitisha ile miti na kusambaza ni kilomita karibu 29,826.

Mheshimiwa Spika, haya yamesemwa kwenye ibara ya 13 ya hotuba ya Waziri wakati akiwasilisha bajeti yake Bungeni. Hii inaonyesha dhahiri kwamba umeme unawaendea wananchi lakini uwezo ulikuwa umetushinda, lakini Serikali inafanya kila jitihada kuonyesha kwamba tunafanikisha suala la umeme kwa sababu huwezi kuwa na teknolojia yoyote bila kuwa na umeme, *computer* na vitu vingine vilivyoingia sasa hivi ni mpaka uwe na umeme.

Kuna mambo mawili tu nataka kuzungumza kwamba kwa mfano, hili suala la Muungano limekuwa *taken care,* sheria ya *Executive Agency* ambayo ilipitishwa ndani ya Bunge lako Tukufu ilikuwa inaanzisha *Central Medical Store* kuwa *Executive Agency,* Ofisi ya Mkemia Mkuu kuwa *Executive Agency.* Kwa hiyo, ingetumika kuanzisha kwa kutumia sheria ile ya *Executive Agency.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri katika Kamati alituambia kwamba huu ni Wakala mkubwa mno. Kwa hiyo, itabidi ianzishwe sheria yake ambayo inajitegemea. Kwa kweli nilikuwa *comfortable* kabisa. Hapo nikaangalia sheria ya umeme inaitwa *Electricity Ordinance, Cap. 131, Supp. 57, Section 84* kama inakuwa imeleta migongano na sheria hii ambayo inanzishwa kwa sababu ile sheria imetoa mandate kwa *TANESCO* kuunda kanuni ndogondogo ambazo zisije kuingilia huu Mfuko wa Umeme ili iwe separate isiwe super imposable, zikaingiliana na kuleta matatizo na migongano. Nashukuru sana wataweka sawa Wanasheria kulielimisha suala hilo. Kwa sababu suala la kuandaa *PSMP* yaani *(Power System Master Plan)* kwamba iliambiwa kwamba Wizara ya Nishati na Madini isimamie *TANESCO,* Shirika la Ugavi wa Umeme kuandaa *PSMP* kwa kudhibiti mambo yafuatayo:-

Kwamba *TANESCO* itaajiri mtaalam mwelekezi wa kutoa maelezo na kuandaa kwa kuzingatia maoni ya wadau na sera ya Taifa kiuchumi, kijamii na kimazingira. Sasa

sidhani kama ile *Master Plan* ilikuwa imeshafanyika tayari, lakini nadhani iko mbioni. Badaye tulikuwa tumeongea kuhusu mambo ya makaa ya mawe kwa mfano, ukiangalia yale ya Mchuchuma, Namwele kule Rukwa ambayo utafiti wake ulifanyika katika mwaka 1925 na baadaye ukafanywa utafiti tena mwaka 1928 na 1929 ambapo ugunduzi uligunduliwa mwaka 1917 wakati huo na *East African Engineering* ambapo kulionekana kuna hekta karibu 6200 hazipo consumed nadhani Muswada huu ukishapita basi watafuatilia utajiri huo ulioko huko katika kufuatilia masuala haya.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, umeme ni kitu ambacho ni muhimu lakini kuna vipaumbele, kuna Sheria kwa mfano ya Songosongo, tulipoanzisha Mradi wa Songosongo ni kwamba umependekeza Vijiji arobaini na vimeorodheshwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, jedwali namba tano, katika ukurasa wa mwisho kabisa, kwamba kuna Vijiji arobaini ambavyo vitapatiwa umeme kwa mradi wa Songosongo. Sasa nafurahi kwa sababu mliwapa moyo watu wa kule angalau bado hamjafanya lakini angalau mtu kama mchafu ukikutwa una sabuni na taulo unakuwa unajiandaa kuoga. Kwa hiyo, huu ni utaratibu mzuri tu ila katika Vijijini vile arobaini nimekuta kuna suala lingine tena, kuna Mji unaitwa Utete, Ikwiriri na Kilwa ambavyo vimeandikwa ni Vijiji. Halafu baadaye kuna mradi mwingine tena ambao umeelezwa kwenye hotuba hiyo hiyo ambao umeelezwa kwamba kuna mradi mwingine nao utakaosaidia mambo hayo. Lakini hapa Mawaziri wanajibu hoja na kukidhi hoja za Wabunge, wakati ule tulipokuwa tunachangia Wabunge wengi tulimudu kutaja maeneo kadhaa ya kutaka umeme, mengine ni Vijijini na mengine ya Mijini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Chiduo katika Jimbo lake la Gairo sasa hivi umeme mpaka Gairo pale kwa kipindi cha muda mfupi tu. Vile vile ni muhimu kuangalia vipaumbele vya wananchi, kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo umeme sio kipaumbele cha kwanza, watu wana vipaumbele vyao. Kwa mfano, katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, vipaumbele vya umeme ni Gwataujembe, Mkono wa Mara, maeneo ya Kidugaro lakini Kitongoji kidogo cha Polambili na maeneo mengine.

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, kwenye Jimbo lake alipendekeza kwamba umeme utolewe kwa urahisi zaidi kutoka Reli ya *TAZARA* kuja Kisaki na maeneo ya Matombo kusudi uje kuunganisha na maeneo ya Mkuyuni na Kiloka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo itakuwa inasaidia sana kwa sababu umeme unapita reli ya *TAZARA* uki-*step down* kama utaratibu ule ambao tulikuwa tunataka kuufanya katika maeneo ya Makambako ambapo Waswedish watatoa 220m/=, Mheshimiwa Waziri alitaja katika hotuba yake kwamba ku-*step down* ule umeme kutoka *kilovolts 220* kwenda mpaka *kilovolts 73* kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Ruvuma. Kwa hiyo na kule nako tunaweza ku-*step down* tukawasaidia wananchi wa Vijiji vya kule Mikese na maeneo ya Kidugaro pale wakapata umeme. Lakini sehemu za Kinole kule kipaumbele cha kwanza ni barabara, Mkulazi ukiwaambia mambo ya umeme hawaelewi, kule kipaumbele ni barabara na maji. Suala hili litafaulu sana kwa kuzingatia haya.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuwa makini katika kusimamia huu Mfuko. Mara nyingi Mifuko hii inapoanzishwa kunakuwa na kutokuwa na uaminifu katika masuala ya

fedha na kutokuwa makini katika utekelezaji. Kwa hiyo, *financial regulation* zinafuatwa ili kusudi Mfuko huu udhibitiwe. Huu ni Mfuko wa wananchi wa Vijijini, hivyo basi wengi watakaoteuliwa ni wale ambao wanakuwa na commitment katika Vijiji, wasiwe kama wamewekwa pale lakini kitu hicho si chao. Kwa mfano, mtu unanua miwani, unaita miwani ya jua wakati kumbe ni miwani yako. Kwa hiyo wakabidhiwe watu ambao ni vyao, wenye mali zao. Au kwa mfano, unanua koti, unaliita koti la mvua wakati ni la kwako. Kwa hiyo, wawe ni wadau hasa wanaohusika na hicho kitu. Washughulikie ili kusudi wasimamie na wawe *committed* na uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, halafu lingine sekta ya umeme imewekwa kwenye sekta ya uchumi. Kwa mfano, hata Ilani ya Uchaguzi katika sura ya pili, imeongelewa katika ukurasa wa 49 na ibara ya 50 kwamba nishati imeelezwa kama ni sekta ya uchumi. Sasa kwa suala la umeme Vijijini liwe uchumi na vile vile huduma za jamii ili kulegeza angalau ikiwa uchumi peke yake kama lile swali la Mheshimiwa Lutavi lilivyojibiwa asubuhi leo kwamba umeme ni biashara, kwa hiyo utaelekea maeneo ambako mwekezaji anapata faida. Sasa nadhani Mfuko huu utakuwa kwa ajili ya huduma na uchumi ili kusudi Watanzania ambao wapo Vijijini kwa sababu hata Mijini ukiangalia kwa kweli hata kwenye majumba ya watu ambao wana uwezo sidhani kama wanatumia umeme kwa kupikia. Mkaa mwingi unasombwa, hata Dar es Salaam kule. Hata kama siku moja Mheshimiwa Spika atauliza nani ambaye hatumii mkaa nyumbani kwake, nitashangaa sana mtu akinyoosha kidole na akinyoosha tutafanya *inspection* nyumbani kwake kama hakuna mkaa. Kwa kweli wengi tunatumia mkaa. Sasa unapeleka Vijijini, nadhani hiyo inaitwa nishati mbadala, hili la ku-*step down* bei nadhani litasaidi ili tusije kupata matatizo. Mara nyingi ukiwa hujui tatizo linajitokeza utapata wasiwasi kama wasiwasi wa yule Msukuma anayeitwa Maganga.

Mheshimiwa Spika, Maganga alipata safari kwenda Marekani, aliambiwa unakwenda Marekani na utakaa miaka miwili. Mtoto wake mdogo akamwambia tafadhali baba naomba twende wote. Akasema tulia nitakuletea baiskeli. Msukuma akiambiwa baiskeli anafurahi kweli. Alipokwenda kule akakaa, baada ya miaka mitatu aliporudi, mtoto akamwambia baba baiskeli yangu, alidhani amesahau. Akamwambia samahani nimeisahau inakuja kwa njia ya meli, alimjibu kwa kumdanganya tu. Yule mtoto akawa anamsonga songa, nataka baiskeli yangu, akasema kwa kweli nimesahau. Akamwambia kama umesahau sikwambii aliyekuwa analala chumbani kwa mama. Basi baba ilibidi ashangae na apite haraka haraka kwenda kuchukua baiskeli. Akaileta baiskeli, akasema mwanangu baiskeli hii hapa, haya niambie. Mtoto akasema, nilikuwa mimi. Kumbe yule mtoto ndiye alikuwa amehamia kule chumbani kwa mama yake. Sasa ilikuwa imempa wasiwasi kidogo, kwa hiyo mtoto akawa ameipata baiskeli kwa vitisho kama hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa utaratibu kama huu ni lazima kwa kweli tuwe wazi katika utekelezaji ili tuweze kufanya vizuri. Umeme ni muhimu kwa ajili ya teknolojia, kama nilivyosema wananchi wanaomba kwa kweli Muswada huu upite ili kusudi tuanze kufanya *process.* Kwa sababu mnatekeleza Ilani ya Uchaguzi, mmejibu hoja za Wabunge wa Tanzania, Vijijini wanausubiri kwa hamu sana. Lakini la msingi ni kwamba kwanza tuzingatie uwezeshaji wa Watanzania kwa ujumla, ujenzi wa nyumba

bora, kwa sababu hata ukiwaambia watu wafanye *wiring* kwenye nyumba zao *unless* unawamulikia umeme kwenye maeneo muhimu ya kufanya mikutano tu kwa usiku. Kwa hiyo, ni muhimu kuhimiza wananchi wajenge nyumba bora, wawezeshwe ili kusudi hali yao ya maisha iende vizuri ndipo hapo wanafanya *wiring.* Lakini kwa utaratibu huu wa nyumba za baadhi ya Vijiji katika Vijiji 10,000 vya Tanzania ukimwambia afanye *wiring* anaona kama unamkebehi. Lingine uwezo wa Watanzania walionao ni mdogo. Kwa hiyo, basi Mfuko huu usiangalie umeme kama ni uchumi bali iwe ni sekta ya huduma za jamii ili kusudi Watanzania waweze kufaidika kwa suala la umeme. Baada ya kusema haya ni kwamba naunga mkono hoja hii na wananchi wa Vijiji vya Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Uponda, Mifuru, Hewe, Bagiro, Nyamigadu, Mkololo, Kumba, Amini, Ludewa, Burugi, Lung'ala mpaka maeneo ya Ngerengere wanausubiri kwa hamu Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Lakini mimi nilikupa nafasi ya kuchangia bila ya kushinikizwa na waliolala chumbani kwa mama. *(Kicheko)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kukushukuru kwa kuniweka mtu wa pili katika kuchangia Muswada huu. Mimi nimesukumwa sana na Muswada huu kwa sababu naamini katika vitu muhimu ambavyo vinapaswa kuanzishwa katika nchi yetu baada ya Mfuko wa Barabara kwa kweli kitu muhimu ambacho kinawagusa wananchi wengi Vijijini ni nishati na nishati kubwa ambayo inazungumza hapa ni umeme kwa sababu uzoefu umeonyesha vyanzo vyote vingine ambavyo vimebuniwa huko nyuma havikufanikiwa sana kuwasaidia wananchi na ndio maana wananchi wengi wanaendelea kutumia kuni au miti kama chanzo kikuu cha nishati. Sasa nishati mbadala ambayo inaeleweka wazi, inaweza kumsaidia mwananchi na ipo ni umeme.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze katika maeneo ambayo nina wasiwasi nayo, lakini nianze kabisa kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii na nakubali kabisa kwamba Mfuko huu uanzishwe. Maeneo ambayo nina wasiwasi nayo kwamba huko baadaye yataleta matatizo ni kwamba, Serikali haijajionyesha waziwazi itashiriki vipi katika kutoa kitu kinachoitwa ruzuku ili kuhakikisha kwamba umeme huu unakuwa rahisi. Haionekani katika sheria, inaonekana tu kwamba Serikali itasaidia watu, vyama, kampuni au mashirika ambayo yataanzisha umeme Vijiji, lakini ni vipi Serikali itadhibiti bei ya umeme au ya nishati zitakazotolewa kuwa rahisi haijaelezwa kikamilifu katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumepitisha Miswada Bungeni hata hii ya Mifuko lakini mwisho wake hata wananchi hawakunufaika, kikubwa wameteseka zaidi. Kwa hiyo, mimi nina woga kwamba ni vizuri Serikali ingekuwa *major partner* katika utekelezaji na hii nitakuja kueleza baadaye katika upande wa kuunda Agency, lakini Muswada huu pia nauona una upungufu maana hauelezi zaidi jinsi *EWURA* itakavyoshirikishwa, haitajwi humu wazi wazi. *EWURA* ni mdhibiti katika eneo la nishati. Sasa sioni humu inavyotajwa jinsi itakavyowadhibiti hao watakaopewa ruzuku

ili bei za umeme zilingane na uwezo wa wananchi. Kwa hiyo, ninaogopa kwamba Serikali kama haitaonekana moja kwa moja itakuwa inajitoa pole pole itawaachia wananchi waumie na hawa wawekezaji. Mimi ni mfanyabiashara, hakuna mwekezaji ambaye amekuja kuuza nishati atakubali akupe kwa bei ya kutupa, hakuna, mpaka afidiwe. Asipofidiwa hata hao walioko Mtwara na hao wengine wa *Song gas* ni kwamba lazima Serikali inafidia na ndio maana *IPTL* imekuwa ghali sana kwa Taifa kwa sababu haikuangaliwa katika msingi wa bei watakazotaja, kiasi gani Serikali itafidia, wao walipewa tu bei ya kuuzia Serikali na bei ambayo kama Serikali haikununua bado mwekezaji alipwe. Sasa na hawa ni vi-*IPTL* vidogo. Tusipokuwa wawazi na waangalifu tutaunda vi-*IPTL* huko Vijijini ambavyo vitakuja kuwanyonya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa *EWURA* lazima ionekane na kila mwekezaji anapokuja apewe kibali cha kuwekeza kwa misingi ambayo itatolewa na *EWURA* kinyume chake tutawaacha wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Spika, nikija kuchangia sasa kifungu kwa kifungu, kuanzishwa kwa Mfuko wenyewe mimi nashukuru vyanzo vya mapato vimetajwa na kwa kweli chanzo ambacho nakiona ni moja kwa moja kitaanza kuchangia na kianze kuorodheshwa katika vyanzo hivyo ikifika Julai ni hili tozo kifungu cha (c) katika ukurasa wa 58, kifungu kinachozungumzia tozo la asilimia kutokana na matumizi ya wanaotumia umeme na kile kinachofuata cha (d). Hivyo ndivyo vyanzo pekee ninavyoviona kwamba ni moja kwa moja vinaweza kuanzisha hii *Fund* ikafanya kazi. Sasa ni vizuri taratibu zianze kutayarishwa. Tusichukue muda mrefu kwa sababu *TANESCO* imekwishajitoa katika utekelezaji wa umeme Vijijini. Sasa hapa kati kuna gap, ni vizuri hii *gap* tuione ili wananchi wasiendelee kusubiri kwa muda mrefu wakimsubiri ni nani atatekeleza.

Mheshimiwa Spika, mimi naona eneo ambalo litapata fedha kwa haraka ni kuletwa sheria au utaratibu ambao kwenye bajeti ya fedha kwa mwezi Juni kuanzia mwaka kesho basi sheria hiyo itajwe na ionekane wazi kwamba vifungu hivi vya asilimia tano vinaonekana ndio Mfuko utaanza. Kinyume chake tukimtegemea huyo mkubwa hapo juu *by the Government in annual budgetary,* hapa ni ndoto maana yake Mifuko mingi imeundwa kama vile wa Elimu na mingine, si rahisi kwa sababu Serikali ina mzigo mkubwa. Sasa hapa nitazungumzia kidogo kwa uzoefu tulioupata kutokana na Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara kabla ya kuanzishwa kulikuwa na chanzo tayari kilikuwa kinapata fedha na ni kodi kutokana na mafuta. Kwa hiyo, tulipoanzisha Mfuko wa Barabara haikuwa shida ilikuwa ni sheria tu na sheria ile hela zile zikaelekezwa huko kwenye Mfuko. Sasa ni vizuri kwa hii *Agency* au hii *Fund* ya umeme Vijijini ikawa na utaratibu na ukatamkwa wazi na hela ziingie ndio tuanze, vinginevyo itachukua muda mrefu na tutawakatisha tamaa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nije katika kuzungumzia eneo lingine kuhusu uendeshaji wa Mfuko wenyewe. Ni kweli mfumo uliochukuliwa ni kama wa *TANROADS* au wa Mfuko wa Barabara na uzoefu ulioonekana ni mzuri sana wa kuendesha Mfuko huu wa Barabara. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba katika huu Mfuko wa *Energy* au wa nishati hauelezwi utaratibu mzima utakaofuatwa.

Kwa mfano, tunataka tujue katika Mfuko wa Barabara kuna Kamati ya Ushauri ya Mkoa, lakini humu sioni. Ni vizuri kabisa kuwe na chombo kwa sababu huu umeme wa Vijijini utakwenda nchi nzima, kwa hiyo kuwe na chombo kitakachoshauri Kimkoa ili tujue bajeti inayotengwa, misaada inayotolewa na isimamiwe na Mkoa. Isiwe hawa watu wanapewa hela na misaada, wanakula bila mtu wa kuwadhibiti. Kwa hiyo, naomba ije sheria na itamkwe kwamba kutakuwa na *Advisory Committee* ya Mkoa ambayo itaangalia uwekezaji katika umeme Vijijini, hiyo haipo. Mimi naogopa sana, tukiachia tu hawa watakuwa hawana mdhibiti katika maeneo ya Mkoa na kwa kweli umeme ni investment kubwa sana ya Serikali. Mimi naomba hilo liwe *noted* na kwa kweli pawe na *some sort of Regional Consultative Board* ambayo itashauri hao wawekezaji.

Lakini pia nizungumzie suala lile *Agency.* Wakati *TANROADS* inaanza *Agency* ile ilikwishatamkwa kwamba itachukua Ma-*Engineer* wa Ujenzi ambao walikuwa Mikoani badala yake walibadilisha tu wakawa *Fund Managers* na Mfuko *immediately fund* ilikuwa na Watendaji. Sasa hii *Agency* yetu najua Waziri ameahidi itakuja sheria. Mimi nashauri hiyo sheria itakapokuja ni vizuri matawi ya *TANESCO* yaliyoko huko Wilayani na Mikoani yawe ndiyo *Agencies* za utekelezaji. Kwa sababu tayari wana bajeti na tayari wanaelewa miundombinu iliyoko Vijijini. Tutakapoanza ku-*creat another organisation* au kujenga Shirika jipya tutaanza kuunda walaji wapya. Hawa wanajua kula na tunatakiwa kuwa-*handle.* Lakini mtakapoanzisha upya bado tutakuwa na *implementer* ambaye anaanza kazi mpaka atakapoanza kuzunguka kwenye kiti aweke utaratibu, ajue maeneo itatuchukua miaka mitano mpaka ashibe kidogo na tuweze kumdhibiti itachukua muda mrefu. Mimi naomba katika kuanzisha ile *Agency* itakapokuja ile sheria mimi naamini kama tulivyofanya kwenye *TANROADS* na Mfuko wa Barabara basi hii *TANESCO* katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ndiyo iwe ni chimbuko la hii *Agency.* Huo ni ushauri.

Mheshimiwa Spika, mwisho mimi nakubaliana kwenye *Part I clause 4(c)* Serikali kuwa facilitator tu. Mimi hii *phrase* sikubali sana. Serikali tusikubali iwe *facilitator* tu. Kwa kweli Serikali awe ndiyo mbia mkuu katika umeme Vijijini. Maana yake ukishamsema *facilitator* atakuambia nimekujengea mazingira mazuri. Sasa ukishamjengea mazingira mazuri hivi ni nani leo kweli atakubali kwenda kuwekeza kwenye umeme Vijijini. Sasa tukubaliane ule ukweli. Hata leo tukisema atakwenda kuanzisha kwenye vyanzo vidogo vidogo vya maji *obvious* gharama yake itakuwa kubwa kuliko ya *TANESCO.* Hata kama amepewa fedha na Serikali utamdhibiti vipi ili bei zake zilingane na gharama zake na wananchi wasinyonywe, hilo ndilo suala la msingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikishakuwa *facilitator* ikajitenga ni kujiondoa kiujanja na *experience as shown.* Serikali unasema siku hizi ni utandawazi sisi hatuhusiki lakini wanaoumia ni wananchi wetu na hawatuelewi. Lazima tujenge *mechanism* ya kuwasaidia. Sasa *EWURA* ipo lakini haya Mashirika ya Udhibiti mimi nasema bado ni machanga uwezo wa kuweka kwanza hilo Shirika kama *EWURA* halijazaliwa. Sasa tatizo kubwa sana ni vizuri kwa hii *Energy Fund* itakapoanzishwa hiyo *Agency* ipewe uwezo mkubwa Serikali isijitoe, Serikali isiwe *facilitator* tu. Uzoefu umeonyesha Serikali inaanzisha vitu hivi inakwenda kupumzika. Kwenye Tumbaku leo wameunda *cartel,*

serikali imeunda Bodi. Bodi zenyewe zimechanganyikiwa, sasa hili ni suala muhimu sana. Tujifunze kwa makosa ya huko nyuma na tusiyarudie.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo mimi naunga mkono hoja na kwa kweli nashukuru sana na tuanze mapema. Hii *gap* iliyopo sasa hivi tuizibe haraka maana yake *TANESCO* hawahusiki na utekelezaji wa Vijijini. Sasa ni vizuri hii *Rural Fund* pamoja na *Agency* izaliwe haraka hii *gap* isiendelee kuwachosha wananchi na kuwakatisha tamaa. Nashukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kunipatia nafasi na mimi nichangie katika huu Muswada.

Awali ya yote naomba niungane na wazungumzaji walionitangulia kwanza kwa kutoa pole kwa familia ya Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria, kwa msiba wa Mheshimiwa Mbunge na vile vile naomba nitoe pole kwa familia ya Balozi Paul Bomani, kwa kifo cha Mheshimiwa Bomani. Viongozi ambao wamekuwa nasi kwa muda mrefu. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara tulichangia katika kujadili huo Muswada katika Kamati. Ingetosha kwamba mchango wangu niliotoa katika Kamati hapa nisingesimama kutoa mchango mwingine. Lakini kwa sababu nina mambo machache ambayo na mimi yananigusa kama Mbunge ninayo machache sana na nilikuwa naomba niyazungumzie.

Mheshimiwa Spika, la kwanza liko katika kifungu cha 6 kile kinachoanzisha Bodi ya Umeme Vijijini. Pale panasema lengo la kuanzisha hiyo Bodi ya Umeme Vijijini ni kukuza ama kuendeleza shughuli za kijamii na kiuchumi Vijijini kwa kuwezeshwa Vijiji vikapata umeme ili ziweze zikapatikana huduma nzuri kama za afya na kadhalika kama ilivyoelezwa pale. Lakini katika kifungu cha 6 (2) katika mabano kifungu cha (c) kinaeleza kwamba katika kugawa hizo fedha kwa ajili ya hiyo kazi itafanyika kwa ufanisi na katika hali ya ushindani kwa miradi ambayo itaonekana ina *social economic benefits* na ile ambayo itahakikisha kwamba inaleta uwiano wa kimaendeleo katika Mikoa na ile miradi ambayo itakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, hii ni kweli na hilo pia limezungumzwa au limetiliwa mkazo katika jedwali la kwanza pale ukurasa namba 65 iliposema kwamba: *For the purpose of regional equity the Board may differentiate grants by region and location.* Sasa mimi nilikuwa naogopa sana kama tutasema kwamba hii miradi ambayo tunakusudia kupeleka Vijijini tuanze kuiangalia kwa kuangalia vigezo kama *social economic benefits.* Kama tutafuata hii sana tutaendelea kuigawa nchi hii. Wengine wataendelea kupata umeme na wengine wataendelea kukaa gizani muda wote. Kwa hiyo, kigezo kama hiki nilikuwa naomba kisiangaliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu iliamua kugawanya Umeme wa Mijini na Vijijini. *TANESCO* imeachiwa ishughulike na Umeme wa Mijini kwa sababu kuna uwezekano au hali ya kibiashara mijini ni kubwa. Kuendelea na hatua kubwa ya Umeme

Vijijini ambako ni huduma tu ilionekana kwamba haiwezekani. Na ndiyo sababu iliyotufikisha leo kuanzisha huu Muswada ili Vijiji vyote nchini viweze kupata umeme kwa sababu Umeme Vijijini si wa biashara ni huduma. Kwa hiyo, hilo nilikuwa naomba ndio kiwe kigezo cha kupeleka hii miradi huko Vijijini. Kwa hiyo tusiangalie sana suala la kuangalia ile *social economic benefits.*

Mheshimiwa Spika, umeme ni kichocheo kikubwa sana cha maendeleo. Mimi sina uhakika au sina ushahidi ni mahali gani kulipelekwa Umeme Vijijini au katika Kijiji baada ya kufika umeme kijijini watu wakahama katika hicho Kijiji eti kwa sababu kuna umeme. Sijaona mahali umeme umeanzishwa shughuli ndio zikazidi kupungua za kiuchumi. Kwa hiyo, ninachotaka kusema mahali popote umeme ukifika kwa sababu kuna uwezo wa kuanzisha shughuli nyingi za kiuchumi na za kimaendeleo basi umeme upelekwe kwenye shughuli zote hizi za maendeleo ya kiuchumi na kadhalika. Zitaanzishwa na hatimaye kama ni mapato yanaweza yakazalishwa kutokana na huo umeme ambao umepelekwa.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa kwenye Kamati tulielezwa kwamba Serikali imejitahidi kuondoa kodi hasa ya *VAT.* Lakini katika taarifa yetu ya Kamati, Kamati imeendelea kupendekeza kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa kodi na hata wazungumzaji wengine waliotangulia vile vile wamezungumzia suala hilo. Mimi kama Mbunge wa Manyoni Magharibi, nipo hapa na ninaendelea kusisitiza kwamba Serikali iondoe kodi kwa vifaa vya umeme Vijijini. Nasema hivyo naomba niiondoe wasi wasi Serikali kwa sababu itakapoondoa kodi katika hivi vifaa, hivi vifaa vitanunuliwa, vitatumika kupeleka Umeme Vijijini na hawa wananchi watakapopata umeme wa uhakika wataanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kimaendeleo. Matokeo yake watakapokuwa wanafanya shughuli zao za kibiashara watapata uwezo wa kuendelea kulipa kodi kwa Serikali. Kwa hiyo, itakuwa ni njia mojawapo ya kufidia hii kodi ambayo Serikali sasa hivi tunaiomba isamehe.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna lingine amelizungumza Mheshimiwa Shekifu. Kama nilivyosema kwamba tulipokuwa kwenye Kamati Serikali ilisema kwamba inaondoa *VAT* na hapa tunaendelea kuomba Serikali iondoe kodi kwa vifaa vya umeme. Lakini nilikuwa naomba niulize je, hivi Serikali inavyokubali ku-*forego* haya mapato yake kwa kuondoa hiyo *VAT* na kodi nyingine lengo ni kuhakikisha kwamba mtumiaji wa mwisho anafaidika kwa kuondolewa kwa hii kodi. Lakini ina utaratibu gani Serikali kuona kwamba kweli lile lengo la kufanya huyu mtumiaji wa mwisho aweze kufaidika ina utaratibu gani? Nilikuwa naomba hapa kama Serikali itasamehe kodi na ile *VAT* iliyosamehewa basi iangalie inatumia njia gani kuhakikisha kwamba huu msamaha kweli mtu wa mwisho anafaidika isiwe ni nafasi inatolewa kwa huyu mfanyabiashara kuzidi kunufaika yeye zaidi badala ya mtumiaji wa mwisho. Nilikuwa naomba kama alivyozungumza Mheshimiwa Shekiffu, mtani wangu pale kwamba ikiwezekana kwa kutumia *EWURA* pamoja na kwamba hatuna utaratibu wa kusimamia bei hivi sasa basi *EWURA* isaidie katika kuona kwamba ile kodi iliyosamehewa kweli inamfikia mtumiaji wa mwisho ili kuwe na maana katika kuondoa hii kodi kwa mlaji wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ya kuomba hii kodi iondolewe kuna mpango ulioanzishwa na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji unaitwa *Business Environment Strengthening Programme in Tanzania (BEST).* Katika huu mpango Serikali ilikwishasema kwamba biashara au uchumi binafsi ndio unaotegemewa uwe ndio injini ya uchumi katika nchi yetu katika kukuza uchumi wetu na baadaye kuondoa umaskini. Sasa katika huu mpango kati ya mambo yanayosisitizwa ni kuangalia vikwazo gani ambavyo hawa wafanyabiashara ambao wanakumbana navyo ikiwezekana katika sheria ama katika kanuni ziweze kuondolewa ili huyu mtu aweze kunufaika apate mazingira mazuri ya kufanya biashara na baadaye awe mlipa kodi mzuri wa Serikali. Hii ndiyo sababu ya pili ambayo nilikuwa naomba kwa Serikali ijaribu kuondoa hiyo kodi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo nataka kuzungumzia ni kifungu namba 16 kile cha uteuzi wa miradi. Tunasema kazi zile za *Rural Energy Agency* moja itakuwa ni kuteua miradi ya kufanyiwa tathmini lakini vile vile kuteua watu au wakandarasi watakaotekeleza mradi ambao utakuwa umeteuliwa kwa kigezo cha ubora wa mradi, kijamii na kiuchumi. Lakini vile vile tulivyokuwa kwenye Kamati kulikuwa kuna *Organization Identification Chart* imeonyeshwa pale katika hiyo *Chart* Kitengo cha *Promotion and Project Electrification* ambacho kitafanya kazi ya kifungu Namba 2 na 3 kwa maana ya kuteua miradi na kuteua watu ambao watatekeleza hiyo miradi.

Lakini hapa nikawa najiuliza suala la kwanza kutakuwa na utaratibu gani kuona kwamba kila Wilaya miradi yake inatambuliwa na kufanyiwa tathmini. Lakini la pili ni nani anaamua miradi ya Wilaya hii itazamwe na miradi hii isitazamwe. Sasa nilikuwa naomba katika kifungu hiki hii *Agency* itakapokuwa inafanya kazi basi ihakikishe kwamba miradi ya kila Wilaya inatazamwa. Vinginevyo tusipoangalia itakuwa inatazamwa miradi ya maeneo fulani na maeneo mengine hayatazamwi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba liangaliwe. *(Makofi)*

Lakini lingine lipo katika jedwali la 1 ukurasa Namba 65 ile ibara ya 9. Inasema kwamba Bodi itaangalia miradi gani ambayo inastahili kupewa kipaumbele na hii miradi tunayoizungumzia ni ya kijijini. Hivi katika kuteua hii miradi ambayo inapewa kipaumbele ni vigezo gani vitaangaliwa. Ni vizuri hivi vigezo vikawekwa wazi ili kama kutaanza kutekelezwa miradi ya aina hiyo basi kusiwe na manung'uniko kwamba miradi ya maeneo fulani ndiyo inayotazamwa tu na miradi ya maeneo mengine haitazamwi. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie juu ya Muswada ulioko mbele yetu. Kwanza nitoe pongezi kubwa kwa Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Nishati Vijijini.

Ni muda mrefu Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tunapiga kelele hapa kuomba umeme uende maeneo yetu na hasa tukizingatia kwamba wananchi wetu wengi sasa hivi wameshajiandaa kwa kupokea umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwa sababu wamejenga nyumba za kisasa, wameshajiandaa kupokea umeme kwa ajili ya kuanzisha

viwanda vidogo vidogo, kama vile vya kukamua mafuta, useremala, uchomeleaji na kazi zingine muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hili ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba Mfuko huu unaanza na kama wenzangu walivyochangia Mifuko kama ya *TANROAD* ilianza kwa kuweka fedha mapema. Lakini huu Mfuko sisi tunaomba pamoja na kazi nzuri ambao Serikali ya awamu ya tatu imefanya Serikali kabla haijamaliza muda wake itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha Mfuko huo. Niseme umeme kwenda Vijijini ni huduma kama vile tunavyopeleka maji kwa wananchi wanaokaa Vijijini.

Kwa hiyo, huu umeme unaokwenda Vijijini usiwe na lengo la kumkomoa mwananchi anayeishi Vijijini, uwe na lengo la kumwezesha. Kama wenzangu walivyochangia kwanza vifaa vya umeme vipunguzwe bei, gharama ya kuingiza umeme ndani ya nyumba zipunguzwe na mashine zinazokwenda kwa ajili ya kazi za Vijijini nazo ziondolewe kodi. Wananchi wetu wamejiandaa na wakisikia huu mradi unakwenda kwa kweli watafurahi sana na wataipongeza Serikali yetu kwa kazi nzuri inayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme huu unaokwenda usigeuke kuwa mwiba kama ule wa *IPTL* ambao sasa hivi unatugharimu fedha nyingi sana. Pia ningeiomba Bodi inayoteuliwa izingatie kuwahusisha watumiaji wa umeme huu wasiwekwe watu ambao hawahusiani moja kwa moja na Wanavijiji. Mimi ningeshauri Mwenyekiti wa Bodi hii kama Bodi zingine ambazo zinateuliwa Mwenyekiti wa Bodi hii si mbaya akiteuliwa na Rais kama Bodi zingine zozote zile kwa sababu kwa kweli mtu kama Rais ana busara zake na ana imani atateua mtu ambaye atawasaidia sana wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwa vile mambo ya nishati kama wenzangu ambavyo wametangulia kusema ni masuala ya Muungano. Mimi naomba na wenzetu wa Zanzibar waingizwe kwenye mpango huu tusianze kubaguana, twende wote sambamba kwa sababu mambo yanayohusu Muungano yanatuhusu sisi wote. Mfuko huu ni Mfuko muhimu ambao unagusa Watanzania wote na mimi naomba uongozi utakaokuwa ndani ya Mfuko wasiwe wabaguzi, waangalie Tanzania yote Wilaya zote, Vijiji vyote.

Mimi niungane na wenzangu tuwe na Wawakilishi Mikoani, tuwe na Baraza la Ushauri la Mkoa kama vile ambavyo tunafanya *TANROADS.* Tuwe na *RTC* na hii itatusaidia sana kwa sababu *RTC* ikishapendekeza na kwa sababu inahusisha Wilaya zote tutakuwa na uwiano mzuri wa kupata umeme. Mimi nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Muswada huu.

Kwanza naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kilosa kuwapa pole Ndugu na jamaa wa Marehemu Balozi Paul Bomani. Pia Ndugu na jamaa wa Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria.

Mheshimiwa Spika, sisi katika jimbo la Kilosa tulipata bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Alipotembelea katika Kijiji cha Berega pamoja na kazi alizozifanya pia alikagua Hospitali ya Berega na kuzungumza na wafanyakazi wa hospitali hiyo iliyokuwa chini ya Kanisa la *Anglican.*

Baada ya hapo alitembelea Shule ya Sekondari ya Mgugu na kujionea mwenyewe mapungufu yaliyokuwepo katika shule hiyo. Wakati alipokuwa anazungumza na wafanyakazi wa Hospitali ya Berega alielezwa matatizo ya hospitali ile. Moja ilikuwa ni madawa na pili ilikuwa ni mahitaji ya kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, alipotembelea Shule ya Mgugu alijionea mwenyewe upungufu wa magodoro kwa watoto wa shule na pia alijionea mwenyewe upungufu wa jengo la Maktaba ya shule. Alitoa ahadi baada ya kupata maelezo ya wafanyakazi wa Hospitali ya Berega ya kupeleka dawa na pia alitoa ahadi ya kupeleka magodoro na kutoa fedha kwa ajili ya kujengea Maktaba. Ahadi hizo alikwishatekeleza zote.

Lakini alipopata ahadi ya umeme aliichukua na baada ya muda mfupi tuliona Meneja wa Mkoa wa *TANESCO* kuja katika maeneo yaliyoombewa mradi huo wa umeme ili kufanya mchanganuo. Alikuja kwa barua aliyoandikiwa na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, alifanya mchanganuo huo ili kujua kama mradi wa umeme unalipa. Aliona unalipa. Baada ya hapo tulipata bahati ya kutembelewa na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Msabaha, akapita sehemu zile zile ambazo tuliomba mradi upelekwe na yeye aliona kweli mradi unalipa.

Sasa ombi langu katika kuunga mkono Muswada huu Mheshimiwa Waziri ajue kwamba ahadi hii au ombi hili lilikwishatolewa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na pia mchanganuo kwa barua iliyotoka Wizarani kwa Meneja wa Mkoa wa *TANESCO* ulikwishafanya na kuonekana mradi unalipa. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba katika utekelezaji wa Bodi hii wataweka kipaumbele katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa kuwa madhumuni ya Muswada huu ni kuchochea uendelezaji wa huduma za Nishati Vijijini ili kusaidia juhudi za kujenga uchumi, kuinua hali ya maisha Vijijini na kupunguza umaskini.

Kwa kuwa Serikali tayari imeshajenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika jimbo la Kilosa na pia kwa kuwa Vijiji vingi katika jimbo la Kilosa wananchi ni wakulima wadogo wadogo tayari wameshajijengea wenyewe miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri Bodi hii wakati wa utekelezaji wake itoe kipaumbele cha kupeleka umeme katika Kijiji cha Lumuma, Kijiji cha Kidete, Mwassa, Kikundi, Nzaganza, Mvumi, Msowelo, Kitete, Mfuru, Madudu, Ludewa, Gongoni, Kimamba A, Kimamba B na Kijiji cha Mbigili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo natazamia Mheshimiwa Waziri amenielewa na i*nshallah* atatusaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii leo asubuhi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Muswada ambao uko mbele yetu.

Lakini kabla sijafanya hivyo naomba uniruhusu na mimi nitoe kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Mlalo salaam za rambirambi kwa kumpoteza ndugu yetu, kaka yetu Balozi Ahmed Hassan Diria na Mzee wetu Marehemu Paul Bomani hivi karibuni na kwamba tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. *(Amin).*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru na ninafurahi sana kuona kwamba Muswada huu umeletwa, kusema kweli Muswada ulioko mbele yetu inawezekana umechelewa kidogo kwa sababu kama walivyosema wenzangu umeme ni mwanzo wa maendeleo ya kila aina. Umeme ni kichocheo cha maendeleo yote. Kwa hiyo, kuleta Muswada huu sasa, ni maandalizi makubwa ya uwezekano wa kupata maendeleo makubwa kwa wananchi wetu hasa kule Vijijini tunakotoka.

Mheshimiwa Spika, mahali ambapo pamepata umeme Vijijini kama unaweza ukatembelea Kijiji ambacho kimepata umeme miaka miwili iliyopita, leo maisha ya eneo hilo ni tofauti kabisa na wakati huo kabla hawajapata umeme. Watu watakuwa wamechangamka sana, ustaarabu umeingia na kwa kweli maendeleo yanaonekana waziwazi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kusema kwamba hata ile programu yetu tunayoizungumzia ya Mpango wa Uzazi Vijijini, maeneo ya Vijijini yakipata umeme kwa kweli mpango ule pengine hata utakuwa hauna nguvu tena zaidi kwa sababu watu wazima hawawezi tena kulala saa moja, saa mbili, watakuwa watu wanalala saa tano, saa sita kwa sababu watu watakuwa na shughuli za kufanya na hasa michezo ya usiku. Ni maendeleo ya kila namna hasa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumza mengi hapa. Lakini pia tukiweza kupata umeme Vijijini tutaokoa sana mazingira yetu ya Vijijini. Kama walivyosema wengine, hivi sasa kuna kazi kubwa sana inayoendelea huko ya kukata miti kwa wingi na kuchoma mkaa. Sasa shughuli hii ikifanyika mapema na kwa kweli *agency* hii ikifanya kazi na hela zikipatikana, tutapunguza sana uharibifu wa mazingira hasa ukataji wa miti ovyo huko Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia naamini kwamba umeme ni chanzo kikubwa cha kupambana na umaskini, maana yake miradi mbalimbali ya maendeleo itaweza kuibuka mahali ambapo pana umeme. Sasa kwa sababu ya hayo machache niliyoeleza na walivyoeleza wenzangu, Serikali tafadhali isijitoe kama kabisa katika utaratibu huu wa

kupeleka umeme Vijijini. Maana Serikali ikijitoa ni sawa na kwamba Serikali imemwachia mtu mwingine mwekezaji maisha ya Watanzania katika kupambana na umaskini wao, maendeleo yao na huduma mbalimbali za maisha. Kwa hiyo, Serikali iliyochaguliwa na watu tafadhari isifanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningekuwa radhi kabisa Serikali ikijitoa *TANESCO*, ikimpa mwekezaji *TANESCO* na hata kujitoa kwenye shughuli zake kwa sababu *TANESCO* ikifanya kazi Mjini, Mijini kuna Taasisi nyingi za waziwazi ambazo mahitaji ya umeme ni lazima. Mjini kuna viwanda, kuna watu ambao hawawezi kukaa bila umeme. Mijini kuna vifaa mbalimbali vinavyoweza kutumia umeme. Kwa hiyo, biashara ya umeme Mijini wala haina haja ya kutangaza *tender*. Kwa hiyo, naiomba kabisa Serikali isijiondoe hata kidogo katika mpango huu wa kupeleka umeme Vijijini. Mambo ya *facilitation* wanaweza kufanya, lakini lazima wawe bega kwa bega na *agency* hii ambayo tunatarajia kuiunda hivi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme Vijijini pia ni kuboresha mazingira ya elimu. Mimi naishauri sana Serikali wakati *agency* hii inaanzishwa nitaomba kabisa maeneo mengine ya uwekezaji, basi wale wawekezaji waelekezwe wapi wapeleke umeme. Tusiwaachie wafanye wanavyotaka, vinginevyo matumaini ya Watanzania wengi juu ya utaratibu huu yatakuwa hayana maana sana. Kwa sababu hivi sasa tunajenga Shule nyingi za Sekondari huko Vijijini na Shule hizi nyingi haziko katika maeneo yenye umeme.

Napendekeza, miradi hiyo ya kwanza pamoja na kupelekwa kwenye Vijiji vinavyohitaji, matumizi ya nishati hiyo ya umeme lakini miradi mingi ielekezwe kwenye maeneo ya Shule ya Sekondari ambazo tunajenga hivi sasa. Kwa kweli tukifanya hivyo tunatimiza ule wajibu wa Serikali wa kuwaendeleza Watanzania kwa pamoja na kwenda sambamba na wenzetu. Hivi sasa Shule nyingi za Mijini zinafaidika sana na elimu ya sasa ya sayansi na teknolojia, utandawazi na masuala mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Kwenye gazeti hapa nimesoma, mwenzangu mmoja ametoa *computer* kwenye Shule zake kule. Lakini kwa sababu kuna umeme! Kama hakuna umeme, basi *computer* hizi zitakuwa hazina faida. Ni vizuri watoto hawa wanaosoma kwenye Shule za Sekondari za Vijijini, basi miradi kama hii, *agency* hii na fedha hizi zielekezwe kwenye Shule zile ili hatimaye nao waweze kutumia *computer,* waweze kujua *internet* ni nini, waweze kujua *email* na Watanzania wote waende sambamba mbele siyo kundi moja liende mbele kwa kujua elimu na maendeleo ya kisasa zaidi na wengine wakaachwa nyuma. Tafadhali naomba jitihada hizo zifanyike hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na wenzangu kwamba vifaa vya umeme Vijijini kwa kweli viondolewe kodi kama tuna nia ya kuwasaidia wakazi wa Vijijini. Maana huku tunachochea maendeleo, tunachochea watu waanze kuuchukia umaskini, watu waanze kuufurahia ustaarabu, watu wapende kuona kwamba sasa na wao wameingia kwenye mtandao wa maisha ya dunia ya leo. Kwa kuwa ndiyo tunavyofanya sasa hivi, basi ni vizuri vifaa hivi viondolewe kodi na pia tuangalie hata mchango wa umeme wenyewe kule Vijijini, njia mbalimbali ziangaliwe na kodi nyingine ziweze kupunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahia sana kwamba Muswada huu ukipitishwa kwa kweli utaleta mabadiliko makubwa kwenye miradi ya maendeleo na maisha yenyewe ya wananchi wa Vijijini. Katika Muswada huu nimesoma kwamba kuna ule Mfuko mkubwa wa Nishati Vijijini, lakini kuna mifuko mingine mbalimbali itakayoanzishwa, inaitwa mifuko maalum.

Sasa labda baadaye tungepata maelezo kidogo, Waziri atakapahitimisha hoja yake, ile mifuko maalum midogo itashughulika na kitu gani. Inatoka na Mfuko huu mkubwa au ni mifuko ambayo itatokana na fedha gani na shughuli zake zitakuwa ni nini?

Mheshimiwa Spika, narudia kusema kwamba maendeleo yoyote kwa kweli yana vichocheo vyake. Sasa moja ya kichocheo kikubwa tumefika mahali pake ni nishati hii ya umeme Vijijini. Kwenye Shule, tafadhali kuwepo umeme. Kule kwangu sasa hivi tuna Shule za Serikali zilizojengwa kwa nguvu za wananchi kama kumi, tumejenga na Shule za Mashirika mengine. Sasa bila kuwapatia msaada huu wa miradi kama hii, kwa kweli maendeleo yatapishana sana ya elimu na hata maendeleo yenyewe kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hayo machache. Nina hakika mengine mengi wenzangu wameyachangia, lakini niseme tu kwamba ninaunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia kwa kuwa unatuletea mwanga Vijijini, ustaarabu maendeleo na Serikali isijitoe tafadhali. Afadhali ijitoe *TANESCO* kuliko kujitoa kwenye *agency* hii ya kupeleka umeme Vijijini. Nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki unatosha wasemaji wasiozidi wanne, nao ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimiwa Leonard Shango.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia Muswada huu ambao ni muhimu sana. Awali ya yote na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Korogwe na Mkoa wa Tanga kwa ujumla kutoa rambirambi kwa familia na ndugu wa Marehemu waliotutoka, Hayati Balozi ndugu yetu Mheshimiwa Hassan Diria pamoja na Balozi Paul Bomani ambaye alikuwa Makamu wa Chuo Kikuu cha Dar es Saalam. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaongea na mimi naomba nitamke tu rasmi kwamba naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa sababu ni Muswada muhimu na kwa kweli umekuja kwa wakati ambao ni muafaka. Mengi yamezungumzwa, sheria za Bunge hazitaki turudierudie yale ambayo wenzetu wameshazungumza. Mimi nataka tu nitoe ushauri kwa chombo hiki ambacho kinaundwa sasa. Nina mambo matano ambayo naomba niyasisitize kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunajua katika dunia nzima kwamba sasa hivi kuna kilio kikubwa cha uharibifu wa mazingira. Kwamba, nishati kubwa inayotumika Mijini na

Vijijini ni mkaa na kuni. Vijijini tunatumia kuni na Mjini nako tunatumia kuni na mkaa. Kwa hiyo, kwa kweli kwa Muswada huu na Wakala huu kuundwa ni kuokoa hali ambayo nchi yetu na dunia nzima hasa nchi, inaweza kuwa jangwa. Maana ukipita barabarani unavyoona magunia ya mkaa na hali ikiendelea hivi, basi tutaweza kujikuta kwamba nchi yetu inakuwa jangwa kwa sababu nishati inayotumika zaidi na wananchi walio wengi ni hiyo.

Kwa hiyo, nishati hii mbadala ambayo wakala huu unaoundwa utatusaidia kabisa kuweza kutafuta vyanzo mbalimbali vya nishati mojawapo ikiwa umeme wa maji*, biogas, gas* yenyewe na vitu vingine. Kwa hiyo kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Daniel Yona pamoja na Naibu wake ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na wataalam hawa kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kuuleta Muswada huu. *(Makofi)*

Naomba kushauri machache tu kwamba yale ambayo yamo kwenye ibara ya 4 sehemu ya 16 kwa kweli kuna mambo mengi tu, kama kazi za wakala ziko nyingi pale, lakini nasisitiza kipengele kile cha (d) mpaka (e) kwa kweli kifanyiwe kazi ya ziada kabisa kwa sababu kila kitu pale kimeelezwa na uko ushauri ambao mimi ningependa kutoa katika ile ibara ya 16 ambayo inaeleza kazi halisi za wakala na ushauri ambao utafanywa. Yako mambo ambayo ningependa niyasisitize ambayo wenzetu Wakala wangeyasisitiza hayo, basi hata hizi shughuli za gharama umeme katika Vijijini vyetu zingepungua. Nina mambo matano ambayo ninaomba niyasisitiza katika mchango wangu.

La kwanza kabisa ambalo naomba Wakala ifanye ni kwamba Wakala watakaofanya hii miradi katika Vijiji wanakoweka umeme katika Vijiji fulani fulani, naomba waweke umeme katika Kijiji chote. Tuna uzoefu katika baadhi ya Vijiji vyetu katika nchi yetu, umeme unawekwa katika Kitongoji fulani. Hawaweki katika Kijiji chote. Sasa mimi naomba wenzetu walione hilo. Mimi nina mifano na siyo kwangu tu, nimeona katika Vijiji vingi katika nchi yetu kwamba *TANESCO* walikuwa na tabia ya kuweka mahali umeme, lakini Kijiji kile kinaweza kuwa na Vitongoji na ni kirefu, lakini wanaweka sehemu fulani tu. Kwa mfano Mashewa hapa wameweka umeme lakini ni Kijiji kirefu na hakiwekwi chote. Kwa hiyo, inakuwa miaka yote Kijiji kile kina umeme lakini sehemu nyingine hazina umeme.

Kama kweli tunaweza kusaidia wananchi, basi kuwe na utaratibu kwamba ule mradi unaotengenezwa wakati huo kama Wakala wanaweka, basi iwe ni Kijiji chote kiwe kinapatiwa umeme. Nikitoa mfano kama Mashewa, umeme umewekwa Mjini tu, lakini kuna sehemu inaitwa Kijungumoto na sehemu nyingi hazina umeme kabisa na ni gharama kubwa. Kwa hiyo, ni vizuri *project* ya umeme ikifanya katika eneo, basi ikamilishwe katika eneo lote badala ya kupita sehemu fulani. Nina mifano mingine kama kwa Mndolwa. Umewekwa umeme kwa Mndolwa, lakini kwa Meta hakuna umeme, au sehemu za Mgombezi umewekwa umeme lakini kuna Kitongoji kingine cha mgambo hakina umeme. Hivi ni vitu ambavyo kwa kweli naomba Wakala wakiamua kuweka umeme mahali, basi waweke Kijiji chote.

Ushauri wa pili ambao ningependa kutoa ni kwamba, vipo Vijiji vingi ambavyo nguzo za umeme zinapita karibu yake. Sasa mradi kama huu, kwa Wakala kinachotakiwa pale ni *transfomer* na gharama ndogo. Sasa badala tena ya kuanzisha kitu kipya, ni vizuri basi yale maeneo ambapo umeme unapita na Vijiji vinapita, tufanye kama wanavyofanya *TANROAD* kwamba barabara inapotengenezwa, inachukua Vijiji vingi mpaka mwisho.

Kwa hiyo, ni vizuri basi wenzetu Wakala walione hilo kwamba zile sehemu ambazo nguzo ziko karibu, basi ziwekwe *transfomer* ili maeneo hayo umeme uweze kupatikana kwa urahisi kuliko kuanza mradi mpya. Ni mradi ambao unahitaji *transfomer* tu na maeneo hayo yako mengi katika Vijiji vyetu. Hilo nilikuwa nasisitiza sana ambalo ni jambo rahisi na kuweza kufuatilia kupata umeme.

Ushauri wa tatu ambao naomba Wakala wazingatie ni ahadi ambazo Mawaziri waliopita katika Wizara hii wamekuwa wakituahidi humu ndani ya Bunge, kwamba watatuwekea umeme.

Sasa ukisoma *speeches* za Mawaziri waliopita, Mheshimiwa Daniel Yona utachoka maana tumeahidiwa humu Bungeni mpaka wote tumechoka. Tumeahidiwa umeme, tena kuna siku moja nakumbuka Mheshimiwa Dr. Shija alituambia kila Mbunge tuweke kwenye *pigeonhole* Vijiji gani anataka umeme. Tukaandika kweli kweli lakini mpaka leo hatujapata.

Sasa nadhani Wakala wana sehemu ya kuanzia, watufanyie kazi hiyo. Ndiyo yale wenzangu wanayosema kwamba tunapokuwa na *Regional Consultative Council* inakuwa rahisi ku-*monitor* na kujua kwamba ni Vijiji vingapi ambavyo havijapata umeme. Kama ilivyo kwenye barabara, tunakaa tunaamua kwamba barabara zimegawanywa katika *grade*. Basi hata umeme nao tungesema vile Vijiji ambavyo vilianza kuahidiwa na Mawaziri waliopita huko enzi na enzi, basi vianze kupata umeme halafu tunakuja mpaka vya Mheshimiwa Waziri Daniel Yona. Hiyo ingetusaidia sana. Ni ushauri tu ambayo ungeweza kutusaidia maana ziko ahadi hapa nyingine ni za miaka nenda, miaka rudi.

Mheshimiwa Spika, lingine limezungumzwa na wenzangu, lakini ni muhimu naomba nilirudie. Sasa hivi uko mwamko katika nchi yetu ya kuendeleza Sekta ya Elimu kwa kiwango cha juu sana. Tunasema kwamba kila Kata iwe na Sekondari, lakini tukubali kwamba Sekondari bila umeme kwa kweli Sekondari hiyo haitakuwa na mafunzo ya kutosha. Hili ni suala la msingi sana ambalo Mheshimiwa Charles Kagonji amelizungumza. Ni vizuri nalo tukalipa kipaumbele. Lazima waelekezwe kwamba kama tunaanzisha Sekondari kwenye Kata bila umeme hatuwezi kupata mafanikio.

Kwa hiyo, tungeweza kuweka kabisa kwamba katika kigezo kimojawapo katika Wakala ni kuhakikisha kwamba Sekondari zinapata umeme. Ziko baadhi ya Sekondari nazo zimepitiwa na nguzo za umeme, hizo zingeanza mara moja wala Mheshimiwa Daniel Yona asicheleweshe hilo. Ziko *Secondary Schools* ambazo zimepitiwa na nguzo za umeme karibu, hizo ndiyo zingeanza moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba nilizungumze na ambalo wenzangu wameshauri ni kwamba kweli Serikali ipende isipende isijitoe kabisa kwenye suala hili.

Hilo lazima kabisa Serikali labda ndiyo ingekuwa na *share* kubwa kushinda wengine wote ili kuhakikisha kwamba kweli zoezi la kupata umeme linafanikiwa, vinginevyo hatutafikia lengo letu la kusema kwamba tunapunguza gharama ya umeme. Gharama ya umeme kama Serikali inajitoa, itazidi tu kwa sababu mwekezaji anataka faida kubwa. Kama tunataka umeme wa Vijijini kweli usaidie wanavijiji kwa maana ya kujikwamua na uchumi na mambo mengine ambayo tumeyazungumza, bila Serikali kuweka mkono wake pale, gharama hiyo itaendelea kuwa kubwa tu. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, nisisitize kabisa kwamba *VAT* kwenye vifaa vya umeme na vifaa vya umeme kwa kweli Serikali ingefuta kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikuwa na mengi, ni hayo tu. Naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu hoja hii ya msingi sana juu ya nishati Vijijini. Mimi moja kwa moja naunga mkono hoja hii ipite kwa asilimia mia kwa mia kwa sababu za msingi zifuatazo nilizoziona:- *(Makofi)*

Kwanza Sekta binafsi ikishirikishwa itachangia kusambaza umeme Vijijini kwa haraka zaidi badala ya Serikali peke yake kufanya kazi hiyo. Hata hivi tumechelewa sana, tungeshirikisha Vijiji vingi na maeneo mengi yangekuwa na umeme. Hiyo ndiyo sababu ya kwanza na hasa baada ya kusoma Muswada kwa makini.

Pili, itaharakisha maendeleo mbalimbali yafuatayo:- Umeme ukienea katika maeneo mbalimbali Vijijini na kadhalika utaharakisha kukua kwa uchumi, sisi sote tunajua uchumi unajengwa na wananchi walio wengi zaidi Vijijini. Kwa hiyo, wananchi waliowengi zaidi wakipata umeme ni nyenzo ya kuleta maendeleo kwa haraka sana na tutakuwa tumeinua kiwango kikubwa kabisa katika kujenga uchumi.

Lakini pia kingine ni teknolojia ya kilimo cha umwagiliaji. Sisi sote tunategemea kilimo na tunakwama kwa sababu hatuna nyenzo za kusaidia kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, umeme ukienea katika maeneo mbalimbali, teknolojia hii ya kilimo cha umwagiliaji itapata mchango mkubwa zaidi. Lakini pia kuna kuchochea kwa ufundi wa aina mbalimbali kule Vijijini. Uko ufundi ambao umedumaa kule kwa sababu hakuna nyenzo ya umeme. Kwa hiyo, umeme ukienea utachochea sana maendeleo ya ufundi mbalimbali, lakini pia viwanda vidogo vidogo. Tunazungumza viwanda vidogo vidogo, lakini bila umeme haviwezi kushamiri na wala haviwezi kuzaa matunda. Lakini tukipata umeme huu ambao Serikali imeleta Muswada wa kushirikiana na hawa mawakala, kwa maana hiyo tutapata umeme wa kutosha katika maeneo mbalimbali, basi tutaimarisha viwanda vyetu na kuanzisha viwanda vidogo vidogo, lakini pia kuwapunguzia kazi wanawake, hasa kazi zile za harubu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sulubu.

**MHE. KHALID S. SURU:** Sulubu ndiyo, hata ukiangalia Kamusi hata harubu ni sawa sawa. Harubu, sulubu ni sawa sawa. Kwa hiyo, tutakuwa tumewapunguzia kabisa matatizo akina mama. Kazi ambazo zingefanywa kwa mikono zitafanywa kwa mashine na kadhalika. *(Makofi)*

Lakini pia huko Vijijini kuna Zahanati mbalimbali zinashindwa kutumia hata vifaa vya kisasa, darubini na kadhalika. Umeme ukienea katika maeneo hayo, matibabu yatakuwa ya kweli na yatakuwa ya msingi kabisa. Lakini lingine, maendeleo ya kisasa yataibuka karibu kila kona. Lingine ni kwamba, kompyuta zitaingia pia Vijijini, maana sasa hivi kompyuta ziko Mijini mahali ambapo pana umeme. Sasa umeme ukienea huku Vijijini hata kompyuta zitaenea, zitatakiwa zitumiwe na wananchi kwa mujibu wa maendeleo ya sasa.

Mheshimiwa Spika, labda tuone hali ya sasa ya nishati nchini na hasa Vijijini. Kasi ya usambazaji umeme Vijijini si ya kutosha, ni ya pole pole sana. Kwa hiyo, matumizi ya teknolojia ya kisasa kutokana na jua na upepo na nyenzo nyingine bado hazijazaa matunda vizuri Vijijini. Kwa hiyo, ndiyo maana na Serikali imeleta Muswada huu na mimi nauunga mkono ili tuweze kuharakisha maendeleo haya ya msingi kabisa huko Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo na mimi naunga mkono kwamba bei ya umeme ni kubwa sana na ikiendelea kuwa kubwa zaidi hata tukipeleka hii nishati kule Vijijini wananchi maskini hawawezi kumudu. Tutapeleka sanamu tu ya nyaya wananchi watashindwa kabisa kufunga umeme kwenye nyumba zao. Wote tunajua wananchi wetu bado ni maskini, hawana uwezo wa kukabili matatizo makubwa. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe tunaona umeme huu haupandi bei na hata ukishushwa ni vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania, pamoja na kuboreshwa kiutendaji, lakini bado limekuwa linasuasua katika kusambaza umeme Vijijini. Hata pale mahali ambapo pana nyaya za umeme zimepita katikati ya Kijiji lakini umeme haukushushwa na wananchi wamekuwa wakilalamika wakati fulani hata wanafanya hujuma kwa sababu umeme huo uliopita hapo hauwasaidii. Lazima tutoe mfano wa hali halisi. Kwa mfano kule Kondoa, kuna nyaya zimepita katika Vijiji fulani, lakini mpaka leo havijapata umeme. Kila siku wanaieleza Serikali kwamba hawajapata. Lakini kwa sababu Waziri atasikia, vile Vijiji na ataviandika na naomba afuatilie ili vipate umeme maana ni zaidi ya miaka sita au saba umeme uko angani tu. *(Makofi)*

Vijiji hivyo ni hivi vifuatavyo:- Kijiji cha Mji Mdogo wa Bereko, Kijiji cha Pahi, Salanka, Masawi, Kikilo, Bukulu, Humai, Kwadinu, Kolo na Choka. Hawa watu wamevumilia kiasi cha kutosha. Sasa tunaomba Serikali iwasaidie kupitia sheria hii, aidha umeme wa *Grid* au utaratibu wa hao mawakala umeme huo uwafikie haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ziko dalili za mpango wa kuleta umeme katika baadhi ya Vijiji kule Kondoa katika mwaka huu wa 2005 na hasa kwenye Jimbo la Kondoa Kaskazini. Viko Vijiji kama sita, kuna Gereza la King'ang'a, Mheshimiwa Waziri baadaye atafuatilia; kuna Kijiji cha Kingale, ni Mji Mdogo; kuna Iyoli, Kolo,Mnenia na kuna Mji Mdogo wa Pahi. Programu hiyo naomba itekelezwe maana kuna kawaida ya kutoa taarifa halafu wakati mnatengeneza bajeti mnafuta tena. Mimi sitaki ifutwe, tutapambana tu kwenye Kamati. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Wakala wa Nishati Vijijini na kwa mujibu wa Muswada huu, naomba Kata zifuatazo, zifikiriwe kupata umeme mara baada ya sheria hii kupita, tutakuwa tumeongeza nguvu ya kusambaza umeme. Moja ni Kata ya Masange, Kata ya Kisese, Kata ya Kikore, Kata ya Chang'aa, Kata ya Haubi, Kata ya Busi na Kata Thawi. Zote hizo zifikiriwe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri azingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mawakala wapatikane haraka ili waweze kukabidhiwa kazi katika nchi nzima, lakini Kondoa isisahaulike kwa maana ya Kata hizo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawatakia ushindi katika uchaguzi wa mwaka 2005 Waheshimiwa Wabunge warudi wote. Lakini pia Mawaziri na Naibu Mawaziri warudi na warudishwe kwenye nafasi zao. Nawatakia kwa nia njema kabisa, lakini na mimi mniombee Mungu nirudi Bungeni. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nashukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi mchana huu niweze kuchangia machache katika Muswada ambao uko mbele yetu. Lakini kama ilivyokuwa ada, naomba na mimi kabla ya kuchangia nitoe pole na rambirambi zangu kwa jamaa na ndugu kwa aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole na rambirambi kwa familia na jamaa ya Balozi Bomani ambaye alikuwa Mkuu wa Chuo cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Wakristo wa dhehebu la Kikatoliki na watu wote wapenda amani duniani kwa kumpoteza Kiongozi mmoja ambaye alikuwa anasimamia amani duniani Papa Yohane Paul II. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote mahali pema Peponi. Amen.

Baada ya kusema haya ya utangulizi na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge, niipongeze Serikali kwa kweli kwa kuleta Muswada huu mbele ya Bunge. Muswada huu ulikuwa umesubiriwa kwa muda mrefu lakini bila shaka maandalizi yenyewe ndiyo yamecheleweshwa kuletwa mapema zaidi ya leo. Kwa hiyo, napenda kuishukuru Serikali kwa kufanya jitihada kubwa ya kuweza kuandaa Muswada mzuri na kuuleta leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi siyo kawaida yangu kuunga mkono Muswada wakati wa kuanza kuzungumza, lakini kwa Muswada huu, napenda nitamke kabisa naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba nichangie maeneo machache tu ya Muswada wenyewe. Kwanza napenda niangalie vyombo au Taasisi ambazo zinaundwa na Muswada huu. Ukisoma Muswada huu utaona kuna Taasisi nne zimeundwa. Nazo ni:-

(1) Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Board);*

(2) Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency);*

(3) Mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund);*

(4) Wakala wa Mfuko *(Trust Agent)* .

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri hivi vyombo kweli vyote tunavihitaji! Nasema hivi kwa sababu ukisoma Muswada utaona vyombo hivi vyote vinahitaji gharama katika uendeshaji. Bodi yenyewe inahitaji kuendeshwa kwa gharama, ukichukuwa Wakala wa Nishati Vijijini, ndio kabisa. Kwa sababu pale ilipendekezwa kwamba kuwe na Mkurugenzi wa Kimataifa mwenye sifa za Kimataifa ingawa sasa hivi wamerekebisha kidogo. Lakini kuwe na Mkurugenzi na Watumishi na hawajasema ni Watumishi wangapi wanahitajika. Lakini inaonekana Watumishi wengi sana wataajiriwa katika eneo hili kwa sababu ya majukumu ambayo yameelezwa katika Muswada huo.

Pia Mfuko wa Wakala nao unaelezwa namna utakavyoendeshwa, pia nao unahitaji gharama. Wakala wa Mfuko unaelezwa, mpaka Mabenki yanapendekezwa kuwa Wakala wa Mfuko. Mimi nafikiri itakuwa ni gharama kubwa sana. Lengo letu ni kupata pesa za kuweza kusaidia kueneza umeme Vijijini. Lakini tukishaunda vyombo vingi namna hiyo, nina uhakika kwamba sehemu kubwa ya mapato ya Mfuko yataingia katika uendeshaji wa vyombo hivyo na matokeo yake ni kwamba walengwa hawatanufaika na Mfuko huo.

Kwa hiyo mimi napendekeza Serikali iangalie mahali gani pa kuweza kupunguza. Mimi kwa haraka haraka ningeweza kusema chombo kile cha mwisho yaani Wakala wa Mfuko *(Trust Agent)* angeondolewa tu, sioni kazi yake. Kazi hiyo ingeweza kufanywa na Wakala wa Nishati Vijijini ambayo ina wataalam wengi sana. Pia, kama haiwezekani kuondoa au kupunguza vyombo hivi, basi tuangalie katika ajira tusiajiri watu wengi sana kiasi cha kuweza kugharimu hela nyingi sana za kuendesha Taasisi hiyo. Kwa hiyo napendekeza aidha tupunguze vyombo, ama tupunguze Watumishi katika vyombo hivyo. Kwa hiyo katika eneo la kwanza hilo ndilo pendekezo langu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili linahusu Wajumbe. Katika Sehemu ya Saba ya Muswada, inapendekezwa aina ya Wajumbe wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini ambayo imeorodhesha Wajumbe hao na sina sababu ya kuwataja.

Lakini katika sehemu ndogo ya sehemu hiyo ya Saba, Sehemu ndogo ya tatu inapendekeza kwamba Mjumbe atakayetajwa ama aliyetajwa katika sehemu ndogo au Sehemu ya Saba, sehemu ndogo ya (i) au (j) asiwe na haki ya kupiga kura. Sielewi sababu kwa sababu haijaelezwa. Huyu ni Mwakilishi wa kikundi kinachoitwa *Development Partners.* Sasa huyu kwa nini ananyimwa kupiga kura na kwa nini tunamweka kwenye Bodi? Kama ni mtu wa kualikwa, tusimweke kwenye Bodi, awe anaalikwa tu. Lakini kama tunamworodhesha kwenye Muswada kwamba ni Mjumbe halafu tunamkataza kupiga kura, mimi sioni mantiki yake.

Kwa hiyo mimi napendekeza kwamba kipengele hicho cha Tatu cha Sehemu ya Saba ya Muswada kingefutwa ili Mjumbe aliyetajwa katika sehemu ya 7(1)(j) aweze kupata haki ya kupiga kura. Sioni sababu ya kutokupiga kura kama ametajwa katika Muswada au Sheria.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye vyanzo vya mapato vya Mfuko. Katika Sehemu ya Kumi na Tisa ya Muswada imeainishwa vyanzo vinne vya mapato ya Wakala wa Nishati Vijijini. Vyanzo hivyo ni Bajeti ya Serikali ya kila mwaka, mchango wa Wafadhili, ushuru wa asilimia tano kwenye umeme utakaozalishwa kibiashara na kuunganishwa kwenye *Grid* ya Taifa. na mwisho ushuru wa asilimia tano kwenye umeme utakaozalishwa kwa ajili ya matumizi binafsi.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi na kipengele cha tatu na nne ambavyo vinahusu ushuru. Unapoanza kuweka ushuru kwenye umeme tangu awali kwa kweli mimi ninafikiri ni kuongeza gharama. Sisi au nchi yetu ukilinganisha na nchi za jirani mpaka sasa gharama iko juu sana ya umeme. Sasa ukiongeza tena ushuru kwenye umeme unaozalishwa na kuunganishwa na *Grid* ya Taifa, utakuwa unaongeza gharama kwa wateja. Kwa hiyo suala la gharama ya umeme litakuwa bado juu na itaendelea kupanda kama tutakubaliana na vipengele au kipengele cha tatu. Kwa hiyo napendekeza kipengele hicho kifutwe.

Jambo la pili, kuwatoza ushuru wa asilimia tano wazalishaji ambao wanazalisha umeme kwa ajili ya matumizi binafsi, kwa kweli mimi nafikiri tunakwamisha uzalishaji. Mimi nilifikiri kwamba Serikali ingependekeza kwamba hawa watu binafsi ambao wana uwezo wa kuzalisha umeme kwa ajili ya matumizi yao binafsi, tungewapa nafasi. Lakini tukiwekewa kikwazo cha ushuru wa asilimia tano ya gharama wanayoitumia, kwa kweli itakwamisha. Lengo la Serikali la kusambaza umeme Vijijini halitafikiwa kwa sababu tutawakwamisha na wengi watasita kuzalisha umeme kwa sababu ya ushuru huo ambao tumeuweka. Kwa hiyo pia napendekeza kwamba kipengele hicho kingeondolewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo, naomba niende kwenye uteuzi au nafasi ya Mkurugenzi Mkuu. Katika Sehemu ya 25(2) ya Muswada inapendekezwa kwamba Mkurugenzi huyu wa Wakala wa Nishati Vijiji, sifa ambayo ilikuwa imependezwa ni kwamba apatikane kwa ushindani wa Kimataifa. Nashukuru kuona kwamba katika marekebisho Waziri ameliona hili na ameliondoa. Lakini pia bado nasisitiza kwamba pamoja na kuondoa neno lile *internationally* halafu akaacha tu

sentensi ibaki hivyo, mimi ningefikiri angeweka neno lingine zaidi. Mimi ningependelea liwekwe neno *nationally* yaani ushindani huo uwe ndani ya nchi. Kwa hiyo neno *nationally* lingewekwa ili kuzuia watu wa nje kugombea nafasi hiyo.

Hii ni kwa sababu tunao wataalam wengi sana ambao wamebobea katika masuala haya. Sasa tukiacha tu wazi ni kwamba yeyote anaweza kuchukua nafasi hiyo. Lengo letu si kuunda chombo cha Kimataifa hapa, lengo letu ni chombo cha Kitaifa. Tunao wataalam wa kutosha na wa kuweza kushika nafasi hiyo kama nafasi ya Mkurugenzi Mkuu kwa hiyo hatuna sababu ya kutafuta mtu mwingine nje. Kwa hiyo naomba neno *nationally* liongezwe pale ili kuweza kubana ile nafasi kwa Watanzania peke yao.

Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu ya mwisho ya usambazaji wa umeme Vijijini, katika Muswada imependekezwa kwamba wakati wa kugawa miradi katika nchi nzima, basi waangalie uwiano mzuri kwa kila Mkoa. Lakini wenzangu waliotangulia kuzungumza wamekwenda zaidi wakasema tuangalie kwamba uwiano mzuri wa usambazaji uende hadi ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo na mimi ninaungana nao kwamba tuangalie usambazaji kwa kila Wilaya, Mkoa kama ilivyokuwa *TANROADS,* kuwe na utaratibu wa kuweza kusambaziwa ama utaratibu wa miradi ya kusambaza umeme katika Vijiji husika. Kwa hiyo jambo hili lizingatiwe sana na Mfuko wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo ningependa nilichangie ni kuhusu vyanzo vya nishati yenyewe. Muswada huu haukutaja sana vyanzo gani vitatumika kusambaza nishati Vijijini. Lakini mimi ningependa nikumbushe kwamba tuna nishati ya jua ambayo ni nyingi sana katika nchi yetu. Nishati hiyo sasa iweze kutumiwa zaidi na ikiwezekana na Nishati ya Makaa ya Mawe ndio nishati ama vyanzo vikubwa sana ambavyo viko nchini, kwa hiyo vitumike hivyo zaidi. Mimi ninaona kwamba nishati ya jua ina gharama nafuu sana. Tungeweza kukazana kutumia nishati hiyo, usambazaji wa umeme ungekwenda haraka zaidi katika Vijiji vyote kuliko kuendelea kutumia nishati ya *Grid* ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na narudia kusema kwamba naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada uliyo mbele yetu. Awali ya yote naungana na wenzangu kutoa rambirambi kwa familia ya Marehemu Balozi Diria aliyekuwa Mbunge mwenzetu na Balozi Paul Bomani waliyofariki hivi karibuni. Mungu awape mapumziko ya milele.

Mheshimiwa Spika, mimi pia naunga mkono mia kwa mia Muswada huu. Nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Yona kwa kutuletea Muswada huu kwa wakati huu. Lakini mimi naungana na wenzangu kusema kwamba Muswada huu ungekwishaletwa wakati Bunge lilipoanza yaani wakati wa kipindi chetu, kwa sababu ndio tungeufanyia kazi vizuri zaidi na tungeona matokeo yake katika Vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika madhumuni ya Muswada huu umejumuisha waziwazi mambo ambayo nitanukuu, kwa ruhusa yako naomba kusoma: “Madhumuni ya Muswada huu ni kuweka utaratibu wa kisheria kuanzisha Wakala wa Mfuko Vijijini ili kuratibu juhudi na kuendeleza nishati za kisasa Tanzania Bara, kuchochea uendelezaji wa nishati bora na kuhakikisha ukuaji wa huduma za nishati Vijijini ili kusaidia juhudi za kujenga uchumi na kuinua hali ya maisha Vijijini.”

Mheshimiwa Spika, mimi ninavyoona, Muswada huu ungeletwa pamoja na kuainisha kuwa unapoongea kuhusu maendeleo Vijijini unaongea kuhakikisha kwamba uchumi unakua na umaskini unatokomezwa. Kwa hiyo katika Muswada huu, ni sitaongea kuhusu Taasisi ambazo zinatakiwa kuundwa. Nitaongea kuhusu *impact assessment* ya Muswada huu katika Vijiji vyetu.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme siyo suala la kuwa ni kitu cha burudani tu. Nishati ni muhimu katika kusaidia juhudi za kuendeleza uchumi wetu na kuboresha maisha ya wananchi. Sasa tunapokuwa tunaongea mara kwa mara tunataka kuendeleza Vijiji vyetu na kweli Vijiji viko gizani. Mimi sijaona kama tumefanya juhudi za kuendeleza Vijiji. Lakini Muswada kama huu ungekwenda sambamba pamoja na sekta zile ambazo zinahusu Vijiji kama Kilimo, Maji, Afya na Elimu. Kwa sababu suala la teknolojia la kisasa haliwezekani pasipokuwa na umeme. Katika sekta hizi zote unapoleta umeme patakuwa na *leakages* na *multiplier effects.* Kama wenzangu walivyosema, utaona mabadiliko haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, sisi tumeona katika Vijiji vyetu ambavyo vimepata umeme, vimebadilika haraka haraka, unaona watu wanajituma,wanajihamasisha. Watu wanakuwa na muda mdogo wa kujipumzisha kwa sababu wanataka kujishughulisha. Sasa mimi ningeomba tu kuwa labda tufikirie kuwa Mfuko huu pamoja na Wakala sasa upewe jukumu la kwanza la kuhakikisha kuwa maeneo ya Vijijini ndiyo ambayo yatanufaika na nishati hizi ambazo zitapelekwa.

Pia, ningeomba labda Muswada huu ufafanue, hatuwezi kuwa na Mfuko au Wakala pasipokuwa na vyanzo vya kutosha. Mimi ningeomba labda baada ya kupitisha Muswada huu, *TANESCO* sasa ijihusishe na kuzalisha umeme tu. Usambazaji iwe Mijini au Vijijini liwe jukumu la Mfuko pamoja na Wakala. Hii ndio itakuwa chanzo kikubwa cha kuuwezesha Mfuko huu kufanya kazi zake. Nasema hivyo kwa sababu mahali pengine ndivyo inavyofanyika. Hili suala la kusema kuwa *TANESCO* na jeuri yake tuiachie iendelee mpaka Mikoani, bado itatukwimisha.

Mimi nina uzoefu ambao niliupata katika nchi moja kuwa umeme ulipopelekwa Vijijini, ulisimamiwa na Ofisi ya Rais. Kweli mabadiliko yalikuja katika sekta mbalimbali kwa sababu hiyo inayoitwa *multiplier effects and leakages,* ilifanya kazi. Sasa Mfuko huu na Wakala huu ndio ungepewa jukumu la kusambaza umeme ambao unazalishwa na *TANESCO. TANESCO* iendelee kuzalisha na kuuza umeme kwa Mfuko na kwa Wakala. Sasa tukiwa na *TANESCO* Wilayani, Mikoani na Mfuko, Wakala pia wako kule wote, itakuwa ni vurugu mechi. Mimi ningeomba mambo haya yafikiriwe

sana. kwa sababu kukiwa na Taasisi moja ambayo inawajibika, tutaweza kuiwajibisha pale ambapo inaonekana haitafanya kazi vya kutosha. Sasa hivi Mameneja wengi wa *TANESCO* katika Mikoa wengine walikuwa na tabia zao za kuona kwamba kupeleka umeme Vijiji ni kupendelea, siyo haki. Lakini ningeomba sasa Muswada huu baada ya kupitisha, Mfuko na Wakala uchukue jukumu la kusimamia usambazaji wa umeme kuanzia Mijini mpaka Vijijini.

Ningeomba pia suala la Mfuko huu na Wakala upewe nguvu za kisheria kusudi uweze siyo tu kupata ruzuku kutoka Serikalini au vyanzo vingine humu ndani, uweze kuchupa nje kwenye Taasisi za Kifedha za Kimataifa. Sasa hivi miradi ambayo Taasisi nyingi kama za *African Development Fund, AIDA,* zinapendelea sana miradi ya *Rural Electrification Project.* Sasa suala hili pia liangaliwe siyo tu kuwa tuunde Mfuko, sasa tuwe na Taasisi zetu zilizo hapa ndani zifanye kazi za ndani.

Mheshimiwa Spika, suala la maendeleo ni suala la Kimataifa. Kwa hiyo nguvu zaidi ziongezewe kwa kukopa nje. Mikopo ambayo inatokana na Taasisi kama *African Development Fund, URICA Development Fund* au *AIDA* ina masharti nafuu sana. Kwa hiyo ningeomba suala hili lisiwe tu kuanzisha leo, halafu tuone kuwa itakuwa tatizo la kuwa haina uwezo. Pia, Mfuko huu na Wakala uje na labda Muswada huu ungekuwa na Jedwali la mipangilio ya kila Wilaya na Kata ya jinsi umeme utakavyopelekwa kule. Siyo wao watoe maamuzi yao ya kuwa tutapeleka Kilimanjaro au Tanga halafu na Mikoa mingine ambayo imesahaulika iendelee kusahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jedwali ni la muhimu sana kuwa katika Wilaya kama ya Iramba, Vijiji fulani vitanufaika kwa mwaka huu na huu. Labda na kwa Wilaya wa Sumbawanga hivyo hivyo kusudi kuepusha suala la upendeleo. Pia ningeomba katika utawala mzima wa Mfuko huu na Wakala huu wawe na Ofisi zao Mikoani kama ikiwezekana, waanze na Kanda siyo wakae Dar es Salaam, kila kitu mtu atoke Vijijini aende kuwaona Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama za umeme, tunajua kweli umeme hata ukipelekwa kwa gharama za sasa, wananchi wengi hawatafaidika na huduma hii kwa sababu bei ni ya juu sana. Sasa ningeshauri kuwa, katika Muswada huu kuwekwe utaratibu wa kusaidia Mfuko huu kwa kupunguza makali kwa watumiaji wa umeme. Yaani kuwe na ruzuku au *subsidies* ambazo hizo ndizo zinaweza kupatikana kupitia labda Bajeti zetu ambazo tunazipitisha kila mwaka za Serikali, katika mikopo au misaada itatoka katika Mashirika ambayo yatashirikiana na sisi katika kuendeleza Vijiji vyetu.

Kwa hiyo, suala nzima la umeme Vijijini vitazame vyanzo vingine. Mambo kama *biogas* kwa wafugaji itakuwa ni muhimu sana kwa matumizi madogo madogo ya nyumbani na mambo ya *solar* na upepo. Sasa uwekezaji katika maeneo haya ndio wawekezaji wangehimizwa katika maeneo hayo. Pia, kwa sababu tunataka; Je, tuna umeme wa kutosha kupeleka Vijiji vyote? Kwa hiyo sasa ni wakati muafaka na muhimu kuwa mahali ambapo unasikia kuna *Songo Songo Gas, Mnazibay Gas* na makaa ya mawe katika maeneo fulani , yale ndio wapewe Wawekezaji wakubwa mara moja na siyo suala tena la kuandika majarida na kuendelea kuandika *report*. Lakini tuhakikishe kuwa

umeme katika maeneo haya unazalishwa. Kwa sababu umeme wa sasa hata tukitaka hautatosha kupeleka kwa Vijiji vyote, ni kidogo. Mahitaji ni makubwa lakini kwanza hata kutabirika kuzalishwa kwake ni vigumu kwa sababu unategemea maji.

Kwa hiyo ningeomba Mfuko huu ndio usimamie pamoja na Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati katika kutafuta Wawekezaji iwezekanavyo katika maeneo yale ambayo yanaweza kuzalisha umeme kwa wingi ambao utatosheleza kwa Vijiji ambavyo vinataka mabadiliko ya haraka kwa kila Kijiji. Ni muhimu katika Vijiji ufike kwa sababu hali halisi ya sasa, siyo tu kuwa tunadidimia, lakini ukitazama sana utaona kuwa vijana wetu wengi wanakimbilia Mijini na kuondoka Vijijini. Sasa suala nzima la nguvukazi linahama. Kwa hiyo kuboresha mazingira Vijijini itakuwa vizuri sana na itasaidia katika vijana kujiendeleza na kuendelea kutumikia Vijiji vyetu katika kuzalisha kwenye kilimo na viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea haya, mimi naomba kusema tena kwamba naunga mkono hoja hii na Muswada huu lakini ningesema tu kuwa, kweli lazima tuone kwamba umuhimu wake ndio huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kufikia hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Kwa hiyo, kutokana na orodha yetu, Prof. Maghembe ajiandae kuwa wa kwanza katika kipindi cha mchana. Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 jioni.

*(Saa 6:50 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11:00 Jioni)*
*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini wa Mwaka 2005 *(The Rural Energy Bill, 2005)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. PROF. JUMANNE ABDALLAH MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kwanza mchana huu kutoa mawazo yangu kuhusu Muswada wa Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini wa mwaka 2005.

Kwanza kabisa napenda nitoe pole nyingi sana na rambirambi kwa kifo cha jirani yangu hapa Mheshimiwa Mbunge wa Rahaleo, Mzee Hassan Ahmed Diria, ambaye alifariki katika kipindi hiki, kati ya Bunge la 18 na leo. Ninaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri pia niwape pole na kutoa rambirambi kwa familia ya Mzee wetu aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mzee wetu

Paul Bomani kwa kifo ambacho kimetokea hivi karibuni. Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wa kutengeneza Mfuko wa umeme Vijijini umekuja wakati mzuri labda hata wengine tungesema ungekuja kabla ya leo tungefurahia zaidi. Huko Vijijini hali iliyoko ya nishati ni mbaya sana na wengi huko Vijijini wanatumia nishati ya kuni, mkaa na bidhaa nyingine za miti ambayo uharibifu wake wa mazingira sasa umeanza kuwa dhahiri nchi nzima. Kwa hiyo, Mfuko huu utengenezaji wake umekuja wakati muafaka na tungependa tuwapongeze wenzetu kwenye Wizara ya Nishati na Madini hasa Mheshimiwa Waziri na wataalam wake tuwapongeze sana kwa kuleta Muswada huu wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapowapongeza ni vema tukatafakari mambo muhimu ambayo yapo katika Sekta hii. Kitu cha kwanza ingefaa tutafakari na kujua kwamba katika nchi yetu tunao uhaba mkubwa sana wa umeme. Ukitaka kujua ufikirie kwamba sisi ni nchi ambayo inaendelea na tunaweka vivutio kwa ajili ya wawekezaji na wawekezaji wengi ambao wanahitaji kutumia umeme. Lakini uzalishaji wetu wa umeme wakati huu hauzidi *Megawatt 600*. Sasa ukilinganisha na nchi kama *South Africa* ambao wanazalisha umeme kiasi cha *Megawatt 38,000,* basi utakuta sisi labda uzalishaji wa umeme wote tulionao tunaoweza kutumia ni kama umeme wa Mji mdogo kule *South Africa.*

Kwa hiyo, tungependa kuleta Makampuni makubwa ambayo yanaweza kuongeza uzalishaji hasa katika sekta ya *manufacturing* hatuna uwezo wa kuwapa umeme. Kama tutawapa umeme, basi tutawapa umeme kwa njia ambazo kwa kweli siyo muafaka. Sasa matokeo ya kuwa na uhaba wa umeme mkubwa kiasi hiki na kuzalisha umeme kidogo hivi ni kwamba umeme bei yake nchini kwetu ni kubwa sana. Umeme wa majumbani bei yake ni kubwa sana.

Kule kwenye Jimbo langu kule Mwanga, kumekuwa na jitihada kubwa za kupeleka umeme Vijijini. Mimi kwa hili, ninaishukuru sana Serikali tangu miaka ya 1980, 1990 na wakati huu kwa kutupelekea umeme katika maeneo mengi. Lakini bei leo ya kuunganisha umeme kwa mwananchi, umeme unapita hapo nje aunganishe nyumbani kwake ni Sh.204,000/=. Sasa wananchi wa Mwanga mapato yao yote yale mwaka mzima kila mmoja ni Sh.150,000/= wastani wao. Sasa kama wanatakiwa kuunga umeme kwa Sh.200,000/= maana yake wanakula fedha yote ya mwaka huu na fedha ya mwaka kesho hakuna chakula, hakuna watoto kusoma, hakuna nguo. Sasa ni dhahiri kwamba umeme wa gharama ya namna hii, wananchi wale hawawezi kumudu.

Ni ukweli kwamba kumekuwa na utaratibu kwamba walipe kwa awamu. Lakini kweli awamu ya watu wanaopata fedha zao zote mwaka mzima Sh.150,000/= hata ukiwaambia walipe awamu kwa Sh.70,000/= halafu ndiyo wapate umeme, bado ni ghali kweli kweli.

Kwa hiyo, tunahitaji kwa kweli tutafute njia ya kuteremsha bei ya umeme. Lazima tuteremshe bei ya umeme. Haiwezekani kwa bei iliyopo hapa tujidanganye kwamba tutapeleka umeme Vijijini. Utapelekaje? Utapeleka umeme, waya utafika, lakini wananchi hawatatumia umeme. Umeme huu ni ghali kweli kweli. Sasa licha ya hiyo, bei ya *Watt* ya umeme, *unit* ya umeme inayotumika nyumbani ni kubwa sana. Kwa bei ya sasa kwa kweli ambayo ukitumia umeme mwingi unalipa zaidi, ukitumia umeme kidogo unapunguziwa.

Mambo haya ni mambo ya ajabu sana maana kwenye bidhaa ukitumia nyingi unapunguziwa bei, lakini katika umeme nchi kwetu ukitumia umeme mwingi unalipa zaidi. *Negative economics.* Maana unakuwa *discouraged* usitumie *units* nyingi. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kama tunata kweli wananchi hawa waondokane na umaskini na waende mbele, lazima watumie umeme zaidi wazalishe. Sasa kama wakitumia *units* nyingi wanalipa zaidi, hii ni *negative economics.* Madhara yake yanaonekana wazi. Wananchi wengi, wote hapa tuliopo humu ndani wengi wetu tunatumia mkaa kupikia. Siku hizi kuni zinaletwa Dar es Salaam watu wanakoka moto nje wanapika ugali. Madhara yake yanaonekana, misitu yote inakatwa. Watu wanasema hapa ni hekta 90,000 hii ni *estimate* ya huko nyuma wakati umeme ulikuwa bei rahisi sana.

Sasa hivi misitu inafyekwa na balaa yake wote mnajua. Hata hivi sasa tulivyotoka Dar es Salaam tunakuja hapa Dodoma mto wa Wami hapa katikati ya masika umekauka na mito yote. Ukitoka Lushoto unakwenda Moshi njiani ile mito iliyokuwa inapita chini ya daraja zote, yote imekauka. Ukitoka Moshi mpaka Arusha mito yote imekauka. Hivi mnadhani mito inakauka kwa sababu gani? Misitu yote imekatwa ama imepasuliwa mbao lakini mingi imegeuzwa mkaa tumepikia ugali.

Sasa umeme wetu mwingi unatokana na maji. Sasa kama maji yenyewe hatuwezi kuyatunza yakawa mtoni yakazalisha umeme tunaacha misitu inakatwa na maji yakauka hivi huko mbele umeme tutatoa wapi? Ni kama yule mtu anapanda juu ya ngazi akifika juu anaanza kukata chini, ukikata chini ngazi itakatika wewe utaanguka na nyingine chini itaanguka. Kwa hiyo, ni vyema kabisa tukatafuta njia ya kutunza misitu yetu, tukapunguza bei ya umeme, tuka-*subsidize* mafuta ya taa, watu wengi wakatumia mafuta ya taa badala ya kuni na *gas* tuliyopata Songo Songo tukai-*subsidize* ikawa rahisi watu wakatumia *gas* kupikia na matumizi ya nyumbani ili tupunguze uharibifu wa mazingira ambao unaikumba nchi yetu.

Hivi sasa mvua hainyeshi vizuri, inanyesha mabaka mabaka tu, kwa sababu hakuna kizuizi kinachozuia unyevu unapotoka baharini, ukusanyike unyeshe mvua ambao inaaminika. Mito inakauka kama ninavyosema, kiwango cha *carbon* kwenye hewa yetu kimeongezeka sana na kiwango cha joto hivyo hivyo kimeongezeka na kwa hiyo mvua hazinyeshi. Kwa hiyo, lazima tutafute njia tupunguze bei ya umeme. *(Makofi)*

Katika viwanda ukilinganisha bei ya umeme viwandani, Kenya, *South Africa* na Tanzania utakuta bei yetu ni kubwa sana na viwanda vyetu haviwezi kushindana kwa sababu hiyo na umeme wenyewe huu unakatikakatika. Kwa hiyo, kama una kiwanda

kama cha *Cement,* umeme ukiwa unakatikakatika ina maana kwamba lazima uwashe mara kwa mara  na kuwasha zile mashine zipate moto ni gharama kubwa sana na viwanda vingi vina matatizo hayo.

Kwa hiyo, lazima tuangalie upya, hivi kwa nini tusizalishe umeme kutokana na makaa ya mawe na tunayo makaa tele kule Mchuchuma, Kiwira. Kwa nini tusiongeze uzalishaji wa *gas* ya Songosongo? Tunayo *gas* nyingi Songo Songo, Mnazibay, nimeambiwa hata kule Mingoyo iko *gas*. Kwa nini tusizalishe umeme zaidi kule *Stigler's gorge* na ile ina-*potential* ya kuzalisha zaidi ya mara mbili ya umeme ambao tunao na tunazalisha kwenye vi-*hydro plant* kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini wakati huu sasa tusianze *dialogue* kwamba hivi kweli, hivi tunavyozalisha umeme hii ni *sustainable* kweli au namna gani kwa sababu maji tunayataka tunywe, maji tunataka kumwagilia mashamba yetu na maji hayo hayo tunataka kuzalishia umeme. Hivi kitu gani muhimu hatuwezi kupunguza uzalishaji wa umeme kutoka kwenye maji tukaongeza kwenye makaa ili maji haya tukamwagilie mashamba? Nchi nzima ina njaa, watu hawasemi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kushauri kwa kweli kwamba wakati umefika tuanze kuzalisha umeme wa kutosha na umeme bei yake iwe rahisi. Tutapeleka umeme Vijijini na Mfuko huu ambao mimi naunga mkono, lakini tutapeleka umeme ambao hautakuwa na mtumiaji kwa sababu wananchi hawana uwezo wa kununua umeme kwa bei hii ambao tunauza sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie hapa kwa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya pili kati ya wazungumzaji mchana huu. Kwanza kabisa,  ningependa nitamke wazi kwamba naunga mkono hoja hii.  Lakini vile vile, ningependa nitoe rambirambi zangu kwa kifo cha Mzee wetu Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo Zanzibar, ambaye imempendekeza Mwenyezi Mungu kumchukua. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza mwenzangu aliyetangulia sasa hivi, Mheshimiwa Profesa Maghembe na ninaungana naye katika *concerns* zake alizozitoa hasa juu ya gharama ya umeme. Kwa hiyo, tunashindwa kupanga vizuri mipango yetu kwa sababu gharama za umeme zinatuzidi nguvu. Kwa hiyo, utakuta kana kwamba mwaka 2000 katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tumetamka wazi kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano tutajitahidi kusambaza umeme katika Vijiji vyote vilivyo karibu na *Grid* ya Taifa ya Umeme.  Sasa tazama baada ya miaka mitano kwa kweli hili ni eneo ambalo mafanikio yake ni mazuri lakini siyo makubwa hata kidogo.

Katika Jimbo langu la Kalenga, Kijiji ambacho kimeweza kupata umeme ni Kijiji cha Magubike Kata ya Nzihi. Kulikuwa na Vijiji vingi ambavyo vilikuwa kwa kweli vipate umeme kama Wenda, Muwimbi na Vijiji vingine vingi. Lakini haikuwezekana kwa sababu gharama ni kubwa mno na wakati huo tulipokuwa tunafanya *restructuring,* wenzetu hawa *wa Net solution* ndio walikuwa wanaingia. Kwa hiyo imeshindikana, kwa hiyo tunapoanzisha Mfuko huu wa Nishati Vijijini ni wazi ni hatua muhimu inayoashiria hali njema ya maisha yaliyo bora kwa wananchi Vijijini kama kweli tutajidhatiti na kufanikisha mpango huu.

Kwa mfano sasa hivi tuna mpango wa *MMESS,* kujenga Shule za Sekondari na tumejipanga kwamba tujenge Shule za Sekondari kila Kata. Sasa Shule hizi ziko huko Vijijini. Shule ya Sekondari kama hakuna umeme huwezi kuwa na uhakika kwamba kutakuwa na elimu bora, lazima wajifunze masomo mbalimbali. Kwanza tu wao wenyewe kusoma kwao kama wanakaa kwenye mabweni lazima wasome usiku, halafu vile vile mafunzo kwa vitendo ya Sayansi kama hakuna umeme, ni vigumu kuweza kujifunza.

Kama kweli tutafanikisha mpango huu, basi Shule zetu hizi tunazozijenga zitakuwa na mafanikio makubwa. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Kalenga, mwaka 2000 tulikuwa na Shule mbili za Sekondari zilizojengwa na Wananchi, Shule ya Sekondari ya Kalenga na Shule ya Sekondari ya Isimila. Sasa hivi inaonekana na tukisaidiwa na mpango huu wa *MMESS* pamoja na nguvu za wananchi, tunaweza kabla ya Uchaguzi Mkuu tukawa tumekamilisha Shule nyingine za Sekondari tisa. Kwa hiyo tukawa na Shule 11. *(Makofi)*

Tunajenga na tumeshafungua Shule ya Kiponzelo na Wasa, karibu tunafungua Shule ya Sekondari Lumuli halafu Lyandembela, Mgama, Luhota, Mseke Kiwele na Kidamali. Natamka hivi ili wananchi wangu kule wawe na matumaini kwamba tunazungumzia mambo muhimu yanayoleta matumaini kwamba Shule hizi wanazozijenga zinaweza kweli zikapata umeme na watoto wao wakaweza kusoma na kupata elimu iliyo bora. Nisipozungumza mimi, nani atazungumza tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimesoma vizuri Muswada huu, nimepata faraja niliposoma kifungu cha 19 (3) ambacho kinaonyesha vyanzo vya mapato ya Mfuko huu wa Nishati Vijijini, maana tunaweza tukaanzisha Mfuko ikawa hakuna fedha inayoingia. Kwa hiyo ikawa ni Mfuko hewa. Vyanzo vinavyoonyeshwa vinaonekana ni vyanzo vya uhakika. Kwa hiyo naona huu Mfuko kweli utakuwa na fedha, lakini chanzo kimoja ambacho ni kizuri sana ni kile ambacho kitatokana na fedha zinazotokana na Bajeti ya Serikali, *Annual Budget Allocations.*

Ningependekeza kwamba Mheshimiwa Waziri ajitahidi kwamba katika hizo *Budget Allocations* angalau kila mwaka *minimum* fedha zinazotolewa zisishuke kiwango fulani ili tuwe na uhakika kwamba Mfuko huu uko *sustainable*, lakini kama itakuwa tunapata fedha nyingi safari hii, safari ijayo zinaeleweka na kadhalika, Mfuko huu utakuwa *sustainable*.

Kwa hiyo ni vyema tuwe na fedha za kutosha, *reasonable amounts* ambazo zitauwezesha Mfuko huu kuweza kufanikisha mipango yetu. Nimesoma vile vile Muswada huu namna mipango ya umeme itavyoendelezwa Vijijini ambapo tutatumia *developers* na kuweza kutoa *grants*. Wasiwasi wangu ni kwamba, unaweza kukuta kwenye Wilaya fulani hawajitokezi *developers* ambao wapo tayari kuomba fedha ili kuendeleza umeme Vijijini. Kwa hiyo unaweza ukakuta umeme unakwenda kwenye Vijiji vingi vya Wilaya fulani ambako wako watu ambao wako *more aggressive* wanaweza wakaziomba fedha hizi. Kwa hiyo, ni vyema Mheshimiwa Waziri atazame kwa upeo mkubwa kuhakikisha kwamba Sheria hii ili iweze kuwa ina haki mbele ya wananchi, lazima *rural electrification* ifanyike kwa Wilaya zote nchini. *(Makofi)*

Halafu nimeshindwa kuelewa juu ya uendeshaji wa umeme Vijijini. Sasa baada ya kuwa tumesambaza umeme Vijijini kutumia Mfuko huu, nani atakuwa anaendesha umeme huu Vijijini? Je, ni *TANESCO* au *TANESCO* haihusiki au ni *developer*? Lakini mimi nilidhania *developer* anafanya kazi yake akikamilisha ana mahali pa kukabidhi Mradi huu kwamba tumekamilisha, ndio maana unakuwa *verified* kwamba umekamilika. Sasa nani anayeendesha miradi na inaweza kuwa pengine ni umeme wa *solar* au *biogas*, ni *TANESCO* watakaosimamia miradi kama hiyo.

Naona kwenye Miswada haijionyeshi wazi wazi nani atasimamia, lakini vile vile ningependa nione kwamba *TANESCO* ina *role* maalum kwa mfano kama suala la *verification*. Suala la kiutaalam kwamba umeme umefungwa vizuri una usalama, *TANESCO* ndio shirika lililo na wataalam wa kutosha kuweza kutuonyesha kwamba umeme huu unaosambazwa Vijijini hauwezi ukaleta hatari yoyote kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile sasa hivi tunayo hii teknolojia mpya ya *LUKU.* Ningeomba teknolojia hii iingie Vijijini tunapofanya *rural electrification* ili wale wanaopata umeme waweze kununua umeme kulingana na mahitaji yao. Lakini wakiwa wanatumia ile teknolojia ya zamani, anatumia umeme baadaye inamshinda kulipa *bills* zinazokuja, umeme unakatwa ndio mwisho wa *electrification*. Lakini kama anakuwa amenunua mwenyewe kiwango hicho, ikizima basi imezima. Akipata fedha tena ya kwenda kununua nyingine anawasha umeme wake anaendelea. Hii ni teknolojia nzuri. *(Makofi)*

La mwisho ni juu ya vifaa vya umeme, nyaya za umeme, *transformers,* sasa hivi zinaibiwa sana. Kwa *transformer* ni mafuta ya *transformer*. Tusipoangalia tunaweza tukafanya *rural electrification* halafu wajanja wakatuibia nyaya na mafuta ya *transformers,* kwa hiyo mipango yetu ikahujumiwa. Mimi ningependa tu nimwulize Mheshimiwa Waziri, hivi *suspect* mkubwa anaweza kuwa nani? Mwananchi wa kawaida kweli anaweza akapanda hayo manguzo ya umeme akaenda kufumua nyaya za umeme huko au akatoa mafuta ya *transformer!!* Lazima awe ni mtaalam wa mambo haya. Wataalam wa mambo haya wako wapi? Si wako *TANESCO*!! Sasa inakuwaje? Nafikiri *TANESCO* haijalitizama vizuri suala hili.

Inatakiwa Shirika la *TANESCO* liweze kujidhibiti wenyewe. Sina ushahidi wa kuwafikiria baadhi ya wafanyakazi au mafundi wanafanyakazi hiyo, lakini mtu wa kawaida nina uhakika kabisa hawezi kupanda kule juu akatoa mafuta ya *transformer. It impossible!* Nyaya nyingine akizitazama mwananchi wa kawaida hajui kama ni *high-tension* au nini kwa hiyo hawezi kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo ili tuweze kulinda *installations* muhimu kama hizi ni vyema tatizo hili la kuibiwa nyaya za umeme na mafuta ya *transformer* na vifaa vingine likomeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu sana Kitaifa na kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Kabla sijaendele pia naomba niungane na wenzangu katika kutoa rambirambi kwa familia ya Hayati Balozi Diria, pamoja na familia ya Hayati Balozi Bomani ambao wametutoka na Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una madhumuni yafuatayo, na ni vema tukajikumbusha hayo wakati tunatoa mchango wetu. Madhumuni makubwa ya Muswada huu na Sheria hii ni kuendeleza nishati ya kisasa na kuhakikisha ukuaji wa huduma ya nishati Vijijini na jawabu lake ni kujenga uchumi. Hayo ndio madhumuni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitazungumzia katika maeneo hayo tu na nikianzia na hili moja la ukuaji wa huduma za nishati Vijijini, hali halisi iko vipi hadi hivi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni kwamba ile *Grid* ya Taifa ambayo ndio tunayoitegemea kusambaza umeme katika maeneo mengi Vijijini ni ndogo na haitoshelezi mahitaji. Hilo ndio tatizo moja kubwa sana. Kwa hiyo lazima kama tuna nia yoyote ile ya kutaka kufikisha umeme Vijijini lazima tukuze *Grid* hii ya Taifa tuiongezee uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, kutokana na madhumuni hayo ni kwamba sehemu kubwa ambayo inalengwa na Sheria yenyewe ni Vijijini. Kwa hakika Vijiji vingi sana Tanzania havina umeme. Kwa hiyo tuna uhakika tuna tatizo kubwa, *Grid* haitoshi na vile vile Vijiji vingi havina umeme. Sasa tunatengeneza Sheria hii yenye dhamira ya kwenda huko, tunakwenda kwa utaratibu gani wakati tunajua kabisa kwamba *Grid* haitoshi na vile vile Vijiji vingi havina umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, jawabu la kwanza ni kuanza kuhakikisha kwamba tunatunisha Bajeti yetu ya Wizara hii ya Nishati na Madini. Bila hilo tutakuwa tunazungumza lugha tu. Kwa hiyo la kwanza ni kuangalia *seriousness* yetu katika suala hili; tutaiona mwaka huu katika Bajeti hii ya mwaka 2005/2006 kwamba itaonyesha kwa uhakika kuna kukua na kuongezeka kwa Bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini au la.

Kama haitakuwa imeongezeka, basi tunazungumza tu mambo ambayo hatutayatekeleza katika kipindi cha mwaka 2005/2006, labda Mwenyezi Mungu akitujalia ni huko usoni na sio sasa. Sasa lazima tuwe *serious* katika hili kwa sababu tunaona tuna mapungufu makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kubwa ambalo linatukabili kwa huu, umeme tunaouita umeme wa kisasa ambao wengi wanaita umeme wa *TANESCO* ni gharama zake ni kubwa sana. Umeme huu ni ghali kiasi kwamba kuna mashaka kama kweli huko tunakolenga sijui kama kweli wananchi wetu watamudu kuupata. Kwa wastani gharama za kufanya *wiring* tu nyumba ya vyumba vinne sio chini ya Sh. 300,000/= na sasa tumesikia hapa kwamba hata kupata *service line* kuvutiwa ni Sh.200,000/=. Kwa hiyo yeye mwenyewe mwanakijiji ili aweze kujiandaa ni lazima awe na hela si chini ya Sh.500,000/= na hayo ni maandalizi ya awali.

Lakini vile vile, lazima ajiandae mwanakijiji huyu kwamba atakuwa analipia matumizi ya umeme ya kila siku na kufuatana na *tariff rates* ambazo kwa bahati nzuri ninazo hapa. Kwa wastani wa matumizi *unit* zaidi ya 51 mwanakijiji huyu atapaswa kulipa Sh.115/= kwa kila *unit*. Tukisema kwa wastani watatumia *units* 60 peke yake kwa mwezi, basi huyu atatakiwa pale Kijijini alipe si chini ya Sh.6,900/=. Hizi ni kwa *unit* peke yake. Lakini bado tunazo kodi nyingine zinazowekwa juu ya kiwango hiki cha Sh.6,900/=. Kwanza ni *VAT*.

Sasa huyu mwanakijiji kule Kitongojini kwanza hata uwezo wake wa kipato ha-*qualify* yeye hata kulipa Kodi ya Mapato. Lakini leo anaambiwa alipe *VAT*! Kwa uwezo wake na kwa biashara yake ndogo anayofanya pale Kijijini ha-*qualify* hata kulipa ile ada ya leseni za biashara, leo anaambiwa alipe *VAT*. Sasa tunamwongezea mzigo mkubwa kwamba hiki kiwango anachopaswa kulipa kwa kweli kinazidi kuongezeka.

Lakini vile vile, katika Mfuko huu tumesema lazima tuwe na kiwango tutakacho-*charge* juu ya viwango hivi vya matumizi ili kutunisha Mfuko wetu. Tumesema tuanzie na wastani wa *percent* tatu. Lakini nilikuwa napendekeza kwamba, hebu tuiweke pembeni *VAT* kwanza ili tuweze ku-*deal* na hili suala la kutunisha huu Mfuko kwa kiwango hiki cha angalau asilimia tatu au mpaka asilimia tano ili kweli tuweze kuanza kuutunisha Mfuko wetu. Tukitaka yote mawili, tunataka *VAT* na tunaka kutunisha Mfuko kwa uhakika hatutaweza, tushike moja na hili la kutunisha Mfuko kwa kiwango cha wastani wa asilimia tatu mpaka asilimia tano, lakini tuache pembeni *VAT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii ya gharama za umeme Vijijini, tunasema tunataka kuwa na umeme wa kisasa. Ni aina gani ya umeme wa kisasa mwingine ambao hata mpaka sasa hivi teknolojia zetu zinaruhusu? Moja, ni umeme huo wa *solar,* lakini vile vile tunaweza tukatumia *biogas* na vile vile tunaweza tukapata umeme kutokana na katani. Sasa hayo ndio baadhi tu ya maeneo ambayo pia tunaweza tukapata umeme. Lakini hebu tujaribu kuangalia gharama za umeme wa *solar* nazo zinasemaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uweze kuwa na *solar* katika Kijiji chako, moja ya kazi ya kwanza kabisa lazima ufanye *wiring* na *wiring* hii inafanana kabisa na *wiring* ile

ya umeme wa *TANESCO*. Kwa hiyo lazima uwe na kama Sh.300,000/=. Lakini betri moja tu ya *solar* sasa hivi madukani ni Sh.150,000/= mpaka Sh.200,000/=. Vile vile, *tubelight* moja tu ya *solar* sio chini ya Sh.25,000/=. Sasa ukizikusanya gharama zote hizi ili uweze kuweka *solar* katika nyumba yako ya vyumba vinne pale Kijijini, lazima uwe na wastani wa Sh.1,150,000/=. Hizi ni gharama kubwa sana tukidhani kwamba wanakijiji wanaweza kuzimudu. Sasa lazima twende Vijijini kwa nguvu moja ya ku-*develop Grid* ya Taifa.

Lakini vile vile, twende na mpango huu wa *solar* na kwa sababu ndani ya Mfuko huu kuna *provisions* kwamba Mfuko huo utatunishwa kwa michango mbalimbali, tunategemea vile vile tutaweza kupata Wahisani watakaosaidia katika kuendeleza umeme Vijijini Tanzania na inawezekana wakatoa mikopo na inawezekana vile vile zikatolewa *grants*. Sasa nasema wakati tunajiandaa kukuza ile *Grid* ya Taifa, hebu tuanze kwenda na utaratibu wa *solar* kwa kutumia Mfuko huo.

Mimi nilikuwa napendekeza kwamba kule katika Wilaya yetu ya Mheza tumejenga Zahanati mpya 16 katika kipindi hiki cha miaka minne. Lakini Zahanati hizi ziko katika maeneo mengi ya Vijijini ambapo kwa kweli *Grid* ya Taifa haitaweza kufika leo wala kesho, itachukua muda mrefu. Sasa hivi Zahanati zinahitaji kutoa huduma za kisasa. Hebu tuanze basi kwa kuzipelekea umeme aina ya *solar* kwa majaribio. Kwa sababu *solar* ina uwezo wa kufanya friji ikafanya kazi na hivyo hifadhi ya dawa ikawa inawezekana katika Vijiji vyetu. Vijiji hivyo ambavyo Zahanati hizo zipo na ambazo nazipendekeza kwenu sasa tukafanye majaribio ya matumizi hayo ya *solar* ni Zahanati ya Kigongo Mawe, Zahanati ya Kambai, Zahanati ya Mashewa, Zahanati ya Zirai, Zahanati ya Kisiwani na Zahanati ya Kiwanda. Tuzifanyie majaribio hizo kwa mfumo huo wa *solar* halafu watu wengine waige kutoka katika majaribio hayo mtakayoyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu kuliangalia ni kwamba tutadhibiti vipi kupanda kwa gharama za umeme? Wakati tulipokuwa tuna-*develop* gesi ya Songosongo matarajio yetu sote sisi kutokana na kauli za Serikali ni kwamba wakati gesi ingeanza kutumika bei za umeme zingeweza kushuka. Lakini kwa bahati mbaya hili halikutokea badala ya bei za umeme kushuka, bei za umeme zimeanza kupanda. Sasa mimi nasema hatutaweza kudhibiti matumizi hayo ya gesi yakatusaidia katika kupunguza gharama za uzalishaji wa umeme bila sisi wenyewe kushiriki katika kusimamia mfumo mzima wa uzalishaji wa gesi ile ya Songo Songo.

Baada *TPDC* kufanya kazi nzuri sana kwa miaka yote na kuilinda na kuigharamia gesi ile kwa miaka zaidi ya 20 kwa gharama kubwa, sasa mradi ule umeanza na umekabidhiwa watu wa *Songas*. Wao sasa ndio wanachimba gesi ile, wao ndio wanaosafirisha gesi ile, wao ndio wanauza gesi ile peke yao na hakuna mtu anayedhibiti pale katikakati. *TPDC* sasa hivi wako nje kabisa na mimi nasema nina mashaka makubwa kama kweli *TPDC* wataweza kupata fedha ambazo kimkataba wangepaswa kuzipata kutokana na mauzo ya gesi. Kwa sababu sasa hawapo kabisa katika usimamizi wa mauzo ya gesi, hawauzi gesi, *Songas* ndio wanauza gesi. Pesa zao zile watazipata wapi? Hivi kweli si itakuwa malumbano tu kati ya *Songas, TRA* na Hazina ili kuiwezesha *TPDC* kupata fedha zake ambazo kimsingi wangepaswa kuzipata kutokana na mauzo ya gesi!

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndio machache niliyokuwa nataka kuchangia kwa siku ya leo na nilifanya sehemu kubwa ya kazi yangu kama Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Muswada huu wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niungane na wenzangu kuwapa pole familia ya Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria ambaye alikuwa Mbunge wa Raha Leo na familia ya Marehemu Balozi Paul Boman. Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kama ukiusoma haraka haraka hivi, unasema naam! Kwa kweli umekuja kwa wakati na unatufaa. Kwa sababu katika ukurasa wa 47 katika kifungu (4) wanasema: *"The principles of Rural Energy Development shall be as follows:-"* (a) ambayo ndio ilinitia moyo sana: *"Modern energy electricity supply to rural areas promotes growth in economic production and productivity as well as social welfare."*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dhana nzuri sana. Pamoja na kifungu cha nne (a) kinasema hivyo, mimi ninashindwa kuunga mkono kwa sababu zifuatazo:-

Ya kwanza, katika kifungu kile (4)(c) Muswada unasema: "*The roll of the Government in rural energy service provision is that of the facilitator of activities and investment made by private and Community entities."* Kwa hiyo Serikali ni *facilitator* tu, hausiki. Lakini hii inasema, pale sehemu ya mwisho *"And shall rely on the technical and financial capacity of qualified private sector entities."* Sasa najiuliza, huko Kijijini huyu *qualified technical and financial entity* anatoka wapi? *(Makofi)*

Sasa najiuliza, kama Makao Makuu ya Mkoa wa Lindi hawana umeme wa uhakika mpaka leo, Kijiji kama Nangaru, Kijiji kama Nanjilinji, Mandawa watapataje umeme? Bahati mbaya hawaitwi Nyumba ya Mungu, wala Birika la Mungu, labda ungekuwa na majina wangekaribiwa na umeme. *Private entity* hii yenye uwezo itatoka wapi?

Hivi sasa hata mwekezaji wa uhakika aliyesogea Mkoa wa Lindi hakuna. Leo Serikali inasema, yeye atakuwa *facilitator.* Kwa nani? Au tunataka kugawa nchi kwamba eneo fulani kwa sababu wapo ambao wako *technically and financially advanced* wataendelea, kwingine ambako *technical know how* na *financially incapable,* basi tunabaki tunaduwaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo *point* yangu ya kwanza naogopa kuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu yangu ya pili ni kwamba miundombinu ya umeme inayotakiwa yaani nguzo, nyaya, *transformer* ni ghali mno. Hivi huyu *private sector* tunayemwambia aende Kijijini hata kama Mfuko utatoa ruzuku, tutaweza kusambaza katika Vijijini vingapi? Kwa ruzuku ya kutoka Mfuko huu wa umeme Vijijini au Serikali inataka kutuhakikishia kwamba ina mabilioni iliyotenga? Kama yapo mabilioni iliyotenga badala ya kusubiri watoe ruzuku na msaada, kwa nini wasiwe wazi, Watendaji na kuhakikisha umeme unafika maeneo ambayo hatuna umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu yangu ya tatu ni kwamba tumezungumzia umeme, tumezungumzia *Songo gas* hapa. Songosongo ni kisiwa katika Wilaya ya Kilwa Mkoa wa Lindi. Gesi ile imetolewa Songosongo imekwenda kuzalisha umeme Dar es Salaam. Mkoa wa Lindi, katika Makao Makuu ya Mkoa, miaka 43 ya uhuru hatuna umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge nilikuwa nyumbani, mimi nakaa Kijijini. Mungu kanijalia nina kijenereta changu ninakiwasha toka saa moja mpaka saa nne angalau nisikilize habari. Lakini ndugu zangu pale Lindi Mjini hawakuwa na umeme mchana na usiku. Watu wana biashara za *stationery,* lakini hawana umeme wa uhakika. Lakini *Songo gas* wame-*pump gas* toka Songosongo mpaka Dar es Salaam, eti kuongeza umeme Dar es Salaam.

Niliwauliza siku moja kwamba, mlimsikia nani anachukua ndizi Dar es Salaam anazipeleka Tukuyu? Au anabeba ndizi anazipeleka Bukoba? Wanavyo kule! Au ni usemi ule wa Biblia kwamba walio navyo wataongezewa na wale ambao hawana watanyang'anywa kile walicho nacho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Wilaya ya Kilwa yenyewe Mji wa Kilwa Masoko na Kilwa Kivinje hawana umeme wa uhakika. Sasa unajiuliza, kweli huyu gesi anayo, lakini unaambiwa eti tusubiri mradi wa Mnazibay. *Mnazibay* hawajaanza kuchimba gesi mpaka leo, labda Serikali inihakikishie kuwa wameanza kuchimba leo. Ni sawasawa na kumwambia mtoto kwamba chakula hiki kimeiva lakini ngoja, wewe una njaa lakini huyu hajashiba sana ngoja tumpe huyu ambaye hajashiba sana ili ashibe vizuri halafu wewe cha kwako tunakipika. Mpaka ukatafute kuni tena porini, uje uweke mafiga, uchochee na maji yachemke. Kitaiva lini? Hiyo ni sababu yangu ya tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya nne, umeme Mijini hivi sasa ni ghali. Huu umeme tunaotaka kupeleka Vijijini, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba mwananchi yule tunayempelekea umeme Kijijini ataweza kumudu gharama? Mpango gani watauweka wa kuhakikisha kumdhibiti huyu mtu binafsi, maana mtu binafsi ni mfanyabiashara na kama ni mfanyabiashara lengo lake kubwa ni kuhakikisha anarudisha hela yake haraka na anapata faida. Serikali inatuhakikishiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi wamesema. Miti inateketea hapa nchini, misitu inakatwa usiku na mchana kwa sababu ya kuni na mkaa na tusipoangalia tutakuwa jangwa kwa sababu nishati yetu ni ghali mno. Ninachotaka kujua ni kwamba, tuna utaratibu gani wa kuhakikisha hawa Vijijini gharama yao inakuwa nafuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu yangu ya tano, Tanzania siyo kisiwa na sisi tuko katika karne ya 21. Sera yetu nzuri ya CCM inatuambia tuhakikishe tunaongeza wanafunzi wa Shule za Sekondari kwa kuanzisha *Day Secondary Schools.* Lakini wengine wanamaliza Sekondari kule Vijijini hawajaona umeme. Wanasoma *theory in physics but they have never seen electricity.* Hawajui hata *computer* inawashwaje! Wanapokuja Mjini wanashangaa ile balbu inavyowaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kweli. Samahani nitoe mfano tu. Binti yangu anachukua *masters* kule Chuo Kikuu, alikuwa na wenzake, mniwie radhi, lakini mwenzake mmoja alikwenda chooni alikuwa anaangalia choo anageuka anarudi maana hajawahi kuona choo *European type.* Alikuwa anaogopa, hapa atakaaje? Huyu ni mtu amefaulu Kijijini anakwenda Chuo Kikuu. Imemchukua muda kujua namna ya kutumia choo kile. Wewe fikiria mambo haya, *rural education* tuko kwenye karne ya 21 Shule ziko kule, lakini tumepanga mipango gani ya kuhakikisha tumepeleka Shule kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri ufuatao:- Kama Serikali inaunda Mfuko huu na iko tayari kutoa ruzuku, basi waweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha wanafikia kwanza maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo.

Ushauri wangu wa pili, tutumie nishati mbadala ili tuweze kutumia nishati mbadala badala ya kuwaachia tu watu binafsi waende kiholela. Tuangalie maeneo yafuatayo:-

Kwanza *biogas*. Kwa mfano Mkoa wangu wa Lindi hatuna *biogas,* hatuna ng'ombe wa kutosha, lakini ma-*sister* Narunyu pale wana *biogas* kwa sababu wana ng'ombe. Kwa hiyo, ili mpango huu uweze kwenda vizuri, tuwe na wataalamu wanaokwenda kusaidia Vijijini na washirikiane kwa sababu hii ni Serikali moja, basi wahakikishe wanatupelekea ng'ombe kwenye maeneo ambayo hatuna ng'ombe, *unless* wanatuambia kwamba *biogas* inaweza kutokana hata na kinyesi cha mbuzi.

Pili, tupunguze kodi kwenye vifaa vya umeme ili tuhakikishe wananchi wanapata umeme huu. Tupunguze kodi kwenye vifaa vya umeme maana umeme uko wa aina nyingi kama *biogas, solar* kama aliyozungumzia ndugu yangu aliyemaliza kuzungumza, yapo matumizi na *battery* ambayo ni bei nafuu lakini tunahitaji kupunguziwa gharama. Vifaa hivi vikipungua kodi wananchi wanaweza kumudu kama kuna msaada au mkopo kwenye Mfuko huu, basi wanaweza kukopa kwa bei nafuu.

Ushauri wangu wa tatu sasa, machimbo ya mawe ya Mchuchuma sasa yafanyiwe kazi kwa uhakika ili tupate nishati ya makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kuwa Muswada huu kama nilivyosema lengo lake ni zuri sana. Niko tayari kuunga mkono kama nitahakikishwa kwamba *Songo Gas* pale kwenye *T - Somanga,* Serikali itahakikisha inapeleka umeme Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Nangulukuru, Somanga na Vijiji vyote

ambako gesi ile inapita kuelekea Dar es Salaam, maana gesi ile imetoka kule, basi angalau Wilaya ya ambako gesi inatoka, basi umeme upatikane.

Pili, kama Mji wa Lindi, Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya zake zihakikishiwe zinapata umeme wa uhakika, maana majenereta yaliyoko Lindi sijui yamekufa, ya mwaka gani!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika sehemu mbili tu za Muswada. Lakini kabla sijafanya hivyo na pengine labda sijampongeza Mheshimiwa Waziri, nakumbuka alikuwa na swali langu ambalo linahusu mambo ya umeme ikiwa ni pamoja na madini. Sasa kama kawaida, nadhani alitarajia ningeweza kumwuliza swali la nyongeza moja au mawili lakini sikuyauliza kwa sababu majibu niliyoyapata kwa kweli ilikuwa ni kama unauliza: "Mbuzi wangu umewaona?" Halafu mtu anasema: "Kondoo wale walikuwa wana manyoya." Kwa hiyo huwezi kumwuliza swali lingine. *(Kicheko)*

Sasa pengine hiyo inatuonyesha kwamba tunavyofahamu mahitaji na matatizo ya Watanzania katika maeneo mbalimbali ya nchi hii kubwa katika Afrika Mashariki, pengine inatofautiana kufuatana na mahali tunapokaa. Sitaki kuendelea huko kwa sababu haiko kwenye Muswada, ila niseme tu kidogo kwamba alipokuwa anasema zile *Kilovolts*, ule umeme unaotoka Uganda tu, kwa mfano haujatumika kikamilifu katika Mkoa wa Kagera, sasa nilikuwa nashangaa kwa majibu yale na pengine si kana kwamba utapeleka umeme tu Kyerwa kwa sababu unataka kuchimba *tin* ambayo nayo ilitafsiriwa vingine. Sidhani kama hiyo ndiyo sahihi kwa sababu kuna maeneo mengine katika Wilaya nyingine hazitakuwa na machimbo ya aina yoyote, lakini zina watu wanahitaji umeme katika vitu vingine.

Kwa hiyo ndiyo nilikuwa najaribu kuangalia kwamba kama tutapeleka tu kwa sababu kuna madini, inakuwa si utaratibu huo. Nadhani ndicho anachokisema Mheshimiwa Watondoha kwamba nchi hii watu wote wanalipa kodi na wanahitaji umeme kwa matumizi tofauti tofauti.

Nirudi kwenye Muswada wenyewe. Nilikuwa naangalia sehemu ya kwanza katika suala la *interpretation*, wamejaribu ku-*define* na ku-*interpret* mambo ambayo yatakuwa kwenye Muswada, lakini sikuona kitu kama *energy, rural.* Wamezungumza, sasa ni *area outside the urban area,* lakini hawajazungumza *energy* inayozungumzwa hapa ni ipi kwa sababu hatuwezi kuzungumzia ile ya *calories*. Vyanzo vya nishati ni vipi ambavyo tunakusudia pengine kuvitumia katika sheria hii ili yule anayetaka kutengeneza sasa umeme ule ajue kihalisia anapaswa kuwajibika na nini. Kutakuwa na *atomic energy, wind energy, solar energy, bio, fuel, hydro, thermal* na kadhalika. Sasa huku kwenye definition hawakuweka hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, itatupa tatizo kidogo na pengine labda kabla Bunge hili halijaahirishwa, ninaweza kuona kwamba pengine nitakuwa na nafasi hapa ya kuzungumza kuhusu baadhi ya nishati ambayo inaweza kuwa rahisi *especially* ambayo tunaweza kutumia *uranium* ambayo ninaamini hata hapa tulipokaa chini kwa Mkoa wa Dodoma huku chini, kuna *uranium.* Sasa baadaye nadhani tutaeleza ni kipi kilicho rahisi katika gharama uendelevu kutumia kuzalisha nishati ambayo unaweza ukazalisha na ikakusaidia kuwa rahisi ili uweze kusaidia katika biashara zinazofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kwenye Muswada tena sehemu ya tano ambako anazungumza: *"The Establishment of the Rural Energy Fund,* sasa nikijaribu kusoma na kuiangalia haya yote sioni kitu ambacho wanaji-*commit* mahali fulani kwa sababu anasema katika *section* 18(2): *"The fund shall provide resources for grants towards the capital costs of project implemented by private and public entities, co-operatives and Local Community Organisations."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inakuwa vigumu kwa mtu kutabiri na kubashiri kiusahihi ni miradi mingapi inaweza kuanzishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ngazi za Vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa ili aweze kujua atapaswa kuwa na hela kiasi gani na kwa mujibu wa sheria hii ili aweze kuwatimizia wale wote wanaoomba. Kwa hiyo, kama watu watakuja wanaomba tofauti tofauti, sasa suala hapa litakuja kwenye *resources* zile ambazo wanazisema zitatoka wapi.

Kipengele cha (b): *"The provision of technical assistance, training and other forms of capacity building qualified developers by qualified experts related to the planning and preparation of a project prior to an application for a grant."* Sasa haya yote ukiyasoma na (c): *"The provision of financial assistance"*, hiyo *section* 18 na vipengele vyake vile vingine, sijui tunacholenga ni nini? Tunalenga tutaje hivi ili tuwafurahishe watu au tunalenga kusema kwamba tunawaruhusu watu waje wawekeze katika nishati ya umeme kwa ajili ya Vijiji kwa madhumuni ya kwamba watapata faida na kwa hiyo wataendeleza miradi ile, au tunawaambia kwamba unaweza kuja tutakupa hela tutakusaidiasaidia, lakini itakapofika mahala kwamba ule mradi huwezi kuuendeleza na sisi tukaona kwamba hatuna returns tumtelekeze aende!

Mheshimiwa Naibu Spika, labda pengine ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* ajaribu kutuambia wanacholenga hapa ni nini? Kwa sababu katika nchi hii nimezungumza wakati wa Sheria ya Ardhi kwamba tunapokuwa tunapitisha Muswada hapa, tunakuwa very *euphoric* tunapata hamasa hivi, tunamahasika kwamba Muswada umekuja kwa wakati muhimu, umekuja sasa, tumekombolewa kabisa! Sasa ukiwauliza kwa sheria, Sheria ya Ardhi tuliyoipitisha mwaka 1999 ni nani amekwenda kukopa pale *and it is there*, huwezi kwenda kukopa kwa sababu ardhi yenyewe ilikuwa ni Kijiji cha mtu, hujaipima lakini sheria iko pale, aliyeipima mjanja aliyeko Dodoma, Dar es Salaam atapeleka pale hati na huwezi kusema uende kupima kama Mheshimiwa Waziri Cheyo hukumpa hela za kupimia. Sasa kulikuwa hakuna muunganiko pale. *There is no connections*. Sasa ndiyo maana nasema haya tuliyoyasema nadhani tunaji-*commit*.

Sasa *section 19* inasema: *"All contributions and other payments required by this Part shall be paid into the Fund, for the purpose of the fund and for making other payments required by this Act."* Watu watatakiwa kulipa, watalipa kwenye Mfuko halafu na Mfuko wenyewe utalipwa.

Namba mbili, *"The Board shall, from time to time in consultation with the Minister, fix the size of the Fund sufficient to achieve the objectives of this Act."* Sasa Bodi itamwona Waziri wakubaliane kwamba zitakuwa bilioni tano au kumi kwa nchi nzima. Sasa sijui wanakubaliana kwa *resources* zipi!

Mheshimiwa Naibu Spika, *The sources of the income for the fund shall consist of monies as may be provided by Government in an annual budgetary allocation, to be deposited in the account of the Board at the a beginning of every month or as may be determined by Minister for Finance.* Ina- *sound* kama inaweza ku-*appeal* kwenye masikio yetu lakini katika sheria ya *TANROAD*, Mfuko wa Mamlaka ya Elimu angalau tumeweka kiwango kwamba Serikali itaweka kule asilimia fulani ya bajeti ya maendeleo ya mwaka husika. Pengine wanasema labda ya *GDP*, sasa pale mnaweza kuwa mnajua kinachoweza kufanyika. Lakini hii kwamba wakikubaliana kuweka bilioni moja kueneza umeme huko Vijijini na uwakopeshe watu wapitie *consultancy* kwa nchi ya Tanzania, kwa kweli inakuwa ni vigumu na haifikiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) *"As contributions from international financial organisations, multilateral, bilateral agencies and other development partiners."* Sasa tunaweka tena ule utegemezi. Hatuna uhakika! Mimi sisemi hauwezi kutusaidia lakini hatuna uhakika wa kile tunachojaribu kukifanya. Hoja ya msingi hapa ingelikuwa ni kwamba tunajua kwamba tulivyoruhusu Makampuni ya simu *Celtel, Mobitel* na haya mambo yana utamaduni wake, kwenye simu wanafanya biashara kubwa sana kwa sababu kila mtu hata asiyepata Sh.6,000/= kwa mwezi anatumia simu kwa sababu *barmaid* akipiga simu yeye anajua anakopata hela na anapiga kweli na analipia. Lakini inapokuja Vijijini, watu wengine watumia karabai au koroboi au moto tu amekoka pale wewe unatoka hapa hujawaendeleza kiuchumi unapitisha pale umeme, hakuna kiwanda wala kitu chochote hata Benki hujapeleka iwape mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza na mtu mmoja kwamba, tukiwa hapa Bungeni tunapiga kelele kweli na alikuwa anatoka upinzani akaniambia hata sisi tukichukua madaraka ukitaka kupeleka umeme Kigoma, mtaniwia radhi watu wa Kigoma, ile misitu yote upitie uweke *line* za umeme, ukate, ufyeke haya yote mpaka ufike kule, kwa kweli gharama ni kubwa na kurudisha faida tu ni baada ya miaka 50 na ni kwa sababu ya mazingira na huwezi kukataa hili na ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo mimi kwangu waliniuliza, wewe umekaa hapo umezuia Serikali isituletee umeme kwa sababu wewe ni mpinzani. Mimi nikawaambia ukienda kwa Mheshimiwa Mkapa, Rais wa Jamhuri, kwenye Mkoa wake hakuna umeme wa *Grid* sasa hamwezi kuniambia hivyo mimi. *(Kicheko)*

Ukienda kwa Mheshimwa Yona, kwenye Tarafa yake ambaye anahusika na umeme, hakuna umeme wa *Grid,* sasa ninyi hamwezi kuniambia hivyo. Kwa hiyo umeme haugaiwi kama tunagawa maembe. Kwa hiyo watu wanaopata umeme ni milioni moja katika milioni 35 za Watanzania na kuna sababu ambazo huwezi kuzikataa. Siyo suala la ku-*fight* unataka kumpiga mtu ngumi, lakini lazima tujue kwamba umeme unapoupeleka mahali sasa kama tunasema *TANESCO* tunawapa *subsidy* kwa nini tunawapa *subsidy*? Kwa nini tunawapa ruzuku *TANESCO*? Ziko sababu za kitaalam. Watakwambia hela walizozitumia umeme umepotea watu wengine hawataki hata ku-*switch,* wameondoka tu kwenye *show* hawataki kuzima kwenye ukuta, hataki kuzima anajiendea tu. *(Kicheko)*

Sasa katika mila na utamaduni wa namna hii katika nchi hii, mwingine utamfungia umeme leo kesho anaukata kwa sababu ya matatizo moja, mbili, tatu, nne, tano. Kwa hiyo hata hawa ambao tunadhani watakuja kama binafsi waanzishe vituo vya kuzalisha umeme, kama matatizo haya hatuwezi kuyachunguza na kwa kweli tukayatafutia ufumbuzi, muafaka na njia mjarabati tutarudi kulekule tunapiga *marktime* na kwa sababu mmesema kwenye sheria tutakuwa tunakupa *subsidy*, tutakuja tutakupa *subsidy,* kila mmoja analipwa *subsidy,* msipompa anang'aka anaondoka. Lakini lazima hoja ya kwamba kuwepo na umeme katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni la msingi alichokuwa anasema Mheshimiwa Watondoha.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani katika nchi hii wanafunzi wanaokuja Dar es Salaam wawe wanapiga *computer* yule anayetoka Mabila kwangu pale hakuna simu za *TTCL* walishamdhulumu umeme haupo, jenereta haipo, yeye *computer* haioni mpaka aikute Chuo Kikuu. Sasa hivi hii elimu tunayoitoa, kweli ni haki na yeye akishindwa mnamwambia umeshindwa toka, kwa sababu *facilities* hazikuwepo. Sasa inakuwa kwa kweli siyo haki na siyo ustaarabu.

Sasa ninapendekeza kwamba haya tumeyaona, tuna sera na tumetunga sheria, lakini lazima twende tukafanye utafiti na uchambuzi wa kina wa kujua kwamba sera hii pamoja na sheria hii vinatekelezeka namna gani na pengine tuweze kujua *feasibility study* kwamba katika nchi hii wewe kama unataka kuwekeza, ukienda Kagera uki-*apply wind energy,* ile mitambo nilikuwa naona wale Wachina wanarusha, unatumia hiyo. Kama unakwenda Kusini kwa Mheshimiwa Watondoha, pale tutawapa ule wa gesi, kama ukija kwa Mheshimiwa Mntangi kwa sababu kuna katani nyingi tena na ardhi tunawapa mlime katani nyingi ninyi mzalishe umeme huu, itakuwa inaweza kufaa na ndiyo tuweze kuwasaidia. Lakini hii kuweka mambo ya ujumlajumla halafu tunakaa tunacheka kwamba sasa kwa sababu tumetunga sheria tutakuwa na umeme nchi nzima, haiwezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo nadhani ujumbe umefika sasa sijui tunafanyaje lakini ndiyo sheria imekwisha kuletwa hapa nadhani ilibidi ichambuliwe zaidi ili iweze kukuzwa sana sasa ngoja niwaachie wengine waseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Sana. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza kabisa niwashukuru Wabunge wenzangu kwa kunifariji na kunipokea kwa makofi jana, kwa kweli nimefarijika na tunaendelea na mambo yetu ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya pili niseme tu tofauti na Wabunge wengi niliowasikia wanachangia hapa katika Jimbo langu la Moshi Vijijini asilimia 90 kuna umeme. Tatizo kubwa ambalo nataka nili-*address* hapa ni kwamba maeneo mengine ambayo yamewekwa umeme kama Chekereni, Sehemu za Mvuleni, sehemu chache mbalimbali hazina *transformer* ambazo ni za kuweka sasa ili umeme uwe majumbani kwa watu. Hilo ni kama asilimia 20.

Kwa hiyo kwa kuwa tuna mtambo wa kutengeneza *transformer* Arusha na labda Serikali imeona kwamba iweke umeme kwenye Jimbo langu ili kuonyesha maendeleo zaidi pale, basi niombe kwa kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali basi ituletee hizo *transformers* ili wale watumiaji waweze kutumia huo umeme ambao na nyaya zimepita pale juu wanaziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umeme huo, lazima nii-*argue* Serikali kuhusu bei za umeme. Kabla sijafika kwenye bei ya umeme, niseme kwanza kuhusu Wakala. Tunasema hapa tunaweka Wakala kwa ajili ya umeme wa *rural energy* halafu tuna kitu kinaitwa *Netgroup Solution* na tulivyokuwa tunaongea hapa mwaka jana tuliambiwa kwamba *Netgroup Solution* baadaye watafika mpaka Vijijini. Leo tunaunda wataalam wengine wa kupeleka umeme Vijijini! Samahani mimi ni Mbunge wa Moshi Vijijini, kwa hiyo kila wakati nakumbuka huko. Mimi naona inakuwa ni mzigo kwa sababu hawa watu nimesoma hapa, *Financial Provisions* hawa watatumia fedha na hizo hela zitakuwa ni mzigo kwa watumiaji umeme. Hii *Netgroup* nayo inatumia fedha, mishahara yao ni mikubwa itakuwa ni mzigo kwa watumiaji umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika,hali ya umeme Tanzania ni ghali kuliko sehemu nyingine ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika, lakini *sources* za kupata umeme ziko nyingi zaidi Tanzania kuliko sehemu nyingine. Sasa nilikuwa nafikiri kwamba tulivyoambiwa kwamba gesi ya Songosongo imetokea, nikafikiri kwamba sasa umeme utakuwa nusu bei kwa sababu tayari tumepata gesi tumeshangilia, tumefanya na maandamano, Rais amekwenda kufungua tumepata gesi sasa, umeme utakuwa nusu bei. Lakini badala yake gharama za umeme zimepanda juu, umekuwa bei juu zaidi.

Sasa kama tunaamini kwamba kwa kupeleka umeme Vijijini ni kupeleka maendeleo, basi lazima tujue vilevile hali ya umeme huo na namna ya bei ya umeme, tupunguze hizo gharama za umeme, tukishapunguza gharama za umeme sasa wananchi watatumia na tunaweza tukafanya kazi nyingi ambazo zingeweza zikaleta maendeleo na uchumi wa nchi ukakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka juzi tuliletewa barua hapa kutoka Amerika na Bwana Mrema, kwamba kuna umeme wa bei poa wa Vijijini na mimi nilitumwa.

Naomba tusicheke. Nilitumwa kwenda kwa Waziri, nilikwenda Ofisini kwa Waziri na hiyo barua na jinsi maandiko yake yalivyokuwa na Waziri alipokea. Sasa kwa kuwa Serikali ilikuwa *associated,* tunataka itujibu imefikia wapi mpaka sasa hivi kuhusu huo umeme poa wa Vijijini? *(Kicheko/ Makofi)*

Katika ku-*wind up,* nitaomba Waziri kwa sababu nilimwona binafsi na nikamkabidhi *documents* zenyewe na akapokea na Serikali ikasema itafanyia kazi, hivyo tungehitaji majibu hayo hapa Bungeni ili tujue huo umeme poa bado upo au haupo na ilikuwaje? Maana tulitumia gharama yetu muda mrefu kuchambua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sawa wanasema mimi ndiye ninayejua , lakini mimi nilifika Serikalini nikakabidhi na Serikali ilipokea. Kwa hiyo sasa Serikali ndiyo baba anajua kila kitu cha nchi hii. Kwa hiyo ndiyo watakaosema imefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme Vijijini ni muhimu sana na mimi nimekwishaeleza kwamba Moshi Vijijini katika Jimbo langu kuna umeme, lakini bado sehemu chache za mashule ndio hazijapata umeme kwa sababu ya hizo *transformers*. Naomba Waziri asisahau kuliweka hilo kwamba, hizo *transformers* tunazihitaji na kwa niaba ya Jimbo la Moshi Vijijini lazima niishukuru Serikali kwa jinsi walivyoweka umeme kwa nguvu. Ni ukweli kabisa hata mtu akitembelea kule utaona eneo lote la *Lower* Moshi *Irrigation* kwenye mashamba ya *TPC* na kadhalika ukienda Kibosho au Uru utakuta umeme upo kila mahali. Naomba hicho kilichobakia kitekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba suala la bei kwa ujumla. Suala la bei ya umeme niliwahi kuzungumza hapa katika nyakati zilizopita, nikasema umeme ni nguvu na ndio maana wanasema hapa *energy,* sio kama taa hii ya kumulikia, ni nguvu na ni kitendea kazi. Kama ni kitendea kazi, basi Serikali hii ni kwa nini isifikirie kwamba wawekezaji wengi wanakimbia? Mimi niliuliza katika sehemu wanazoendesha *irrigation* wakasema tunapata gharama kubwa kwa sababu ya kutumia umeme kwenye kufanya *irrigation*. Kwa hiyo ndio maana nasema ieleweke kwamba huo umeme sio unamulikia watu majumbani tu, bali unafanya kazi kubwa ya kuzalisha na uchumi wa nchi utakuwa kwa misingi hiyo. Kwa hiyo, kama tutafanya bei kubwa na gharama ikawa kubwa, kwani niliwahi kumweleza Waziri jinsi tulivyopoteza wawekezaji. Wawekezaji walikuja hapa na sasa hivi tunalilia zaidi wawekezaji kwenye mashamba ili tuweze kuvuna au kupata uchumi mkubwa. Lakini wengine walihamia Msumbiji kwa sababu walikuta umeme hapa ni ghali, wakasema haitalipa kama tutaweka miradi yetu hapa Tanzania.

Mheshimmiwa Naibu Spika, nataka nieleze kwa uchungu sana kwamba kama Serikali itasema tu umeme upo, tutaweka umeme, tutaweka Mawakala, tutaweka *Net Group* na hili na lile na hawafikirii kuhusu kupunguza bei ya umeme, kwa kweli itakuwa ni kazi bure. Hali ya uchumi inaeleweka, hali ya wananchi inaeleweka. Kwa hiyo suala la kupunguza bei ya umeme ili kila mwananchi aweze sasa kutumia ningeomba litiliwe mkazo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda Misri, nilikuta wana umeme wa gesi na nikakuta wana umeme wa *hydropower*. Wakaniambia kwamba *hydropower* ni ghali, kwa hiyo tunatumia wa gesi. Wanazalisha *Megawatt* 2100, wanatumia asilimia kumi na tatu tu katika nchi nzima za huo umeme wa *hydropower* mwingine wanauza nje ya nchi. Lakini wao wanatumia umeme wa gesi na unakuwa ni rahisi sana. Ni kwanini sasa Serikali isiamue tutumie umeme huu wa gesi na tuachane na hii *hydropower* kwa sababu umeme wa gesi ni rahisi?

Pia nimekwenda kule Mtwara nimekuta kuna sehemu vile vile inapatikana gesi, Songosongo inapatikana gesi. Kwa hiyo gesi ipo nyingi Tanzania. Kwa nini isitumike ili sasa umeme uwe rahisi na tuelezwe faida ni nini tunapoambiwa kwamba gesi imepatikana Songosongo, tunashangilia. Mimi mwananchi wa kawaida ninayeshangilia Waziri au Rais anapofungua Mradi wa Gesi, ninafaidika kiasi gani ili nijue kweli juhudi za Serikali kuleta hiyo gesi ya Songosongo, juhudi za Serikali kuleta umeme wa aina fulani zimeleta unafuu fulani. Tulikuwa hapa kwenye *hydropower*, sasa tumepata unafuu. Naomba Waziri wakati ana-*wind up* atueleze hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namalizia kwa kusema kwamba tusiitenge Zanzibar. Zanzibar ni kipande cha Tanganyika kilichomeguka kwa sababu ya maji ya bahari. Kwa hiyo tusikitenge ni cha kwetu. Tusikitenge katika jukumu hili la kusambaza umeme Vijijini au kwingineko. Suala hili la umeme na madini ni la Muungano. Kwa hiyo ningeomba sana tunapozungumzia suala la umeme Vijijini tuunganishe na Zanzibar. Hakuna ubishi na hilo kwamba Wazanzibar ni wenzetu na wanavijiji wenzetu. Hayo mengine ya baadaye tuachane nayo. Lakini tunapozungumza umeme wa Vijijini ni pamoja na Unguja na Pemba sio Tanzania Bara pekee, hapana. Tukisema mafuta tunachimba Unguja, basi ni yetu wote, mafuta tunayochimba Tanzania Bara ni yetu wote na huu umeme ambao unapatikana kwa mafuta hayo kwa nini usiwe wetu wote? Kwa hiyo ningeomba hii sheria i-*apply* kuanzia Tanzania Bara mpaka Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba haya niliyoyataja, basi yatiliwe mkazo na ninawashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MBAROUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Muswada wa Umeme Vijijini na Mfuko wa Umeme Vijijini. Kabla sijafanya hivyo, nami ningependa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa rambirambi kwa familia za Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na Marehemu Paul Bomani kwa misiba mikubwa hii iliyowapata na tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wa Umeme Vijijini ni Muswada muhimu sana. Ni Muswada muhimu sana kwa sababu ambazo zimeelezwa ndani ya Muswada wenyewe na sababu ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezielezea kwa ufasaha sana. Mimi ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Yona na wataalam wake pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri waliyofanya kuandaa Muswada huu pamoja na kuuleta kwa wakati muafaka. Kusema kweli kama

ambavyo imeelezwa ndani ya Muswada huu na kama ambavyo imegusiwa na Waheshimiwa Wabunge mambo mengi ya maendeleo Vijijini yatategemea sana upatikanaji wa nishati ya unafuu na nishati ya kuaminika kama hii ambayo inatarajiwa ipatikane chini ya mfumo huu tunaouandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba jitihada zetu sasa hivi za kutekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi, Dira yetu na Mpango wetu wa Kujenga Uchumi na Kupambana na Umaskini, haiwezi kufanikiwa iwapo hatutakuwa na umeme wa kuaminika, umeme tahfifu ambao utatuwezesha sisi kuibua na kuendeleza shughuli zetu mbalimbali za uvuvi, za kusindika mazao, za viwanda vidogo vidogo, shughuli mbalimbali za maendeleo kama vile Shule mbalimbali tunazozijenga, Zahanati na Vituo vya Afya tunavyovijenga na nyingine nyingi za maendeleo ya jamii ambazo zinategemea kuwepo kwa umeme ili kuweza kufanyika kwa ufanisi ili kuweza kuendeleza shughuli hizi. Dira yetu ya Maendeleo inatarajia kwamba, shughuli zetu tunaweza kuziendeleza kwa uwekezaji na kukuza tija. Sasa vyote hivi viwili uwekezaji na kukuza tija haviwezi kuja kama hatuna umeme wa kutosha na wa kuaminika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba tumefikia wakati tunaunda Taasisi hii na madhumuni yake yameelezwa vizuri pamoja na Mfuko umeelezwa vizuri. Sasa madhumuni, sababu na nia ni nzuri. Mara nyingi tumekuwa na nia na sababu hizo lakini pengine hatujapata mafanikio kutokana na kutokuwa na mfumo mzuri wa upangaji mambo na utekelezaji wake.

Napenda kuchukua nafasi hii kusema kwamba, *TANROADS* ni moja ya Taasisi ambayo imeweza kufanya kazi kwa mafanikio mazuri sana. *TANROAD* imeweza kufanya hivyo kwa sababu ya kuwa na utafiti mzuri, mipango mizuri na mfumo mzuri. *TANROADS* inafanya kazi zake sio tu kutokana na mielekeo ya Kitaifa, lakini inahusisha wananchi katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachohitajika kwa Taasisi hii ni kufanya utafiti na kufanya mipango dhabiti ya maendeleo. Moja ya kazi kubwa ambayo itafanya si kubuni tu na kwenda juu juu tu hivi au kujifanyia mipango ambayo itatekelezwa, lakini nafikiri moja ya kazi kubwa ya Taasisi hii iwe kujenga miundombinu mbalimbali katika maeneo mbalimbali ambayo kutoka hapo ndio wananchi wataweza kujisaidia kutoka hapo kwenda sehemu nyingine. Kwa hiyo naamini kwamba Taasisi hiyo sio tu kwamba itapewa fedha za kutosha kama walivyokuwa wanaeleza Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kuhusu fedha au mambo ya bei mengine, nafikiri yameelezwa vizuri sana, lakini pia itapewa miongozo na taratibu na watendaji bora ambao watawezesha kufanya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara ambayo imezungumzia masuala haya, tumeyazungumza kwa undani sana. Baadhi ya masuala ambayo tulifikiri ni vizuri tuyawekee mkazo maalum, kule ndani kulikuwa kumewekwa pendekezo kwamba Mkurugenzi Mkuu apatikane kwa utaratibu wa *International Tender System.* Tuliona kwamba utaratibu huu pengine unaweza ukanyima nafasi wananchi wetu na sisi hawa wataalam wa kigeni tumeshapata uzoefu

nao. Sisemi ni wabaya, lakini mara nyingi huwa hawana uzalendo, hawana moyo kama ule ambao wanao wananchi. Tunao wataalam wa kutosha ambao wanaweza kufanya kazi hii. Sasa sisi tulifikiri kwamba wapo wananchi ambao wana utaalam wa kutosha, tuwatafute kwa utaratibu wa *competitive basis,* lakini utaratibu huo usizingatie tu kung'ang'ania au kusema kwamba hao wa nje ndio muhimu zaidi. Najua wenzetu wa nje tunashirikiana nao, watafurahi zaidi tukiweka mkazo huo, lakini nashukuru kwamba Wizara imeliona hilo na kujaribu kuona kwamba tuweke *competitive basis* sio *International Tender System.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tulikuwa tunapendekeza mle ndani kwamba, ni vizuri Mwenyekiti wa Bodi akachaguliwa na Waziri kwa sababu ikiwa tunafanya utaratibu kwamba Mwenyekiti wa Bodi achaguliwe na Bodi yenyewe, kwanza sijui hiyo Bodi ya kwanza inaweza kuitwa namna gani. Pili, sijui hiyo Bodi *accountability* yake itakuwa kwa nani, kwake yenyewe, kwa Waziri au kwa nani? Sasa tuliona kwamba, hili ni suala ambalo pengine ni vizuri likatazamwa na Waziri akawa na mamlaka hiyo na hata wale katika Bodi watakuwa wanatoa heshima maalum kwa Mwenyekiti wao ambaye atakuwa *accountable* kwa Waziri. Sasa hilo pendekezo kwamba apendekezwe na Kamati halafu apewe Waziri itakuwa kidogo labda si sahihi sana. Lakini sasa hivi linatazamwa, tutaona limefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kusema kwamba, baadhi ya maelezo au baadhi ya fikra ambazo baadhi yetu sisi Waheshimiwa Wabunge tunazo, si sahihi. Mara nyingi tunafikiri kwamba Mikoa ya Kaskazini hasa Kilimanjaro, Arusha, Tanga ni Mikoa ambayo imeendelea sana kila mahali na tunapozungumzia miradi ya maendeleo na mipango ya maendeleo kama hii, wengi wanahisi au wanafikiri basi kule maendeleo yameshafikia kiwango cha kugota na hakuhitaji tena kufikiriwa katika maendeleo haya.

Mimi ningependa kurudia kwamba, suala hili si sahihi kwa sababu Mikoa hii ni mikubwa na katika Mikoa ile mikubwa kuna maeneo ambayo kusema kweli hayana maendeleo kama vile ambavyo inafikiriwa yapo katika Mikoa hiyo. Maendeleo yanayozungumzwa ni maendeleo ya wastani, maendeleo yanayozungumzwa ni ya sekta kwa sekta. Sasa kwa mfano, kwetu Tanga, Mkoa ni mkubwa, Wilaya yetu kwa mfano ya Tanga yenyewe ni kubwa, Muheza nayo ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Mkinga ni moja ya Majimbo ambayo yapo pembezoni. Lina nafasi nzuri sana ya maendeleo, lina nafasi nzuri ya kuendeleza uvuvi, mazao ya chumvi, madini, kusindika matunda mbalimbali na mazao mengine ya chakula. Hivi sasa tumepata watu wengi sana ambao wana hamu ya kufanya uwekezaji. Lakini hawa wawekezaji wamekatishwa tamaa sana kwamba sehemu nyingi ambazo wanataka kuwekeza kuna shida ya maji, umeme, miundombinu na shida nyingine mbalimbali.

Sasa tunaposema kwa jumla tu kwamba tutazame Mikoa mingine hii na hii mingine tuiache, nafikiri hii dhana si sahihi wala huu mtazamo si sahihi. Tutazame mtazamo ulio sahihi kwa kufanya utafiti na kujua hali halisi kama vile mahitaji ya

umeme na vitu vingine mbalimbali yanakuwaje kihalisi na kupanga mipango ambayo itaambatana na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio chetu katika Jimbo la Mkinga, kwa mufa mrefu sana Vijiji vingi vimetoa maombi na Mawaziri mbalimbali na Viongozi mbalimbali waliokuja wametoa ahadi kwamba wataweza kutekeleza au wana nia nzuri ya kutekeleza haya, lakini miaka nenda, miaka rudi haya yamepita bila hilo kuwezekana. Kwa wakati ule kusema kweli labda *TANESCO* ilikuwa ina matatizo, lakini sasa hivi tunaunda hii Taasisi maalum ambayo kazi yake itakuwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba maombi yaliyotolewa kwa muda mrefu hasa yale ya sehemu kama vile Vijiji vya Daruni, Gombero, Kwale, Mchinga, Mwakijembe na Kigongoi ambavyo vina rutuba kubwa sana na nafasi kubwa ya maendeleo yatasikilizwa.

Tunaomba Taasisi hii mpya iliyokuja isikilize maombi yetu, isisikilize maneno ya juu juu kwamba Mkoa wa Tanga, Wilaya zote za Tanga na Vijiji vyote vya Tanga vimeendelea, si sahihi. Naomba maombi yetu myasikilize na yafanyiwe kazi kama mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa kusema kwamba hii Taasisi inastahili nayo iwe na mfumo ambao una uwakilishi katika sehemu mbalimbali, isiwe tu katika Makao Makuu. Ni vizuri ikawa na uwakilishi Mkoani na Wilayani au ikawa na mfumo kama ule wa *TANROADS* ambapo *RCC* na Halmashauri zinakuwa na uwezo wa kuchangia na kuweza kuzungumzia maendeleo juu ya masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nashukuru sana kwa Muswada huu bora na ni matumaini yangu kwamba Muswada huu utapita na utafikia mafanikio yanayotakiwa kwa maendeleo ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja ya Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini kwa mwaka 2005.

Naomba nianze kwa kutoa rambirambi zangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kusini kufuatia kifo cha Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, Mbunge wa Rahaleo kwa wananchi na familia yake. Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu na niseme baada ya kuupitia, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kuchangia, naomba nianze na rai kwamba Sheria nzuri ya Nishati Vijijini itafikiwa baada ya kuwezesha kutatua matatizo makubwa

matatu na matatizo haya yanazikabili nchi zote zinazoendelea Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi hizo. Tatizo la kwanza, ni watu wengi sana kuendelea kutegemea nishati asilia kama vyanzo vya nishati kama kuni na mkaa. Hili ni tatizo kubwa kwa sababu licha ya matumizi hayo kuwa ni ya familia au kaya, lakini hata uzalishaji katika maeneo mengine unatumia chanzo hicho cha nishati kwa mfano, uchomaji wa matofali, ukaushaji chumvi na hata baadhi ya taasisi kwa mfano kiwanda pekee kilichopo Mkoa wa Kigoma cha Uvinza katika Jimbo langu bado kinatumia kuni katika kukausha chumvi. Sasa matumizi ya aina hiyo yana athari kubwa katika maeneo yetu na katika uchumi wetu kwa ujumla.

Tatizo la pili ambalo sheria nzuri itakuwa imelitatua ni uanzishaji na utekelezaji wa miradi ya nishati Vijijini ambayo haizingatii uwiano wa kijiografia na hili linasababisha matatizo makubwa sana kiuchumi na tofauti na ubora wa maisha kwa maeneo yale ambayo nishati au miradi ya namna hiyo haianzishwi. Sasa sheria hii itakuwa nzuri kama itarekebisha tatizo hilo la uanzishaji wa miradi isiyozingatia uwiano wa kijiografia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la tatu ambalo sheria hii ikifanikiwa kulitatua itakuwa imefanya kazi nzuri, ni kuondoa utegemezi wa *program* ambazo zinashauriwa na mashirika ya fedha duniani hususan Benki ya Dunia kwa sababu utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Garaware, nimeangalia kwenye *internet*, umethibitisha kwamba Taasisi hiyo ya Kimataifa ya Fedha miaka ya mwanzo ilikuwa inawekeza kwa kiasi kikubwa katika miradi ya umeme katika maeneo mbalimbali, lakini Taasisi hiyo hiyo kwa sasa inachangia au inawekeza kiasi kisichozidi dola bilioni mbili kati ya makadirio ya dola bilioni thelathini na nane. Kiasi hiki ni kidogo sana, ni sawasawa na asilimia tano tu. Kwa hiyo katika hali hiyo ni lazima sheria yetu ibadilishe mtazamo wa kutafuta wabia mbadala badala ya hao waliozoeleka.

Sasa hivi nadhani wote ni mashahidi kwamba Makampuni yanayotoka nchi za mashariki yanaonyesha kuwa na ubia wa kuaminika na mzuri katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Sote nadhani tunafurahi tunapoona jengo la Bunge linavyoendeshwa katika kujengwa kwake. Nina uhakika Makampuni ya Magharibi yangejenga kwa kiwango hicho, kasi isingekuwa kama tunavyoiona. Kwa hiyo nilifikiri ni vyema chini ya Sheria hii tuangalie uwekezaji Vijijini kwa kuangalia ubia mbadala badala ya huo uliozoeleka wa nchi za Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuonyesha matatizo ambayo lazima tuyaondoe ni vyema niseme kwamba natofautiana kidogo na wanaosema kwamba tuondoe utegemezi katika chanzo cha maji kama chanzo cha nishati kwa sababu inategemea tunazungumzia maeneo gani. Eneo la magharibi Mkoani Kigoma hususan katika Jimbo langu, kwa mfano, Mto Malagarasi, tafiti zilizofanywa na *TANESCO* zimethibitisha kwamba una uwezo wa kutoa kiasi cha *Megawatt* 80, sawa na kiwango kinachotolewa na Mtera au sawa na kiwango kinachokaribia kiwango cha Mtera na ule mto haujatumika katika utoaji wa nishati ambayo tunaihitaji katika ukanda wa Magharibi. Kwa hiyo nadhani itategemea eneo na eneo katika kusema kwamba chanzo hiki hakiwezi kutusaidia au vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Waziri alipotembelea Mkoa wa Kigoma, tulijadili sana suala la kujaribu chanzo hiki ili tuweze kupata umeme katika eneo lile na hasa tulizingatia chanzo kimoja cha maporomoko ya Igamba. Maporomoko ya Igamba kwa tafiti zilizofanyika kwenye Mto Malagarasi yana uwezo wa kutoa hadi *Megawatt* 45. Lakini tafiti zilizofanyika zilionyesha kwamba inawezekana kwa kuzalisha katika awamu ya kwanza zikazalishwa *Megawatt* nane na hatua mbili baadaye zinaweza kupandisha kiwango hadi *Megawatt* 28. Hatua ya kwanza ilionekana kukadiriwa kuweza kugharimu Dola milioni 13 za Kimarekani.

Sasa kiasi hiki nadhani kingepaswa kuwa katika uwezo wa kuweza kuwekezwa kwa sababu mahitaji ya *Megawatt* 28 kwa Mkoa wa Kigoma yataufikisha hadi mwaka 2025 kulingana na makadirio ya hao watafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa nadhani ni vyema Wizara ikaliangalia hili na tulifanya kazi kwa pamoja, kwa kushauriana na Waziri, mimi nikawa nimeuandikia Ubalozi wa Uchina kwa sababu Kituo chao cha Kusambaza Umeme Vijijini *(Centre for Rural Electrification)* cha Uchina walionyesha kwamba wangeweza kuangalia uwezekano wa kuendeleza mradi huu.

Sasa baada ya kuwaandikia wakanishauri niwasiliane na Waziri na tukawasiliana na kwa kweli natarajia atakapokuwa ana-*wind up* atanipa maendeleo na hatma ya mradi huu kwa kutumia ubia na hao Wachina chini ya Kituo hicho cha *Centre for Rural Electrification* kwa sababu hiki ndicho Kituo ambacho kina uhusiano na hii sheria ambayo tunaianzisha ya Usambazaji wa Umeme Vijijini na kwa jinsi ambavyo nimesema, ni vyema tukabadilisha mwelekeo wa ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika ubia na watu hawa hasa Kituo hicho kinachohusika na Usambazaji wa Umeme Vijijini, ungekuwa ni wakati muafaka kuwa na chanzo cha kufanyia kazi na mradi wa namna hii ungekuwa ni changamoto kwa miradi mingine itakayotekelezwa katika nchi hii chini ya mfumo wa namna hiyo. Kwa hiyo, nilidhani niliombe hilo ili Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, aweze kunijulisha ni hatua gani iliyofikiwa na jinsi gani ambavyo matarajio yanaweza kupatikana katika utekelezaji wa mradi chini ya Kituo hicho cha Usambazaji wa Umeme Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri kwa Muswada huu, nikitarajia kwamba ufafanuzi atakaonipa utanipa matumaini ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kushiriki katika mjadala muhimu. Lakini kabla ya kuzungumza lolote kwanza nami nitoe pole zangu kwa kifo cha

Marehemu Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Marehemu Paul Bomani, aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hawa wote mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala ulioko mbele yetu hapa wa Mfuko wa Nishati Vijijini wa mwaka 2005 kwa kweli ni mjadala wa msingi sana kwa maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania. Umaskini wetu wa Tanzania tunapimwa pamoja na kutotumia nishati ya umeme katika shughuli za maendeleo katika nchi yetu. Kumbe hili ni tatizo la msingi.

Katika mjadala huu imeonyesha wazi jinsi wengine asilimia 90 umeme umeshafika Vijijini, lakini maeneo mengine hata asilimia 0.5 Vijijini wala hawajui umeme ni nini. Kumbe hii ndiyo *desperate* ambayo hatuwezi tukaiacha na tukatunga sheria kama hii tukifikiri kwamba tunatimiza wajibu tu. Ni lazima tuone ni jinsi gani tutakavyoweza kuondoa *desperate* hii. Sehemu nyingine umeme umefika kwa asilimia 90, sehemu nyingine katika Mikoa yetu ni asilimia 0.5 wala pengine hata hiyo hatujaifikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umeletwa kwa nia njema kabisa, lakini wasi wasi wangu ni jinsi utekelezaji wake utakavyokuwa. Tuangalie sana utekelezaji wa sheria hii usije ukatuingiza katika matatizo yale yale wale walichonacho wakapata na wale wasiokuwa nacho wasipewe. Nitasema hili kwa kutoa mfano.

Mheshimiwa Naibu, Spika, tunasema tunataka watu waje wawekeze na hao watakaokuja kuwekeza watakuwa huru kutafuta ni mahali gani wanataka kuwekeza. Wale watakapokuwa wanawekeza watakuwa wanaangalia ni sehemu gani ambazo viwanda vinaweza vikashamiri. Watapeleka huko huko ambako umeme upo. Sehemu nyingine kama Rukwa, Kigoma, Lindi, Mtwara, Ruvuma kutabaki vile vile kama Serikali haitatafuta jinsi ya kuweza kuwabana hawa wawekezaji waweze kwenda sehemu hizo. Kama ilivyo, kwanza huu ndio wakati wa soko huria, sijui ndio soko holela watu watabaki vile vile tunalalamika na sheria hii tunayoitunga hapa itawasaidia watu wachache na watu wengine tutabaki katika mazingira magumu.

Suala la pili, tunapozungumzia juu ya umeme tunasema wawekezaji watapewa fedha kutoka kwenye Mfuko ili waweze kuwekeza kujenga vituo vidogo vidogo vya umeme ili waweze kusambaza Vijijini. Lakini upo umeme wa *Grid* ambao hautoshi. Kwa nini hawa wawekezaji na wao wakionyesha nia ya kutaka kuendeleza eneo fulani kuwekeza katika *rural energy* yaani kusambaza umeme Vijijini wakapewa fungu ili wa-*subsidize* gharama ya ule umeme wauchukue huo wa *Grid* waweze kuusambaza? La sivyo, umeme wa *Grid* utakuwa unatoka Kusini kama ulivyo unakwenda Kaskazini, Vijiji vilivyopo katika Mikoa hiyo visiweze kupata umeme kwa sababu *TANESCO* watakuwa wanasema sisi hatuhusiki na mwekezaji anasema katafute *source* yako ya *energy* ili uweze kueneza. Kwa mtindo huu hatutaweza kuvifikia Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie mfano kwa Urusi, mwaka 1922, Lenin aliposema nataka *Rural Electrification* tulete maendeleo. Yeye alisema tunataka umeme uende Vijijini na ndiyo maana maendeleo ya Urusi yalipatikana haraka na wakaanza

kupata maendeleo makubwa. Sisi leo hii karne ya 21 ndiyo tunazungumza sheria wala utekelezaji wenyewe hatujaanza, sijui kama tutakwenda namna gani.

Suala la tatu ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu *priority*. Maeneo haya tukiwapa watu waje watafute wao wenyewe wawekeze wapi bado, maeneo mengine yataachwa. Mimi nina umeme umepita katika Jimbo langu. Kila siku nimekuwa nikilizungumza na Mheshimiwa Waziri nimeshamwandikia barua anayo mpaka sasa bado hajaweza kunijibu. Umeme umepita katikati ya Jimbo la Kalambo toka Kijiji cha Katesha, Katuka mpaka umeingia Mjini Sumbawanga.

Nina Shule za Sekondari za Ulungu, Matai na sasa Msanzi, nguzo za umeme zimepita juu ya Shule za Sekondari hizo, wanaushangaa tu umeme umepita umekwenda kule. Ni namna gani umeme huu utateremshwa ili uweze kutumika pale Matai na ukiteremshwa Matai uende kusambazwa mpaka Kasanga uweze kuleta kichocheo katika Vijiji vya Mwambao wa Ziwa Tanganyika ili tuanze kusindika samaki tuweze kuwaletea watu wanaohitaji *protein* katika Miji? Hakuna lolote linalozungumzwa! Ukimwambia mwekezaji aje afanye hivyo, *TANESCO* wanaanza kuweka vizingiti umeme huo hautateremka.

Lakini umeme ule ukiteremshwa pale Matai ukapelekwa Mwage, Mpui, Laela na maeneo ya Mwimbi Vijiji vyote katika Jimbo la Kalambo na katika Jimbo la Kwela watapata umeme utakaowasaidia kuleta maendeleo. Kwa sababu wataanza kuweka vinu vya kukoboa na kusindika nafaka, wataanza kufanya shughuli ndogo ndogo na viwanda vidogo na baadaye kuingia kwenye viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala hili ukiliangalia na jinsi lilivyowekwa, anasema tukatafute *source* nyingine, maporomoko mengine tuwaambie watu waje wawekeze ndio waweze kutuletea ule umeme, wakati umeme ule wa *Grid* kutoka Zambia unapita pale pale. Sasa huu Mfuko utatusaidia vipi sisi ambao tayari umeme upo? Tunachohitaji ni umeme uteremshwe ili uweze kutusaidia katika maeneo yetu. Shule za Sekondari tunazozijenga; tunazo Shule za Sekondari sita hivi sasa lakini hakuna hata Shule ya Sekondari moja yenye umeme, lakini umeme umepita umekwenda kule. Ndiyo maana tunasema tunaomba jambo hili liweze kuzungumzika na kuona jinsi gani tunaweza tukafaidi au tukapata na sisi manufaa katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya uendelezaji wa umeme Vijijini haina utata wowote, lakini tatizo hili ni la kufumbia macho katika maeneo fulani na kufumbua macho sana katika maeneo mengine. Hili ndilo tatizo ambalo tunalilalamikia, tunasema Mheshimiwa Waziri sheria hii isije ikaegemea upande mmoja tu. Tunaomba maeneo ambayo ni *disadvantaged* kama Mheshimiwa Ndeka alivyozungumza hapa, jitihada anazozifanya lakini tuweze kupata umeme upande wa Magharibi ungeweza kusambazwa katika ukanda wote ukafika mpaka Bukoba ukashuka mpaka sijui Sumbawanga, umeme kutoka Kigoma kwa sababu *source* inajulikana.

Wafadhili wakiweza kuwa *approached,* wanaweza wakatusaidia sana kujenga mfumo wa umeme katika eneo hili. Ukijengwa mfumo huo, zile *sleeping giants,* lile ni

eneo ambalo limekaa halijaweza kutumika katika uzalishaji mali. Mawese, samaki sijui na vitu gani vyote hivi tukishaweza kupata umeme wa uhakika, nina uhakika kabisa Mikoa ya Rukwa na Kigoma inaweza ikachangia kiajabu sana katika maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Kuhusu suala la Bodi ambayo imependekezwa hapa, mimi sipingani na Bodi inayopendekezwa na Mheshimiwa Waziri, lakini hebu tuangalie uwakilishi wa Bodi hii ambayo inapendekezwa. Ni *bureaucracy* walioko Dar es Salaam katika Mawizara ambao wala hakuna mwakilishi yeyote kutoka kwa wananchi. Hili ni jambo la hatari! Wewe unataka kwenda kuwahudumia watu Vijijini, ni *Rural Electrification,* lakini wanaoshughulikia *Rural Electrification* ni Makatibu Wakuu wa Mawizara walioko Dar es Salaam. Watakaa pale wala hawatajali mambo haya. Ndiyo maana nasema, tuangalie sana. Halafu kitu kibaya sana ambacho kwa kweli kimenisikitisha, hebu tuangalie ukurasa wa 64 *paragraph* ya 28. Mimi *paragraph* ile imenitia wasi wasi na namwomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya kutosha.

Mimi nimezungumza juu ya *desperates* na *bureaucracy* ambao ndio wamewekwa kwenye Bodi hii, wanalipana *sitting allowances* nzuri sana, lakini uwakilishi wa wananchi wenyewe ambao wanataka kuhudumiwa hawapo humu. Hawapo kabisa! Halafu hapa wameweka kipengele cha kuwalinda hawa wakifanya makosa ya makusudi wasishitakiwe. Hebu someni *paragraph* anasema: *"An employee of the Agency shall not, in his personal capacity be liable in civil or criminal proceedings in respect of any act of omission done in good faith in the performance of his functions under this Act"*.

Mimi sikubaliani hata kidogo. Hii ni kulinda ili mtu afanye makosa makusudi. Waziri fulani ukimwambia nataka upeleke katika Jimbo langu umeme anasema, aah sheria inaweza kunibana, anasema tutakulinda kwa kifungu hiki. Hii ni hatari! Wale wengine wanaokosa wataendelea kukosa na wale mnaotaka wapate wataendelea kupata kwa kuwalinda kwa kifungu hiki. Wakifanya *omission* tena mnasema; aah, akifanya *omission in good faith, in good faith for whom*? Kwa nani? Mimi kweli nasikitika sana na naona kabisa si haki kwa sababu watalindwa watu fulani kwa sababu watu wamepeleka umeme mahali fulani, lakini watu wengine hawatalindwa kwa sababu hiki kifungu hakitawasaidia hata kidogo. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri utupe maelezo ya kutosha na sisi wale wengine tutalindwa na kifungu gani hapa? Kama mtu amefanya *not in good faith* mnamfanya nini? Tunataka maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia juu ya umeme. Mimi nasema hivi, umeme hata huu wa *Grid* hautoshi kwa sababu tumekimbilia kujenga *dams* zetu za maji kwenye vyanzo vya mito ambavyo ni vi-*dam* vidogo vidogo. Ukiangalia Kihansi ni *dam* ndogo, Kidatu watu wakiona wanafikiri kitu kikubwa lakini kitu kidogo sana ukilinganisha na Iringa *dam*, *Aswan dam* au na vitu vingine.

Sisi hapa *source of energy* tunayoitaka kutoka maji ni kutoka *Stigler's Gorge* tu. Kama hatutafanya hivyo, tutaendelea kuhangaika na umeme hautatosha katika nchi hii. Wenzetu unakuta wana *source* ya *hydro electricity power,* wana *atomic energy* au wana *thermo*, sisi tuna mkaa wala hatujautumia. Tumepata gesi, *VAT* iko pale pale umeme

unazidi kupanda bei, wala hatuna maendeleo. Mimi nasema hivi, Mheshimiwa Waziri tufanye *coordination* katika haya mambo. Tunaomba *VAT* iondolewe katika umeme ili tuweze kuwapunguzia bei wananchi. Bila kuondoa *VAT* hatuwezi tukafanikiwa.

Pili, katika hii gesi ambayo tumeipata ya Songosongo, tunaomba wawekezaji waletwe ambao wataanza kuuza majiko ya bei rahisi ya gesi na gesi ianze kusambazwa kwa wingi katika Miji ili tupunguze kutumia mkaa wa miti. Misitu inakwisha na tusipoangalia kweli tutafika mahali ambapo nchi itakuwa kame kabisa, kumbe lazima tufanye *coordination* ya shughuli zetu ili tuweze kuendelea.

Kuhusu masuala haya kupanga bei na kupanga *priority* ya miradi, ni lazima tuwe na chombo ambacho kitakuwa madhubuti ili kiweze kuangalia jinsi kitakavyo-*distribute* miradi hii *iende equally* na tusiiache tu iende holela. Tuige mfano wa *TANROAD* na Mfuko wa *Road Fund.* Tukiweza kuiga vitu hivi, *TANROAD* watatoa ripoti kwenye *RTC* katika Mikoa, *TANESCO* wanatoa ripoti zao wapi katika mambo ya *Rural Energy*, hakuna mahali popote wanapotea. Lazima tuwe na mahali ambapo Mikoani huko suala hili la umeme Vijijini litazungumziwa huko huko. Lakini tukitaka *TANESCO* ndio wazungumze au Wizara ndiyo izungumze au chombo hiki kizungumze Dar es Salaam, hatutafikisha umeme kwa wananchi wanaohitaji umeme huu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii. Naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii na mimi niweze kutoa machache niliyonayo. Lakini kwanza napenda nitoe rambirambi zangu kwa Hayati Balozi Diria na hayati Balozi Paul Bomani ambao kwa kweli Mungu amependa awachukue si kwa mabaya ila kwa nia ya kuendeleza hata huko kwa Mungu kwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafika mahali naogopa kidogo kutunga sheria ambazo zinaweza zikatuletea matatizo huko tunakokwenda. Tulipitisha sheria ya mafuta hapa, leo sheria hiyo imetugeuka kimekuwa ni kilio kila mahali, mafuta yanapanda bei kwa mahitaji ya wafanyabiashara. Sasa naona na hii hali ya kusema tuweke umeme rahisi Vijijini haiwezekani hata kwa ndoto tusiote ndoto hizo. Nani aende atafute vifaa alete ajenge iwe rahisi? Ni nani? Tusidanganyane hapa! Tuambizane ukweli ! Vitu hivi ni vizuri kuandika kama hadithi za Abunuwas, kujenga nyumba hewani lakini nyumba haionekani, iwe ndiyo kisingizio cha kuwafanya wengine wakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili lazima tuliangalie. Wizara ilitakiwa iandae taratibu za kuainisha aina ya umeme wa *biogas, solar* au upepo halafu na huu umeme wa *thermo* wa mafuta na huu wa *hydro* halafu igawe nchi hii kwa kadri ya mahitaji ya sehemu hizo. Kama ndugu zangu watani zangu Wasukuma hawa tunaweza kukawafanyia kwa wingi *biogas*; angekuwa na mipango hiyo tungesema itafanikiwa. Lakini kuleta *biogas* kama kule kwangu, mtu ana ng'ombe mmoja tu familia nzima, unategemea kweli kwamba atafanya *biogas* ya kuleta umeme kule? Hakuna!

Huu umeme wenyewe tunaosema ule wa sasa nina miaka sita naomba umeme katika Vijiji vya Iyula, Igamba na Waziri nimesema hata wakati wa bajeti nimemsimamisha anieleze mpaka sasa haupo, halafu mnasema umeme huo ndio utakuja kufaa. Utoke wapi sasa? Huo mpaka sasa haupo! Ni nyumba ya Abunuwas inapiga kengele juu huko watu wanafikiri ni ghorofa. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi ninasikitika kidogo, hivi leo tunasema Bodi iwe ya Makatibu Wakuu *(Permanent Secretaries)*, hivi jamani *Permanent Secretaries* wana nafasi hata ya kwenda kukaa kufikiria Vijiji huko, mtawapata wapi? Nyumba zao zina viyoyozi, usafiri wao ni sawa sawa, hawana matatizo na umeme. Leo yeye ndio awe *member* wa Bodi ya kusaidia wanavijiji wangu kule Ilomba, itatokea wapi hii kama si hadithi ya kuzungushwa ya Abunuwas hapa? Mimi nadhani mambo haya tunafanya tu ili kuridhisha watu kuwa tumeandika hadithi za kueleweka hapa watu waelewe iwe katika hali hiyo.

Vile vile, tulikuwa na utaratibu hapa wa *Agencies* za Wizara mbalimbali; zimefanikiwa wapi? Leo tunaanzisha hii, itafanikiwa wapi? Kama fedha zipo mimi ningekubaliana kama mngesema fedha sasa tuweke kama Wizara ya Ujenzi. Kila pato letu la mwezi la nchi tuweke kifungu au sehemu tunaweka kwa ajili ya barabara, wanasema bilioni moja, sasa tuweke angalau kwa ajili ya umeme huu wa Vijijini angalau nusu bilioni kila mwezi wa pato la nchi hii, liwekwe fungu hilo kwa ajili ya umeme wa Vijijini. Hilo tungekuwa na uhakika. Lakini hii ya kusema bajeti ije iwe na *seal* yake, hapa mimi nafikiri hii ni hadithi tunapakana asali kwenye midomo ili tuendelee kulamba wakati asali haipo. Hili nafikiri mimi nashindwa sana kuelewa kama litafanikiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Halafu ni lazima ndugu zangu tuielewe kwamba hivi tunataka kuendeleza Vijijini au tunaendeleza Mijini? Waziri alipokuwa anatoa maelekezo haya, amesema kwamba watatafutwa watu wenye uwezo hawa ndio watakaoshika miradi hii huko Vijijini kuendeleza. Hivi mnadhani mtu wa Dar es Salaam aende Nkansi akaanzishe mradi na umwambie ajenge mradi huo uwe wa bei ndogo, mtampata wapi huyo kama si hadithi? Kusema atoke mtu Dar es Salaam aende ajenge umeme kule Kigoma kwa bei nafuu! Leo mafuta yenyewe tunapitisha miradi mingine, ni kusaidia Miji mikubwa tu.

Mafuta Dar es Salaam ni nafuu kuliko kwingine huko tuliko Mbeya. Tunaumia na umeme, tunazidi kuumia, tutazidi kugandamizwa katika hali hii. Kama kweli fedha hizo za Serikali zipo, kwa nini wasifanye? Mnataka kuongezea watu ajira tu wapate ajira watu ambao wanaonekana ni *redundancy* wanatakiwa kuondolewa. Wameshindwa kutekeleza kazi zao ndio mnataka muwape kazi waendeleze kula na kutuletea matatizo! Mimi sikubaliani na hili kwa kweli. Afadhali tukubaliane kama fedha hizo zipo zifanye kazi wataalamu hao wawepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunafungua Shule tunasema eti tufundishe watoto. Hivi watoto hawa wanachukua masomo gani? Yale yale ya *arts* tu, Historia, Kiswahili na Siasa! Hivi hawa kweli ndio watakuja kuwa wataalamu wa Sayansi? Hakuna hata masomo ya Sayansi, hakuna hata *Chemistry, Biology, Physics* hata *computer* hakuna,

wanaofanya *computer* ni Dar es Salaam tu na Dodoma nako ni Mjini, kule Vijijini mambo haya hakuna. Shule tunajenga kwenye Kata, tunasema eti zitakwenda na tutaweka usawa katika nchi. Vitu hivi tusiwe tunafanya tu mradi tumepitisha kitu baadaye kinakuja kuonekana kana kwamba tuliopitisha hatukuwa tunaona mbele wala kufikiria. Tutapata matatizo makubwa kabisa na tutalaumiwa hata tukifa makaburi yetu yatabaki ni lawama kabisa katika dunia ya leo na ya kesho. *(Makofi)*

Mimi sioni sababu kwa kweli ya kusema kwamba eti tukubaliane hii iwe ndiyo utaratibu tunaokubaliana. Hivi kwanza kama tunataka tukubaliane, basi kazi hii ianze Vijijini; tusimame Mijini. Miji yote mikubwa ya Mikoa ingoje mpaka Vijiji navyo vipate. Kama tunakubaliana tufanye hivyo. Lakini sasa tunafanya hivi tunaongeza tu, tunasema lami bado zinajengwa, zinaharibika zinarudiwa hizo hizo huku hakuna. Nani atapeleka umeme Kamsamba hata barabara ya kupita haiko? Tutafanya hadithi zisizoeleweka hata kidogo!

Tunasema umeme ni kitu msingi kabisa kingetusaidia hata kuleta maendeleo, leo tunahangaika na njaa lakini nenda Rukwa kuna mahindi tele! Nenda Mbeya mahindi tele! Lakini tulikuwa na *NMC* walikuwa wanasagisha unga, mashine zile sasa haziko, umeme hakuna watu wanalia njaa na mwaka kesho itakuwa ndio kivumbi kabisa. Maana hakuna chakula. Chakula kiko katika sehemu chache, lakini sasa utakienezaje chakula hicho? Tumebaki kutangaza tu bei ya Mbeya viazi sasa Sh.7,000/= gunia; lakini Moshi Sh.20,000/= na kitu gunia la kilo 100, Mtwara Sh.30,000/= gunia. Hivi inatusaidia nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusifanye vitu tu ndugu zangu kama tunajaribu kuleta tu bughudha kwa watu. Maneno haya mengine yanauma, ni vizuri tuangalie. Mimi najua siwezi kufanya lolote peke yangu katika Muswada huu, basi na uende utakavyopita liwe ni lawama kwetu wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Halinga, kwenye orodha hii niliyonayo hapa bado wachangiaji 16. Lakini saba wa mwanzo kila nikimtaja anasema anajiandaa mpaka Jumatatu. Kwa hiyo nadhani walio wengi wangependa kujiandaa vizuri ili Jumatatu waweze kuchangia sawasawa. Basi, kutokana na hilo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha, niwaambie tu kwamba Serikali ambao wanatuletea Muswada humu ndani wanafikiri ni vizuri tukaendelea Jumatatu, kesho tuendelee na Semina. Muswada huu utamalizika siku ya Jumatatu. Hayo ndiyo mawazo ya Serikali. Kwa hiyo, kesho ni suala la Semina kuanzia saa 3.00 asubuhi mpaka jioni watakapoishia. Kwa hiyo, kesho kwa wale ambao walijiandaa kuuliza maswali wajiandae vizuri kuyaweka hayo maswali akiba kwa ajili ya siku ya Jumatatu.

Baada ya kutoa maelezo hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Siku ya Jumatatu Saa 3.00 asubuhi.

(*Saa 1.10 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu*

*Tarehe 18 Aprili, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*